# TAMBULISHO ZA CALVARY CHAPEL

MSINGI WA KANUNI ZA VUGUVUGU LA CALVARY CHAPEL



Kiswahili cha Kenya

CHUCK SMITH

# TAMBULISHO ZA CALVARY CHAPEL

MSINGI WA KANUNI ZA VUGUVUGU LA CALVARY

CHUCK SMITH

**Ku kyora**
Kenny Nek

**Hii ni kazi ya kushirikiana ya**
Calvary Chapel Kampala na Calvary Chapel Bible College Uganda

Dondoo za maandishi zote zimetolewa katika Swahili Union Version (SUV): Hakimiliki - 1952, 1997: kwa: Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya.

Huenda ikawa mwandishi alifanya mabadiliko fulani ya mkazo na aya, katika kazi ya utafsiri.

# FAHIRISI


Dibaji 1

Utangulizi: Mwito Katika Huduma 3

1. Muundo Wa Mungu Kuhusu Kanisa 9

2. Uongozi Wa Kanisa 17

3. Kuwezeshwa Na Roho 29

4. Kulijenga Kanisa Kwa Njia Ya Mungu 35

5. Neema Juu Ya Neema 43

6. Aula Ya Neno 53

7. Nafasi Kuu Ya Kristo 59

8. Kunyakuliwa Kwa Kanisa 67

9. Kwa Kuwa Mlianzia Katika Roho 93

10. Uwezo Wa Juu Wa Upendo 105

11. Kusawawizha 111

12. Safari Za Imani 119

# DIBAJI

Ni nini kinachotofautisha Calvary Chapel na makanisa yaaminiyo Bibilia na ya Kiinjili? Ni vizuri kutambua kazi ya kipekee ambayo Mungu ametenda katika ushirika wetu. Ikiwa kanisa la Calvary Chapel linafanana sawasawa na kanisa lingine lile, si ni heri tuyaunganishe yawe moja? Lakini kama kuna vitambulisho vinavyotofautisha, basi tuko na mahali pa kipekee na maalumu katika mpango wa Mungu. Bila shaka kunayo makanisa tunayo shiriki Imani na desturi zingine sawa nazo. Sisi sio waasi ila Mungu amefanya kazi ya ajabu ya kusawazisha au kuleta usawa katika ushirika wa makanisa za Calvary Chapel ambazo zinatutofautisha kwa sehemu mbalimbali.

Kuna wengi ambao wanaamini katika karama na huduma ya Roho Mtakatifu, lakini hawatilii mkazo mafunzo ya Bibilia, wala hawaitazamii Neno liwaongoze katika tajriba yao na Roho Mtakatifu. Kuna wengi wanaotilia mkazo mafundisho ya Neno la Mungu, lakini hawaamini kuwa karama za Roho Mtakatifu ziko na ni halali leo. Katika Calvary Chapel kunapatikana mafundisho ya Neno na moyo uliofunguka kwa kazi ya Roho Mtakatifu. Usawa au urari huu ndio unaofanya Calvary Chapel tofauti na kuifanya kubarikiwa na Mungu kwa njia ya kipekee. Kwa hivyo, ni muhimu kuelewa misingi ya ki-Biblia ambayo inaonyesha ni kwa nini mungu ameturuhusu kuwepo na kuzidikuongezeka na kukomaa.

Hivi si kusema kuwa Makanisa yote ya Calvary Chapel yanafanana. Kila mara nastaajabu jinsi Mungu anaweza kutumia miundo msingi na kuunda vitu vingine kutoka wao. Kila mmoja wetu ana macho mawili, pua, kinywa na masikio mawili, lakini bado vile tulivyo tofauti, mmoja kwa mwingine. Watu pia wana maumbile tofauti kihisia, lakini Mungu anampenda kila mtu. Anawapenda wale waonyeshao hisia kwa urahisi, na pia anawapenda walio goigoi na wasioonyesha hisia waziwazi. Kwa njia

ile ile, ili kila mtu aweze kuhusiana naye, Mungu alituumbia makanisa mbali mbali. Makanisa mengine huvutia wale wenye kuonyesha hisia nyingi kimaumbile, wakati mengine huwavutia wale wenye utulivu na urasimu. Mungu, akitarajia kufikia na kubariki watu wa kila aina, anaonekana kupendelea makanisa tofauti tofauti ili akutane na mahitaji za kila mtu, kutoka kwa wale wenye hisia za juu mpaka wale walio na ustaarabu na walio katikati. Kila mmoja wetu ana jukumu la kutimiza katika mpango huu wa Mungu, lakini sote tunatakiwa kutambua mahali petu katika mpangilio huu maalum. Hii ndio sababu ya muhimu sana kwetu kuelewa zile tunazoziita vitambulishi za Calvary Chapel. Na tukiona yanayotofautisha ushirika wetu, tutaweza kuelewa vyema mahali petu katika mwili wa Kristo.

# UTANGULIZI: MWITO KATIKA HUDUMA

*"Hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yeye aitwaye na Mungu…" (Waebrania 5:4*)

Kabla ya kutazama yale tunayoita "Vitambulisho za Calvary Chapel", wacha kwanza tushughulikie swala la mwito wetu na kujipeana kwetu katika huduma.

Kama kuna ishara moja ambayo ni muhimu zaidi kwa huduma inayonawiri, ni lazima kwanza kuwa na mwito –kusadikika katika moyo kuwa Mungu ametuchagua na ametuita tumuhudumie. Bibilia inatuambia tuwe na uhakika wa mwito na pia uchaguzi wetu.je Una uhakika kuwa Mungu amekuita katika huduma? Hili ni la muhimu sana kwa sababu huduma sio taaluma ili tuchague. Ni mwtio wa Mungu. Tutajuaje tumeitwa? Huduma kwa walioitwa sio jambo la hiari bali ni la haja. Kama vile Paulo alivyonena, "Ole wangu, nisipoihubiri injili!" (1 Wakorintho 9:16). Yeremia aliamua kuwa hatanena tena kuhusu Mungu sababu lilimtumbukiza katika shida. Aliwekwa korokoni na maisha yake yakatishiwa. Ndipo akaamua, "Ala, nimesalimu amri. Ninatoka mahali hapa." Na kusema, "Sitanena juu yake, wala sitanena tena kwa jina lake. Lakini neno lake moyoni mwangu ilikuwa kama moto uwakao, uliofungwa ndani ya mifupa yangu, nami nimechoka kwa kustahimili, wala siwezi kujizuia." (Yeremia 20:9). Inachukua mwito kama ule kwa sababu huduma sio starehe. Kuna wakati mgumu mno. Kama vile Petro aliandika "wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule misiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho:" (1 Petero 4:12). Tunatakiwa kuelewa kuwa hata ingawa Mungu amekuita katika huduma, mwito huo utajaribiwa zaidi. Una uhakika gani kuwa umeitwa na Mungu umtumikie?

Mwanzoni niliposikia mwito katika huduma, nilienda shule kujitayarisha. Nilitatizika shuleni kwa sababu nilitaka niache shule na kwenda na kuanza huduma. Nilifikiria, “Kuna ulimwengu uliokuwa unakufa bila Yesu Kristo, na ninakaa ndani ya darasa nikivipitia vitabu.” Nilikuwa na uhakika kuwa ulimwengu ulikuwa unaningojea. Sasa wakati nilipohitimu kutoka shuleni na nikapata jukumu la kwanza, unaweza dhania mshangao wangu wakati niligundua ya kwamba dunia haikuwa inaningoja. Ndipo sasa majaribu yakaja. kukawa kugumu kifedha na pia ki roho. Sikuyaona yale matunda niliyodhania nitayaona katika huduma – matokeo ya papo kwa hapo na ya kufurahia.

Na kulikuwa na matatizo mengi ya kifedha yaliyonilazimisha kutafuta kazi ya ziada isiyo ya kikanisa ili niweze kukimu mahitaji ya jamii na nikae katika huduma. Nilipata kuwa sikustahimilika na huduma. Kwa hivyo kwa miaka kumi na saba nilifanya kazi nje ya kanisa/huduma ili niweze kujisaidia. Sasa hii lilikuwa ngumu sana kwa sababu nilikuwa na uhakika kuwa nilikuwa nimeitwa kwa huduma. Na kuna wakati mwingine sikudhania nina mwito na kumsihi Mungu abadilishe mwito wangu. Nikasema, “Mungu niite niwe mfanyi biashara! Naonekana kufanya vyema na naona ni rahisi kupata pesa katika ulimwengu wa biashara. Na Bwana, ninaweza kuwa mwana biashara mwema Mkristo. Ningesaidia kanisa na nisaidie mtu katika huduma.” Lakini Mungu hangeniruhusu nitoroke mwito wake, hata ingawa kuna wakati nilijaribu kutoroka. Maono ya kumtumikia Mungu ilizidi kuwaka ndani ya roho yangu. Kwa hivyo inachukua mwito. Ni muhimu sana tujiulize swali hili rahisi, “Kwa kweli Mungu ameniita katika huduma?”

Pamoja na mwito huja haja yakujitolea. Kunazo mienendo kadhaa za muhimu mchungaji anaweza kuwa nazo zaidi ya kujitolea kwake Yesu Kristo. Niko vile nilivyo sio kwa sababu ya kujitakia makuu, au tamaa zangu au kwa mapenzi yangu. Niko vile nilivyo kwa mapenzi yake Mungu.

Nimeyapeana maisha yangu kwake. Na kama nimejipeana kwa Bwana, pia nitajipeana kwa Neno Lake na huduma, kuwahudumia wengine.

Ili tuwe na nia nzuri katika huduma tunatakiwa kukumbuka maneno ya Yesu, Aliyosema, "…Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote." (Marko 10:42-44). Ni vizuri kutambua kuwa huduma sio mahali pa kuhudumiwa, pa watu kukuletea, kukutukuza, na kukuheshimu kwa kuwa wewe ni mhuduma. Kwa ukweli ni pahali pa kuwahudumia watu hata hiyo ikimaanisha kwenda nje ya hali ya kawaida yako.

Juzi juzi nilihudhuria warsha au baraza ya wachungaji na nilishangazwa ufasiki ulikuwa na hao wachungaji. Walikwa wakichukua vikombe vya kahawa na soda katika chumba/mahali tulipokuwa na mkutano. Sasa, sikuwa na shida na hiyo, lakini wakati tulipomaliza mkutano, vifuniko vya chupa na vikombe vya kahawa waliacha hapo chini. Nilijipata nikizunguka nakuziokota vikombe na vifuniko, na nikisafisha ukumbi. Ninajua nini hufanyika wakati mtu anakuja na kugonga kikombe cha kahawa katika sakafu. Sikutaka kuacha ushuhuda mbaya kwa wachungaji wetu wa Calvary Chapel waliokuwa mle. Kweli watu wengi wanaona huduma kama mahala pa kuhudumiwa badala ya kuhudumu. Kufikiria, "Ni vizuri mtu aje kuokota nyuma yangu sababu mimi ndiye mhuduma," ni jambo lenye utata na pia ni kinyume na mtazamo wa Bibilia.

Kuna wakati nilikuwa nikiacha nguo pande zote za nyumba. Mwishowe bibi yangu, akasema, "Tazama sikukubali kuwa mtumishi wako! Ziweke juu wewe mwenyewe! Kwa nini nizianike nguo zako?" basi, nilitafakari juu ya hayo na kuona alisema ukweli. Haikufaa nitarajie anianikie nguo zangu. Hilo lilikuwa somo muhimu kwangu sijaitwa kutamalaki. Nimeitwa kutumikia.

Usiku ule Yesu alikuwa akila chakula cha mwisho cha jioni pamoja na wanafunzi wake kabla ya kusalitiwa, kukamatwa, na kusulubiwa, alichukua kitambaa na akajifunga kiunoni. Kisha alizunguka na kuwatawadha/kuwaosha wanafunzi wake miguu yao. Baadaye akawauliza, "Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea? Ninyi mwaniita, mwalimu na Bwana; nanyi mwanena vyema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na mwalimu, nimewatawadha/kuwaosha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana/kuoshana miguu ninyi kwa ninyi." (Yohana 13:12-14). Kama vile Petro alisema, kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake" (1 Petero 2:21). Neno "huduma" kweli umaanisha utumishi. Tumeitwa kuwa watumishi. Twahitajika tuwe watumishi, kwanza wa Bwana wetu, na pia kwa watoto wake.

Ni maoni yangu binafsi kuwa wale watu wanaovuta sigara, ndio walio na tabia iliyo chafu sana duniani. Wananuka na wanaacha uvundo popote waendeko. Ni rahisi sana kugundua mtu avutaye. Lakufanya nikutembea karibu na utainusa katika nguo zao. Unaingia katika nyumba ambayo watu wanavuta, ukingia ndani na upulize hewa ya nguo zao, itakugonga nje na harufu. Ni tabia chafu sana. Kuzidisha, wanatupa mabakio yao ya sigara chini mahali popote. Halafu wanakanyaga lile baki la sigara kwa kiatu ili kuuzima moto, na kuacha wamechafua mahali pa kupitia. Watu wajapo kanisani, mara nyingi wanakuja wakivuta na wanapokaribia kuingia kanisani, wanatupa chini sigara halafu wanaikanyaga. Nani anatakiwa kuokota kichungi cha sigara?

Nilipokuwa nikikua, nilifunzwa na mama nisiguse sigara au kichungi chake. Nilichukia sigara kiasi ya kwamba hadi waleo siwezi kushika moja bila kuhisi kama nimenajisiwa. Kila wakati nikiinama kuchukua kichungi cha sigara, kila dakika niishikapo kwa njia moja au nyingine, ulezi wangu tangu utotoni huchukizwa. Naichukia! Huku nikitembea katika uwanja/ardhi wa kanisa nakuyaona vichungi vya sigara, sipendelei jinsi

zinapokaa chini, kwa hivyo ni nazichukua. Lakini, nilijipata nikiziokota ilhali nilinung'unikia mwenye kuzitupa pale. Ningefikiria, "Mchafu, harufu mbaya, uvundo, kujifikiria, mzembe, watu wasio na akili."

Ndipo Bwana akanena na roho yangu. Akasema kwa urahisi, "Unamtumikia nani?" Nikasema, "Nakutumikia wewe, Bwana." Akajibu, "Basi achana na malalamiko yako hayo." Basi, usimtumikie kwa moyo ulio na uchungu. Usimtumikie kwa uchungu au chuki. Kama ninachukua vichungi vya sigara na kufikiria juu ya watu wachafu, basi nina uchungu nikilifanya hiyo kazi. Lakini, nikifikiria vizuri, "Bwana nitaweka eneo lako likiwa safi" ndipo ninagundua kuwa ninaweza kuziokota na kuzitupa bila chuki ndani, sababu ninafanya hiyo kwa Bwana - sio nipate kibali cha mtu yeyote, lakini kwako wewe, Bwana. Kama vile maandishi yanavyotwambia: "Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu." (Wakolosai 3:17).

Hamna mtazamo ulio muhimu zaidi katika huduma. Twatakiwa kutumikia kama ni Bwana sababu tutawapata watu kuwa chukizo. Tutawapata wasio na shukrani. Tutagundua kuwa wanatuhitaji, na mara nyingi ni walalamishi. Kwa hivyo, kama ukifikiria, "Ni lazima niwatumikie," hautafurahia. Lakini ukifiria, "Ninamtumikia Bwana," basi utaweza kuimudu. Huduma yetu yeyote ile, lazima tuifanye kama ni ya Bwana, tukijua kuwa kutoka kwa Bwana, utapata ujira wako.

Usitafute hongera za wanadamu. Usitafute watu wasema, "Ee, asante. Ee, una umuhimu sana kwangu mimi." Mara nyingi haitatokea. Nimetendea watu kazi tena na tena, na baadaye wakanidhulumu kwa sababu singeweza kuwafanyia zaidi. Unahitaji kuwa na mwelekeo wa kufanya jambo lolote kama ufanyiaye Bwana atakaye kutuza. Lazima uyaweke hayo akilini. Mimi ni mtumishi wa Kristo. Yeye ndiye Bwana wangu. Yeye ndiye atakayenilipa kwa huduma yangu. Natakiwa niwe na matazamo huo na niweke mtazamo ulio mzuri katika roho yangu ninapohudumia watu, nafanya lile Kwake.

Hatuna budi kujitoa kwake Yesu na kuwahudumia watu wake, lakini pia ni sharti kujitolea kwa Neno la Mungu. Ninaamini kuwa yeyote ambaye haamini kuwa Bibilia ni Neno la Ufunuo, lisilo na dosari, hana shughuli kuwa katika huduma. Ni jambo la kuhuzunisha kuwa hili lingetoa 50% ya wahudumu walio Amerika leo. Kwa nini ufunze kutoka kwa kitabu ambacho hauamini? Na kama unaamini kuwa Bibilia ni Neno la Mungu na ni Ufunuo, ni jukumu lako kulihubiri, halafu kwa njia zote kulijua. Jitolee kwa Neno hilo. Kama vile Paulo alivyomwambia Timotheo, “Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli” (2 Timotheo 2:15). Unaweza kufunzwa jinsi ya kusoma Bibilia, lakini funzo lenyewe halina mwisho. Hadi wa leo, naendelea kujitolea kwa Neno la Mungu na kujifunza neno la Mungu ili nijionyeshe aliyekubalika na Mungu.

# 1

# MUUNDO WA MUNGU KUHUSU KANISA

*"Juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu…"* (Mathayo 16:18)

Katika Calvary Chapel tunakiangalia kitabu cha Matendo ya Mitume kama muundo kwa kanisa. Tunaamini ya kwamba historia ya kanisa, kwa zaidi, imekuwa ya kuhuzunisha na msiba mkubwa. Mambo mengi ya kuogofya yametendwa katika jina la Yesu na chini ya uvuli wa kanisa.

Nilipoingia chuoni nilikuwa na wakati mgumu sana kwa sababu wakufunzi walipotambua ya kwamba nilikuwa Mkristo, wakaanza kuzua mambo ya kusikitisha kuhusu historia ya kanisa ambayo niliyafahamu vyema. Jibu langu lilikuwa, "Tazameni, msihukumu Ukristo kwa mifano isiyo mikamilifu ambayo tumeiona katika historia. Ihukumuni kupitia Yesu Kristo. Turejee yale aliyosema na kufunza. Alifunza, *'Heri wenye rehema maana hao watapata rehema.'* Una tashwishi na hayo? Alitufunza tupendane. Una tashwishi na hayo? Alitufunza ya kuwa ni heri kutoa kuliko kupokea. Una tashwishi na hayo?" Unaponena juu ya mafunzo ya msingi ya Yesu, hata wenye kushuku hukiri kuwa hawana tashwishi nayo. Walio na shida nao ni wale wanaojidai kuwa Wakristo na Matendo wanayoyafanya kwa jina la Yesu.

Katika kitabu cha Ufunuo, Yesu alizungumzia matatizo ya makanisa saba ya Asia. Hata siku hizo za mwanzoni, Yesu alihimiza kanisa litubu. Alionyesha makosa yaliokuwamo, mafundisho ya uongo yalikuwa yamenyemelea, na desturi iliyokuwa tayari imeanza kupanda mbegu za uozo kanisani. Kwa sehemu kubwa, kanisa lilikuwa limeshindwa hata katika karne ya kwanza. Maendeleo ya jumuia ya makasisi na kuanzishwa kwa mfumo wa kanisa ulianza mapema katika historia ya kanisa. Katika

kitabu cha Ufunuo, Yesu anaeleza kutoridhishwa kwake na mambo hayo yote katika nyaraka zake kwa makanisa.

Tuzingatie kuwa wakati huo kanisa lilikuwa bado halijatimiza miaka sitini tangu kubuniwa kwake. Kwa hivyo haikuchukua muda mrefu kabla ya kanisa kuharibiwa na kuwa si baridi wala moto hata Bwana alikuwa tayari kulitema kutoka kinywani mwake. Kanisa lilimtia kichefuchefu. Nikitadhamini historia ya kanisa sidhani kuwa mambo yamebadilika. Kanisa limeendelea kuharibika zaidi. Mambo ambayo Bwana ameyanenea makanisa saba ndiyo hiyo anayoweza pia kuyasema kuhusu kanisa ya leo.

Kwa hivyo huwezi kuangalia historia ya Kanisa na kupata muundo wa Kanisa, kama vile huwezi kutazama historia ya binadamu na upate kusudi/lengo takatifu la Mungu kwa binadamu. Binadamu ameanguka tangu mwanzo, kwa hivyo ukamilifu Mtakatifu hauonekani kwake. Ni sawa hivyo na kanisa. Huwezi ukapata ukamilifu Mtakatifu kwa kanisa kwa kuangalia historia yake.

Utakatifu ulio kamilifu unapatikana katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Hili lilikuwa kanisa lenye nguvu changamfu. Ni kanisa lililoongozwa na kuwezeshwa na Roho Mtakatifu. Ni kanisalililoleta injili duniani. Paulo, akiandikia Wakolosai miaka thelathini baada ya pentekosti alisema, “Kwa sababu ya tumaini mliowekewa akiba mbinguni; ambalo habari zake mlizisikia zamani kwa neno la kweli ya injili; iliyofika kwenu, kama ilivyo katika ulimwengu wote, na kuzaa matunda na kukua, kama inavyokua kwenu pia tangu siku mliposikia mkaifahamu sana neema ya Mungu katika kweli;” (Wakolosai 1:5-6). Waumini wa kwanza walionja kanisa iliyofanikiwa kuleta ya Injili ulimwenguni.

Tukitazama kitabu cha Matendo ya Mitume, naamini twaona kanisa kama Mungu alivyolikusudia. Mfano unaopatikana katika kitabu cha Matendo ni kanisa lililojazwa na Roho Mtakatifu, likiongozwa naye Roho

Mtakatifu na kuwezeshwa na Roho Mtakatifu. Ni kanisa ambalo Roho Mtakatifu alikuwa akiamuru na kuelekeza matendo na huduma zake.

Je, kanisa la mwanzo lilitegemea Roho Mtakatifu kwa kiwango kipi? Tunampata Roho Mtakatifu akisema, “Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao.” (Matendo 13:2-3). Paulo hutumia misemo kama “ilionekana ni vyema kwa Roho Mtakatifu na kwetu sisi.” (Matendo 15:28), na “wakajaribu kuenda Bithania, lakini Roho wa Yesu hakuwapa ruhusa.” (Matendo 16:7). Hawa ni watu walioongozwa na Roho Mtakatifu, wakaelekezwa na Roho, na waliotafuta mwelekezo wa Roho Mtakatifu.

Twaona katika sura ya nne ya Matendo vile wakati kanisa lilipokabiliwa na Matendo mazito, waliomba na kutafuta usaidizi nauongozi wa Mungu. Ndiposa Roho Mtakatifu alipowajaza upya na wakaendelea mbele wakihubiri Neno kwa ujasiri mkuu.

Kulikuwa na matumizi ya muhimu manne ya kanisa la mwanzoni. Matendo 2:42 yatueleza, “Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.” Misingi hii minne ni lazima iimarishwe wakati ushirika wa waaminifu unapokuzwa. Tukiongoza watu waendelee kuhudumu katika mafundisho ya Neno la Mungu, tukiwafunza mafundisho ya mitume, tukiwaleta katika ushirika wa mwili wa Kristo na kuumega mkate na wawe waombaji, tutashuhudia Mungu akitimiza kila hitaji.

Hakika Mungu alishughulikia kila jambo katika kanisa la Mitume. “Na Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.” (Matendo 2:47). Kamwe usisahau, sio jukumu lako kuzidisha kanisa. Hiyo ni kazi Yake. Kazi yako ni kuwalisha kondoo Wake, kutunza na kupenda kondoo na kuhakikisha ya kuwa wamelindwa vyema. Hii ni hakika hasa kwa kondoo wachache. Bwana akamwambia, “Vema, mtumwa mwema na

mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako." (Mathayo 25:21). Bwana hatakufanya kiongozi kwa wengi hadi uwe mwaminifu kwa wachache. Usiwe mara kwa mara unatafakari, "Ah, lakini ningependa kama tungekuwa na elfu hapa!" Au "Natumaini tungekuwa na elfu tano hapa!" Tumikia hao wanane au kumi ulio nao. Uwe mwaminifu kuwatumikia. Uwe mwaminifu ukiwalisha na Bwana atazidisha kila siku, kama apendavyo watakaookoka. Ukubwa wa kanisa sio shughuli yako wala haitakiwi kuwa.

Ukitazama orodha ya mambo katika kanisa leo, utapata lengo lao kuu ni kuzidisha kanisa. Kuna ratiba na mipangilio mingi na warsha zinazojaribu kukuonyesha namna ya kuzidisha kanisa lako. basi, ni rahisi sana. Hakuna haja ya kulipa $175 kwa warsha kutafuta jinsi ya kuzidisha hesabu ya washirika, waweke watu katika Neno.wafunze wawe watu wa kusli. Walete katika ushirika na kuumega mkate na utampata Bwana akizidisha kanisa kila siku na wale watakaookoka.

Jambo la busara zaidi nililofanya nilipokuwa bado najishughulisha na madhehebu ni kukoma kuhesabu idadi ya watu. Daima kanisa lilikuwa na ramani au chati imebandikwa kwa ukuta ikionyesha jinsi watoto walivyohudhuria kanisa leo, Jumapili iliyopita na mwaka uliopita. Kulikuwa na mazoea ya kutilia idadi maanani. Watu mara kwa mara walikumbushwa takwimu za uhudhuriaji. "Tukilinganisha na Jumapili iliyopita tuko wapi?" Na mwaka uliopita?" Kila mtu yuko wapi leo?" Kwa nini tumepungua?" Watu daima walishughulikia idadi. Mtego wa kuhesabu watu ni mtego mbaya sana ukikunasa. Usifanya hivyo! Waangalie waliomo na utambue, "Hawa ndio Mungu amewaleta niwahudumie leo." Wapatie mazuri yote, watumikie kwa moyo wote-wahudumie kwa uangalifu. Kama ulivyo mwaminifu, na unapodhibitisha uaminifu wako katika usimamizi, Bwana atakuletea watu zaidi uwatunze, uwalinde na uwahudumie. Kwa hivyo kuwa mwaminifu kwa wale Mungu amewaleta chini ya malezi yako.

Katika kitabu cha Matendo, twaona maswali yalizuka juu ya mpango wa ukarimu katika kanisa. Wajane wa waliofuata utamaduni wa Wakiyunani walihisi kama walikuwa wametengwa, na huo upendeleo ulikuwa umepewa wale wajane ambao walikuwa Wayahudi tangu mwanzo. Kwa hivyo walifika mbele ya mitume na malalamiko yao. Mitume wakasema, "Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudia kuwa watu wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno." (Matendo 6:2-4).

Kwa hivyo, Neno la Mungu lilipewa umuhimu wa kwanza katika huduma ya kanisa la mwanzoni pamoja na maombi. Walijitoa katika kufunza Neno la Mungu, kwa ushirika (koinania), kuumega mkate na kuomba. Na "Bwana akazidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." (Matendo 2:47). Wakati kanisa liko vile Mungu alivyokusudia, wakati kanisa litendavyo vile Mungu atakavyo kanisa litende, basi Mungu atatenda vile yeye atakavyo kutendea kanisa. Na atazidisha kila siku wale watakao kuwa wakiokolewa.

Watu wale Mungu alitumia katika kanisa la mitume ni watu waliojisalimisha au waliojitolea kabisa kwa Yesu Kristo, ambao hawakutafuta utukufu/sifa wao, lakini kutafuta kuleta utukufu/sifa kwake Yesu. Wakati umati ulipokusanyika kwenye tao la Suleimaini, baada ya kuponywa kwa kiwete, Petero alisema, "Enyi Waisraeli, mbona mnastaajabia haya? Au mbona mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi, au kwa utauwa wetu sisi? Mungu wa Ibrahimu na wa Isaka na wa Yakobo, Mungu wa baba zetu, amemtukuza mtumishi wake Yesu." (Matendo 3:12-13). Hata Petero, baada ya mwujiza mkuu, hangelichukua utukufu/sifa au sifa. Aliwaelekeza kwa Yesu, kumletea utukufu/sifa Bwana kupitia mwujiza uliotendeka.

Kumtukuza Mungu ndilo lilikuwa lengo kuu la kanisa la mwanzo. Watu ambao Mungu alitumia hawakujitafutia utukufu/sifa wao wenyewe. Hili ni jambo linalosumbua moyo wangu hasa tunapotazama jinsi watu siku hizi wanavyojikaza kufaulu, kujenga jina na kujiletea utukufu/sifa. Wanajaribu kujitokeza au kujionyesha mbele ya watu. Lakini Yesu alisisitiza – njia ya kwenda juu ni chini. "Na yeyote atakayejikweza atadhaliliwa; na yeyote atakayejidhalili atakweza." (Mathayo 23:12).

Kwa hivyo ishi kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Tafuta kuleta utukufu/sifa kwa Yesu Kristo na Bwana atakutumia. Ni ombi langu, mara kwa mara na kila siku, kuwa Mungu atanihifadhi kama chombo kinachoweza kutumika. Paulo alitamani vivyo hivyo. Aliandikia Wakorintho, "Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiria wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa." (1 Wakorintho 9:27)

Ufanisi au ustawi una hatari. Ikiwa Mungu atafanisha huduma yako, utakuwa taabani zaidi kuliko kama ungekuwa unasumbuka tu na unajikaza kufaulu, mbali sana na ushirika wa watu kumi pekee. Ni rahisi kuwa mnyenyekevu katika mazingira kama hayo! Hakuna nafasi kubwa yako ya utukufu/sifa. Lakini ufanisi unapoanza, ndipo hatari ya kweli hufika katika huduma. Watu wanapoanza kukukazia macho, ni rahisi kuteleza na kuanza kupokea sifa na pongezi. Hivi ndio njia fupi zaidi ya kukatiza upako wa Roho wa Mungu. Bibilia inasema, "Msiinue pembe yenu juu, wala msinene kwa shingo ya kiburi. Maana siko mashariki wala magharibi, wala nyikani itokako heshima. Bali Mungu ndiye ahukumuye; Humdhili huyu na kumwinua huyu." (Zaburi 75:6-7). Kuzidishiwa heshima yaonekana kama ndilo jambo la maana zaidi siku hizi. Wachungaji wengi hutumia nguvu wakati mwingi wakijaribu kuinua kanisa au kujiinua wao wenyewe. Lakini heshima, na heshima ya kweli, hutokana kwa Mungu. Kwa hivyo kuwa jitahadhari!

Kitabu cha Matendo hutupea muundo wa kanisa. Ni kanisa linaoloongozwa na Roho, lifunzalo Neno, na linalokuza/ sitawisha umoja - ushirika na koinania. Ni kanisa limegalo mkate pamoja na kuomba pamoja. Yaliyobaki ni kazi Yake Bwana na ataifanya. Na kila siku atazidishia kanisa watakaookolewa.

# 2

# UONGOZI WA KANISA

*“Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa.* (Waefeso 1:22)

Tunatambua ya kwamba Agano Jipya halielezei wazi upendeleo wa Mungu katika serikali za kanisa. Katika maandiko matakatifu, tunapata misingi tatu za mfano wa serikali za kanisa. Mbili kati ya hizi ziko katika Agano Jipya, na hilo lingine limekuwa kwa historia ya kanisa. Namna ya kwanza wa serikali ya kanisa ilikuwa imeongozwa na askofu au wasimamizi. Neno la kigiriki ni ‘episkopos’. Katika waraka wa kwanza kwa Timotheo 3:1, Paulo anaandika, “Ni neno kuamuliwa, mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema.”

Timotheo anatupea ustahili wa ‘episkopos.’ “Basi imepasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mpenda fedha, mwenye kusimamia nyumba yake vyema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu (yaani mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?). Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi.Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke lawama na mtego wa Ibilisi.” (1 Timotheo 3:2-7).

Kulikuwa na aina nyingine ya mwongozo uliowahusisha watu wenye karama ulioitwa ‘presbyteros’ au wazee. Matendo ya Mitume 14:23 inatwambia, “Na walipokwisha kuwachagulia wazee (presbyteros) katika

kila kanisa, na kuomba pamoja la kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini."

Agano Jipya linatufunza dhahiri uimarishaji wa askofu, ndio 'episkopos' na uteuzi wa wazee ndio 'presbyteros'. Hizi aina mbili za serikali, kwa hali yao, huwa kama zina mgongano. Je, kanisa latakiwa kuongozwa na askofu au na Baraza la wazee? Ni episkopos au ni presbyteros? Hizi tofauti zimekuwa wazi siku za leo hivi kwamba tuna madhehebu mbili ambayo yanayosimamia kila upande. Kanisa la maaskofu hufuata episkopos. Hili ni kanisa linaloongozwa na askofu. Pia kunayo presbyteros, kanisa linaloongozwa na wazee wenye cheo sawa ama la kiprotestanti? Ukweli kuwa aina hizi mbili za uongozi ziko, yaonyesha kuwa hakuna fundisho la wazi juu ya serikali ya kanisa. Aina zote mbili za serikali za kanisa zaweza kujitetea kwa njia inayokubalika huleta uhakika kulingana na mtazamo.

Kadri wakati unavyoendelea, aina ya tatu ya serikali ya kanisa imejitokeza ijulikanayo kama mwongozo wa ushirika. Siamini kuwa mwongozo wa ushirika ni mojawapo wa hiari kwa sababu hatuna mfano mwongozo popote katika Bibilia ambapo umati ulijitoza na kusema. Ni mwongozo wa ushirika uliokuja kila wakati na kusema, "Tunataka Mfalme atakaye tuongoza kama nchi zile zingine," wakitaka kwa nguvu yale hayakuwa mapenzi ya Mungu. Sijapata mwongozo wowote wa ushirika uliokuwa unawiri katika Bibilia. Katika Kutoka 16:2 tunasoma, "Na mkutano mzima wa wana wa Waisraeli ukawanung'unikia Musa na Haruni huko barani:" na katika Hesabu 14:1-3, "Mkutano wote ukapaza sauti zao wakalia; watu wakatokwa na machozi usiku ule. Kisha wana wa Waisraeli wakamnung'unikia Musa na Haruni; mkutanoni wote wakawaambia, ingekuwa heri kama tungelikufa katika jangwa hili. Mbona Bwana anatuleta mpaka nchi hii ili tuanguke kwa upanga? Wake wetu na watoto wetu watakuwa mateka; je! Si afadhali turudi Misiri?" Naye Musa akawajibu kwa Mungu katika Hesabu 14:27, "Je! Nichukuane na mkutano

mwovu huu uninung'unikiao hata lini? Nimesikia manung'uniko wa wana wa Israeli waninung'unikiayo." Ole wake mtu anayeongoza kanisa la umati. Kama Musa, mchungaji atapata manung'uniko na machafuko tu.

Hizi ndizo aina tatu za msingi wa serikali ya kanisa tunazoziona leo. Aina ya episkopos, presbyteros, na hii ya juzi ya umati.

Sasa tunapata katika Maandiko aina ya serikali ambayo Mungu alianzisha na kuunda katika historia ya wana wa Waisraeli. Ilikuwa chini ya utawala wa Mungu; watu walikuwa wanaoongozwa na Mungu. Katika mwanzo, nchi ya Israeli, ilikuwa imetawalwa na Mungu. Mungu alikuwa ameiongoza.

Hizi zilichichimia wakati waliochokeshwa na uongozi wa Mungu na kudai uongozi wa ufalme wakasema, "Tunahitaji mfalme atutawale. Tunataka tuwe kama nchi zingine." Samueli alisikitishwa na wao walipokuja kwake wakiuliza mfalme.

Hebu tuangalie namna ya serikali ya kanisa ambayo Mungu alikuwa anaitawala. Chini ya Mungu kulikuwa na Musa. Musa alimwendea Mungu kwa mwongozo na mwelekezo. Musa alikuwa kiongozi wa dunia aliyetambuliwa kama aliyepokea kutoka kwa Mungu mwongozo, mwelekeo, amri na sheria za nchi. Ilikuwa imetambulika na watu kuwa alikuwa kiungo chao kwa Mungu. Wao wakasema, "Angalia tunaogopa kumkaribia, kwani anatisha. Tumeona moto na radi. Wewe enda juu na uongee naye, halafu uje chini utwambie vile asemavyo na tutatii. Lakini hatutaki kwenda. Wewe enda tu." Kwa hivyo wakagundua ya kwamba Musa alikuwa akiongozwa na Mungu. Musa angeenda juu kupokea kutoka kwa Mungu, halafu angetelemka kushirikiana na watu.

Chini ya Musa, matakwa ya kibinafsi yalikuwa yanayumbisha. Foleni ya watu wenye mahitaji kila siku ilikuwa ndefu hadi kufikia upeo wa macho. Walifika kwa Musa kwa kila aina ya shida ili Musa afanye uamuzi

katikati yao na majirani juu ya mambo ambayo yalikuwa yametokea. “Waliomba jembe langu na hawakurudisha”. Na hili liliendelea siku nzima, kwa kila siku. Naye Yethro, baba mkwe akamwambia, “We, kijana, hili litakuua. Wewe hauwezi kushughulikia haya. Huwezi kushughulikia shida zote kwa sababu mstari wa watu unaokungojea uwaamulie in mrefu.” Basi Mungu akamwambia Musa awachukue wazee sabini wa Israeli na awalete katika hema ya mkutano. Akachukua Roho ambayo alikuwa amempa Musa na akawapatia ili watu wawe wanaenda kwao na hoja, mahitaji au malalamiko na wangepeana uamuzi. Na kukitokea mambo ambayo ni magumu kwao, wangemwendea Musa, halafu Musa angemwendea Mungu kupata uwazi wa jambo hili. (Kutoka 18:13-27).

Kwa nyongeza za usaidizi, Haruni na makuhani chini ya Musa, walishughulikia shida za ki roho za nchi, kama vile matayarisho na kutoa kafara. Chini ya Haruni na wazee kulikuwa na umati wa wana wa Israeli. Hii ndiyo aina ya serikali ambayo Mungu aliyowaekea Waisraeli.

Katika kanisa siku hizi tunaona umbo hili kwa njia ilioundika. Tunaona Yesu Kristo kama kichwa cha kanisa. Ni kanisa lake. Yeye ndiye mwenye wajibu. Kama wachungaji, tunatakiwa kuwa kama Musa, tukiwa na ushirika na Yesu na kupokea mwelekeo na mwongozo wake. Kama wachungaji tunatakiwa kuongoza kanisa hivi kwamba watu watatambua kuwa Bwana ndiye mwenye usukani. Baadaye, shida zitokeapo, tunaweza kuseman, “Naam, heri nimwombe Mungu kuhusu hayo.” “Wacha nitafute hekima ya Mungu kuhusu hii.” Heri tutafute mwelekeo kutoka kwa Mungu”. Pia kama Musa, katika kanisa tutakuwa na baraza la wazee ambao wataomba nasi na kusaidiana katika kutafuta mwongozo wa Mungu kwa kanisa.

Wacha nikutahadharishe. Kwanza, watafute wazee ambao ni waombezi, na ambao wanatambua ya kuwa Mungu amekupaka na kukuamuru kuwa mchungaji wa kanisa. Paulo alimtahadharisha Timotheo asimwekelee mtu yeyote mikono kwa haraka. (1 Timotheo 5:22). Kwa

hakika wajue watu vizuri kabla ya kuwapatia nafasi za uongozi. Ni kama ndoa, huwezi kusema unamjua mkeo mpaka mmeonana kwa muda kidogo. Wakati mwingi kuna mastaajabu. Pia ni muhimu kukumbuka kuwa shida hujitokeza wakati unapoanza kunawiri na kanisa linaanza kukua na kupata nguvu. Kuna watu wengi ambao wako na hamu ya mamlaka. Wanapoona kuna pesa katika benki, hapo ndipo wanaanza njama za kunyakua uongozi na utawala.

Ni vizuri kuwa na watu wanaomcha Mungu ambao wanatambua mwito na uamuzi wa Mungu kwako kama Mchungaji wa kanisa. Watu ambao watafanya kazi nawe na kusimama nawe kwa yale mambo ambayo Mungu anakuelekeza, kama mchungaji kuyatekeleza kanisani. Halmashauri nzuri ni jambo moja la muhimu sana katika huduma yako. Ninamshukuru Mungu kwa kuwa hapa katika Calvary Chapel Costa Mesa tumebarikiwa na wazee wakuu wa Mungu wanaohudumu katika halmashauri. Kwa kawaida tunawapata wanachama wa halmashauri kutoka kwa wanaohudhuria mkutano wa maombi wa Jumamosi au wanaokesha wakiomba. Tunawahitaji watu wa maombi. Tunawahitaji watu ambao wanamtafuta Mungu na mapenzi yake. Tumebarikiwa na watu kama hao katika baraza yetu na namshukuru Mungu kwa sababu yao.

Sasa, wazee wa kweli sio tu wale wakusema “ndio ndio,” lakini ni wale ambao wamejipeana kwa Roho Mtakatifu, Wao ni ngao na ulinzi kwangu. Kazi yao nikuunganisha waumini na uongozi wa kanisa. Waumini huwaletea kila shida wanayoiona. Na mara nyingi wao hujibu kwa urahisi, “Naam, hii ndiyo maadili ya kanisa, na hii ndiyo sababu tunafanya mambo jinsi hii.” Na mara nyingi hufika mwisho hapo. Mara nyinginezo katika mkutano wa baraza au halmashauri wataleta maswali mengi kama, "Hili limeletwa mbele yangu. Munaliona namna gani juu ya hili?” Na wakati mwingi ninajibu, “Kwa kweli sina wazo lolote. Wacha tumtafute Mungu.” Lakini kwa wakati mwingi nitawaruhusu wasuluhishe mambo hayo.

Wakati nilikuwa mchungaji mchanga Tucson, Arizona (kanisa langu la pili kuhudumu), kila mwaka tulikuwa na Mandari katika Mlima Lemon kila tarehe nne mwezi wa Saba. Sasa Tucson Julai nne, joto ilikuwa nyuzi 110 bondeni, kwa hivyo tungeenda juu ya mlima ambapo kulikuwa na baridi kidogo. Mbuga la taifa liloko mlimani Lemon lilikuwa na nafasi pana ya mandari. Mlikuwa na vyoo, maji, meza na pia kiwanja cha michezo. Palikuwa ni pahala pa ajabu pa kanisa kwenda kusherehekea mandari ya Julai nne. Na ulikuwa ni wakati mzuri wa ushirika. Siku moja kabla ya Julai nne, mmoja wa washiriki wetu alisema, “Niko na ekari moja ya shamba katika Mlima Lemon, badala ya kuchanganyika na umati wa kawaida ulioko mbugani hili la taifa, nafikiri kuwa lingekuwa jambo bora kama kanisa lingekuja na kufanya mandari yake katika shamba langu.” Tulisema, “Je una maji?” Naye akajibu “La.” “Je una vyoo?” “La, ni ekari moja tu ya shamba.” Pia ilikuwa maili tano kutoka mbugani hadi shambani mwake. Tena akaongezea, “Lakini ingekuwa jambo bora kuwa na siku ya kufunga na kuomba.” Sasa ni nani, kama mchungaji, anayeweza kuongea kinyume na kufunga na maombi bila kuonekana hakika asiye na Roho mbele ya watu?

Kwa hivyo kundi la watu kanisani lilijadiliana na wakakubaliana kuwa ni vizuri kuwa na siku ya maombi na kufunga katika lile shamba. Itakuwa ni sisi pekee na tutakuwa na wakati mzuri.

Kulikuwa na kundi lingine la watu kanisani waliosema, “Hatutawapeleka watoto wetu pahala pasipo na maji. Na ni nani atakayewaangalia watoto, na watakuwa wakifanya nini tunapofunga na kuomba? Hakuna vyoo. Mkienda mahali pale, sisi hatuendi." Nalo kundi la ki roho likasema, “Basi, mkienda mbuga la kitaifa pia sisi hatuendi.” Walionyesha hali ya ki roho ya kweli. Basi kukawa na utengano mkubwa.

Hapa mandarini yetu ya Julai nne, ambayo ilikuwa ya kufunga mwaka baada ya mwingine, ilikuwa inavurugwa na utengano huu. Pande zote mbili zikaja kwangu na kusema, “Chuck ni wapi tutafanyia mandari

yetu ya Julai nne?" Na kwa hekima kutoka kwa Mungu iliyozidi umri wangu nikasema, "Tutaachia bodi kujadili swala hili." Tulikuwa na mkutano wa halmashauri na ikaamuliwa kwa umoja twende mbuga la taifa. Basi, nikawarudia watu nikawaambia, "Halmashauri imeamua ya kwamba tutaenda kufanya mandari yetu katika Mbuga ya Taifa. Basi niliweza kuliendea kundi la ki roho lililotaka kufunga na kuomba na kusema, "Hilo ni wazo kuu na ingekuwa ni vizuri kushinda tukiomba na kufunga mchana kutwa. Yawezekana twende wakati mwingine sisi pekee na tutafunga na kuomba. Lakini kwa mandari wameonelea heri twende mbuga la Taifa."

Kwa kuwa halmashauri ilikata shauri, nilikuwa huru kuyaendea makundi yote mawili. Halmashauri ikawa kinga. Ni vizuri kuwa na kinga ya namna ile, ili watu wasikulaumu wakisema, "Ni mchungaji aliyefanya uamuzi na sijakubaliana na uamuzi wake." Halmashauri iliamua, na wakawa kinga yangu.

Naamini kwamba kifani cha Mungu, ni kwa Mchungaji kutawalwa na Bwana na kutambuliwa na watu kama aliyechaguliwa kama chombo na Mungu kuliongoza Kanisa, pamoja na halmashauri wakiongoza na kuelekeza. Kukamilisha haya, ndio jukumu la wachungaji wasaidizi. Wako hapo kuhudumia mahitaji ya ki roho ya watu kwa kila siku. Kukiwa na vijenzi kama hivyo, kutakuwa na serikali kuu ya kanisa mahali wewe kama mchungaji, hautakuwa na mahali pa mtu wa mshahara. Kuwa mtu wa mshahara ni hatari kweli wakati kanisa linaongozwa aina ya serikali kwa mfano wa Presbeteri, na Halmashauri wanaongoza Kanisa. Mchungaji ameajiriwa na Halmashauri na anaweza kuachishwa kazi na Halmashauri kwa desturi hiyo hiyo. Na aina kama hii ya uongozi, mchungaji huwa mtu wa mshahara.

Na haya pia ni sawa kwa uongozi wa umma. Mchungaji ameajiriwa na umati badala ya kuteuliwa naye Bwana aliye Kichwa cha Mwili. Hajateuliwa na Yesu Kristo, aliye Kichwa cha mwili, lakini amechaguliwa na Halmashauri ama na umati. Hapa tena, mchungaji anakuwa mtu wa

mshahara. Sidhani kuwa kuna yeyote awezaye kufanya kazi yake kikamilifu ikiwa kazi yake ni ya mshahara.

Naamini ya kwamba kila mtu anatakiwa kuwa shemasi. Huduma ya kusaidia ilikuwa ni asili ya utumishi wa ushemasi. Waliokuwa wanatakiwa kuangalia vyombo. Walitakiwa kuangalia haja za washirika na kuwasaidia wagonjwa. Jambo lililo mbaya zaidi ni kuanza kuwapa watu majina yenye vyeo kanisani, hasa majina ambayo yatatofautisha mmoja juu ya mwingine. Hilo ni jambo hatari.

Neno kuhusu kuhitimu ki roho kwa viongozi wa kanisa. Yuda alisema katika baraka, “Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu,” (Yuda 1:24). Mimi nimekosa lawama kama alivyo Kristo. Bado, ni kweli kuwa wote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu/sifa wa Mungu. Kama mtu yeyote akigundua kutokamilika kwake katika huduma, ni Paulo ambaye alisema, "Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nilipewa neema hii ya kuwahubiria Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika;” (Waefeso 3:8). Alikuwa akisema, “Mimi ndiye mdogo zaidi kwa wale ambao ni watakatifu. Mimi sistahili au sifai kuitwa Mtume sababu nilitesa kanisa la Mungu.” Amejisema mahali pengine, “Hii neema ilipatiwa kiongozi mkuu wa watenda dhambi.” Paulo aligundua yakuwa cheo chake ni kutokana na neema ya Mungu. Kama vile alivyosema katika I Wakorintho 15:10, “Kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo.” Aligundua kwa kweli katika Kristo hana dosari/hatia. Kwa hivyo sifa nzuri za Mchungaji au kiongozi wa kanisa ni “kuwa katika Kristo Yesu” na katika hii hali, asiye na kosa.

Naamini ya kwamba kama mtu hadumi ndani ya Kristo, lakini anatembea katika mwili, amekataliwa katika nafasi ya ‘episkopos.’ Kutembea katika mwili huonyesha maisha ambayo imekuwa desturi. Shetani amejitokeza kuharibu yeyote mwenye huduma inayonadhiri na ninaamini ya kuwa kila mmoja wetu anaweza kujikwaa. Kama vile Yesu

alimwambia Petero, “Na Bwana Akasema, Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako.” (Luka 22:31-32).

Naye Petero akajibu, akamwambia, “Wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe.” (Mathayo 26:33). Alikuwa akisema, “Bwana, hata wote wakikuacha mimi sitakuacha! Bwana nitakufa na wewe!” Ule ushupavu lazima ungeshugulikiwa kabla ajue umuhimu wa kumtegemea Roho Mtakatifu. Hili ni jambo ambalo lilitakiwa kushughulikiwa katika maisha yake. Na ninafikiria ni jambo ambalo linatakiwa kushughulikiwa katika maisha yetu. Wakati tunazo sehemu katika maisha zenye ushupavu, Bwana atatuonyesha kuwa peke yetu hatuwezi lolote. Kama vile Paulo alisema, “Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno njema.” (Warumi 7:18). Kwa hivyo wakati tunapofikiria kuwa sis ni wa maana tunakubalika na tumetengwa kando kuongoza, Bwana atatruhusu tukwazika ili atufunze kumtegemea kwa ujumla.

Wakati tunapoenenda katika mwili na kuamua kuwa tutaishi katika ule mwili, tunajiondoa katika sehemu za huduma. Lakini tukichukua neno “Asiye na hatia” kama vile ilivyo, labda inawezekana kwetu sisi kuondoka na tupate kazi ya kuuza magari. Naamini kuwa kutubu ndiyo funguo, na kukiwa na kutubu kwa kweli kunako msamaha na urejeshi unaanza. Lakini lazima kuwe na toba, hali ya kugeuka kabisa na kuachana na dhambi.

Nimechunguza kuwa yale makanisa ambayo yanafuata mwongozo wa wazee wakati mwingi hawamtazami mchungaji bali wanamtazama kama mfanyakazi wa kibarua. Maono yao ya mchungaji ni, “Mtu atakayefuata maagizo yao bila swali bora tu utafuata na kukubaliana nao. Lakini ukithubutu kufuata njia yako pekee, basi hio huwa ni hadithi nyingine.”

Kabla hatujaingia kwa Calvary Chapel nilikuwa nimeanzisha kanisa lenye kujitegemea huko Corona ambalo lilitokana na kusoma Bibilia kwa kikundi cha nyumba. Wengine wetu walioshiriki katika lile somo la Bibilia waliamua kuunda ushirika ambao waliuita “Ushirikiano wa Wakristo wa Corona.” Walifanya ushirika ili watu watoe fungu la kumi na fedha ili waanzishe Kituo cha Redio huko Corona ambacho umuhimu wake ni kunileta kwa hiyo Redio. Hawa watu walioanzisha huu ushirika ndio waliokuwa wakuu wa huo ushirika. Kwa hivyo tulianzisha kupeperusha kipindi kupitia redio na ambayo ilileta watu wengine.

Nilikuwa natamani kuacha hii aina ya ushirika au dhehebu nililoshiriki au nililousika na kujitegemea. Hawa watu walinikaribisha kuanzisha kanisa Corona ambalo nilifanya. Tukaanzisha Corona Christian Center. Lilikuwa limebarikiwa na Mungu, na bado nilikuwa ninaishi Newport Beach na kuendesha gari hadi huko Jumapili. Tungekaa huko siku yote halafu tungerudi Jumapili usiku. Alasiri moja ya Jumapili wakati jamii yangu ilikuwa nami katika chumba cha American Legion tuliokuwa tumekodi, niliamua kuweka viti kwa mviringo badala ya laini. Nilitoa mistari na badala yake mviringo mkubwa wa viti. Watu walipoingia usiku ule tulikaa kwa mviringo kama vile kwa Somo la Bibilia nyumbani. Badala ya kuimba nyimbo tatu za kidini kutoka kwa kitabu, tuliimba pambio tu. Niliwaongoza kwa pambio za kusifu. Baadaye tukawa na wakati wa maombi ambapo yalikuwa ‘maombi ya mwelekeo’ ambapo tungezua swala fulani na watu kuliombea katika ule mviringo. Baadaye nikafunza, kama nimekaa kitini pale tu bila urasmi, kama kawaida.

Nilihisi ilikuwa imeongozwa Roho na yenye nguvu sana. Namaanisha ilikuwa furaha tele! Kunao ambao usiku ule waliongoza katika maombi na hawakuwa wameomba mbele ya watu wakati mwingine katika maisha yao. Wengi wao waliguzwa na wakasisimuka siku ile. Walakini, Halmashauri wakakutana pamoja kwa mkutano spesheli wa halmashauri. Waliniita asubuhi iliyofuatia na wakataka kujua nilifikiria

nilikuwa nikifanya nini, na wakanieleza ya kwamba hawangetaka nirudie hayo tena. Wakati ule nikafikiria, “Naam, nilifikiria hii inaweza kuwa huduma maishani mwangu. Lakini haitakuwa au haiwezekani. Sitaweza kamwe kuwa chini ya vizuizi kama hivi. Ni lazima niwe mkunjufu kuongozwa na Roho Mtakatifu.”

Kwa hivyo wakati tulikuja Calvary Chapel na tukaweka sheria ndogo hatukutengeneza serikali ya Kipresibetero. Serikali iliyokuwa Calvary Chapel, ilikuwa inaegemea sana aina ya serikali ile ya Episkopos. Tuna amini ya kuwa muundo wa Mungu wa kanisa ni kuwa mchungaji aongozwe na Mungu akisaidiwa na wazee kugundua fikira na mapenzi ya Yesu kwa kanisa lake. Na hilo linatekelezwa na wachungaji wasaidizi.

# 3

# KUWEZESHWA NA ROHO

*“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidia wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.”* (Matendo 1:8)

Tambulisho lingine la Calvary Chapel ni kuhusu msimamo wetu kuhusu Roho Mtakatifu. Tunaamini kuwa kuna tajriba tofauti na ya kipekee ya kuwezeshwa na Roho Mtakatifu, katika maisha ya muumini tofauti na ile nyingine ambapo mtu anapookoka ROHO MTAKATIFU uingie na kutengeza makao ndani yake. Paulo aliwauliza Waefeso kama walipokea Roho Mtakatifu walipoamaini au tangu waamini. Haijalishi tafsiri utakayochagua, maandiko yanatueleza kuwa kuna tajriba fulani ya Roho Mtakatifu ambayo ni tofauti na ya kipekee kutoka na ile ya mtu aaminipo.

Wakati Filipo alipoenda Samaria akiwahubiria yesu, wengi waliamini na kubatizwa. Wakati kanisa la Yerusalemu liliposikia kuwa Wasamaria wamepokea Injili, waliwatuma Petero na Yohana, “Ambao waliposhuka huko, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina la Bwana Yesu.” (Matendo 8:15-16). Kwa mara nyingine, tunaiona tendo linguine la Roho Mtakatifu ambayo ni ya kipekee tofauti na mtu anapoamini.

Katika sura ya pili ya Matendo, wakati watu waliposema, “Waume na ndugu zetu, tufanyeje? Petro akawaambia, Tubuni na mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” (Matendo 2:37-38). Paulo aliokoka njiani kwenda Dameski, lakini Anania alimjia na akamwekelea mikono ili apate kuona na kupokea Roho Mtakatifu. (Matendo 9).

Tunaamini kuwa kuna tajriba/tendo la kuwezesha itokayo kwa Roho Mtakatifu ambayo ni ya kipekee na tofauti kutokana na tajriba/tendo la Roho mtu anapookoka. Tunaamini kuna uhusiano aina tatu kati ya Roho Mtakatifu na waumini, inayowakilishwa na vihusishi vitatu vya Kigriki – 'para', 'en', na 'epi'.

Katika Yohana 14, Yesu aliwaambia wafuasi wake, "Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele. Ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnatambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu." (Yohana 14:16-17). 'Nanyi' yaeleza juu ya uhusiano wa 'para', kutembea sako kwa bako. Ile 'en' katika msemo 'ndani yenu' ni sawa na kihusishi 'ndani' kama ataishi ndani yenu.

Tunaamini kuwa Roho Mtakatifu yuaishi na mtu kabla ya kuokoka. Ni Roho anayemjuza dhambi na anamshawishi kuwa Yesu ndiye jibu la pekee. Roho Mtakatifu kila mara anashuhudia kuhusu dhambi, kuhusu utakatifu na hukumu ijayo. Pia, tunaamini kuwa wakati mtu apokeapo ushuhuda wa Roho Mtakatifu, Yesu huondoa dhambi zake. Wakati yeyote anapomkaribisha Yesu moyoni mwake achukue ushukani na atawale maisha yake, tunaamini kuwa Roho Mtakatifu huingia ndani ya mtu huyo. Roho Yuko na kila mmoja wetu, ili kutuleta kwa Kristo, na tunapokaribia Kristo anaanza kuhudumu ndani mwetu.

Paulo alisema, "…hamjui ya kuwa mwili wenu ni Hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe? Maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu." (1 Wakorintho 6:19-20). Pia aliwaeleza Waefeso, "Tena msilewe na mvinyo ambamo mna ufisadi; bali mjazwe na Roho;" (Waefeso 5:18). Kwa hivyo, tunaamini kuwa kila mwana wa Mungu aaminiye na aliyezaliwa tena ana Roho Mtakatifu anayedumu ndani yake. Anahimizwa na Maandiko ajipeane mwenyewe akaongozwe na Roho Mtakatifu na akajazwe kila wakati naye Roho Mtakatifu.

Tunaamini pia kuwa Roho Mtakatifu ndiye humpa aaminiye uwezo wa kushinda dhambi na mwili. Tumehimizwa tuongozwe na Roho Mtakatifu, si mwili. Yule aongozwaye na Roho Mtakatifu hatatimiza dhahiri za mwili. Roho Mtakatifu ndiye hupeana nguvudhidi ya maisha ya kimwili/asili, akituwezesha kukabili asili yetu iliyoanguka. Ndiye nguvu maishani mwetu kutufananisha na mfano wa Yesu Kristo. “Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile utukufu utokao kwa Bwana aliye Roho.” (2 Wakorintho 3:18). Kwa hivyo twaona nguvu za Roho Mtakatifu ndani yetu tunapomkubali Yesu. Anaanza ndani yetu kazi ya kutubadilisha ili tuwe katika mfano wa Yesu Kristo.

Tunaamini kuwa kuna uhusiano wa tatu ambao aaminiye anaweza kuwa nao ambayo ni tofauti na umetengeka na husiano za kwanza mbili. Katika Matendo 1:8 tunaona ahadi hii, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu.” Uhusiano huu huwa wakati Roho Mtakatifu akija juu yenu. Neno ni ‘epi’ ni la Kigriki linalomaanisha ‘juu’ na ‘kufurika’. Napendelea tafsiri isemayo ‘kufurika’ kwa sababu naamini ya kuwa tajriba/tendo hii huruhusu Roho kutiririka kutoka maishani mwetu. Maisha yetu huwa sio tu kifaa kinachohifadhi Roho Mtakatifu, ila huwa chanzo cha mifereji ya Roho inayoadhiri ulimwengu unaotuzunguka. Ninaamini pia kuwa hiyo ndiyo kazi mwafaka ya Roho Mtakatifu. Wajibu wa kwanza ni ndani yetu na kuleta mabadiliko kwangu. Hii tajriba/tendo ya ‘kufurika’ huonyesha ushuhuda mwafaka wa nguvu na uwezo wa Roho Mtakatifu, unaotuwezesha kuwa mashahidi wafaao, wenye mazao kwa Yesu Kristo. Huu ndio ukamilifu na mpango wa Mungu, maisha yangu yawe kama kifaa atakachotumia kuufikia ulimwengu ulionizunguka kama Roho anapofurika na anapotiririka kutoka kwangu, na nguvu za Roho zinapojidhihirisha maishani mwangu.

Tunapata katika Agano Jipya kuwa Yesu aliwapulizia wanafunzi wake na kusema, “Pokeeni Roho Mtakatifu.” (Yohana 20:22). Naamini kuwa Yesu alipowapulizia na kusema “Pokeeni Roho Mtakatifu,” walipokea Roho Mtakatifu.

Wengine husema, “Sawa, lilikuwa tendo la kuonyesha mfano tu!” Nionyesheni Maandiko yanayofunza ya kuwa huu ulikuwa mfano! Kwa nini Yohana hakusema, “Sawa, alifanya jambo la kuonyesha mfano?” Hakuna ushahidi wowote wa Maandiko unaodhibitisha kuwa lilikuwa mfano tu. Naamini kuwa huu ndio wakati wafuasi wa Yesu walizaliwa tena kwa Roho Mtakatifu.

Ndipo Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kuwa wangojee Yerusalemu mpaka wapokee ahadi ya Baba ambayo alikuwa amewaelezea. “Ya kwamba Yohana aliwabatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku chache.” (Matendo 1:5). Pia akasema “Lakini mtapokea nguvu (dunamis), akiisha kuwajilia juu yenu (epi) Roho Mtakatifu,” (Matendo 1:8). Walihitaji kufurika kwa Roho ili waweze kumtumikia Bwana ipasavyo.

Tunaamini kuwa hii ndiyo tajriba Yesu alikuwa akiashiria/pelekeza katika Yohana 7 wakati wa, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama na akapaza sauti kwa mkutano wa watu akasema, “Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama kama Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.” (Yohana 7:37-38). Na Yohana, akifafanua akaeleza, “(Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.)” (Yohana 7:39). Huku ‘kuja juu ya’ kunaelezewa kama kufurika kwa Roho Matakatifu. Kungekuwa ni kufurika kwa aina gani? Kungekuwa kama maji yasio na kipimo yaliyo hai yakitoka kwa maisha ya aminiye.

Kwa hivyo ni jambo moja kujazwa na Roho na ni lingine kuwa na Roho akibubujika kutoka kwako. Kuingia kwa Roho kuna nguvu na uwezo. Walakini, ni lazima kuwe na kububujika kwa Roho kutoka kwa muumini ili aweze kuathiri maisha yangu na kuwagusa wale waliokaribu nami.

Yesu alituahidi mambo matatu kumhusu Roho Mtakatifu: Yumo pamoja nasi, Atakuwa ndani mwenu, na mtapokea uwezo/nguvu atakapokuja juu au atakapowafurikia. Roho Mtakatifu anasi kabla ya kubadilishwa. Ni Roho Mtakatifu anayenenea au anayehakikisha/ anayeshawishi ulimwengu juu ya dhambi, juu ya utakatifu na juu ya hukumu. Ni Roho Mtakatifu anayetuvuta kwa Yesu Kristo na anaashiria kuwa Yesu ndiye jibu la dhambi zote. Ni Roho Mtakatifu, baada ya kukuleta kwa Yesu, na unapofungua mlango, anaingia maishaini mwako na huanza kuishi ndani yako. Nguvu za Roho Mtakatifu anayeishi ndani yako anakuwezesha uwe na mienendo kama ya Yesu Kristo. Ni Roho Mtakatifu anakuwezesha kuishi maisha ya Kikristo na anayekufanya kuwa mfano Kristo. Roho anakufanyia yale wewe kwa uwezo wako, hauwezi jifanyia.

Kama Paulo alivyosema, "Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana aliye Roho." (2 Wakorintho 3:18). Pia alisema, "Au hamjui kuwa mwili wenu ni Hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu." (1 Wakorintho 6:19-20). Kupitia kwa kazi ya Mungu ya wokovu, mwili wangu umekuwa Hekalu la Roho Mtakatifu. Anadumu ndani mwangu. Ana uwezo wa kunibadilisha ili niwe kama mfano wa Yesu.

Ni mapenzi ya Mungu kuwa Roho atiririke kutoka kwa maisha yangu. Ni jambo moja kumimina maji hadi kipimo cha kikombe ni jambo linguine kumwaga maji hadi yafurike na kutiririka toka katika kikombe. Ni jambo

moja kuwa na Roho Mtakatifu amejazwa maishani mwako na ni lingine kuruhusu Roho Mtakatifu kutiririka toka maishani mwako. Hiyo ndiyo inahitajika katika huduma. Hata wanafunzi hawakuruhusiwa kuhudumu hadi walipo pokea 'nguvu mwendo' huo wa Roho Mtakatifu. "Hata alipokuwa amekusanyika pamoja nao, akawaamuru ya kwamba wasiondoke Yerusalemu, lakini wangojee ahadi ya Baba, ambayo mlinisikia habari zake kwangu." (Matendo 1:4). "Ahadi ya Bwana" ni utendakazi wa Roho Mtakatifu ni ile tajriba/tendo la 'epi' na ROHO akawajia. Ni ile tajriba ya 'epi' kule kuja juu ya kujazwa.

Hii tajriba huwa tofauti na kuokoka, lakini inayoweza tendeka wakati wa wokovu kama ilivyotendeka kwa Korineli. Petero alipokuwa akinena Roho akaja juu yao, 'epi' na wakaanza kunena kwa ndimi. Kwa hivyo mitume wakaamua kuwa ikiwa Mungu amewabatiza kwa Roho Mtakatifu, ni heri wawabatize na maji. (Matendo 10).

Kwa hivyo tunaamini kuwa kuna tajriba/tendo na Roho Mtakatifu ambayo ni tofauti nay a wakati mtu anapookoka na roho kuishi ndani yake. Wengine huiita kubatizwa kwa roho. Wengine huiita kujazwa na Roho Mtakatifu. Unaweza kujaza kikombe, lakini ukizidi kumwaga, itajaa itiririke. Hii ni tofauti na kujazwa tu na Roho. Ni kufurikwa na Roho Mtakatifu. Wengine huita kuwezeshwa kwa Roho Mtakatifu. Haijalishi utakavyo iita, la muhimu ni kuwa unayo. Tunaweza kubishana juu ya maneno ya kidini lakini tajriba inaelezwa kama kutoka kwa nguvu ya gharika ya maji yenye uhai kutoka ndani mwetu zaidi. Kwa hivyo, lolote utakaloliita tendo hilo si la muhimu. Swala ambalo ni lazima tutakubaliana nalo kuhusu tajriba hii ya muhimu sana katika huduma yako ni: JE UNAYO?

# 4

# KULIJENGA KANISA KWA NJIA YA MUNGU

*“Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu, asema BWANA wa majeshi”. (Zekaria 4:6)*

Kitambulishi kingine cha Calvary Chapel uliojitambulisha ni ule ukawaida pasi na kuweka sheria. Hatuingilii mambo ya Kristo kupita uasili. Hatujaribu kuwashurutisha watu kwa kimwili, hatupigi kelele tunapohubiri. Hii inatokana na imani yetu na jinsi tunavyomtumaini Yesu na Roho Mtakatifu. Tunaamini ya kuwa kama Bwana hataijenga nyumba, ni kazi ya bure kwa wanaoijenga, kwa hivyo utendaji wetu wa mambo kwa msukumo wa kiasili/mwili na kushurutisha kwake hakutafanya kazi. Kwa urahisi tunaamini katika kazi ya Roho Mtakatifu na wa Yesu Kristo ambaye analijenga kanisa kama vile alivyosema atalijenga.

Tukiwa na imani ya kuwa kanisa ni lake na yeye atalijenga na ya kuwa atafanya kazi yake, na kwa hivyo kwangu mimi ni kuwa mwaminifu. Langu tu ni kutazama kazi yake, na kwa hivyo shinikizo sio kwangu. Sipati masumbuko na shinikizo kwa sababu ya kazi ya Mungu maana sio jukumu langu. Sio kanisa langu, ni kanisa lake. Naamini ya kwamba ni ya muhimu kukumbuka hili kwa sababu ukijaribu kuubeba mzigo huu na wajibu huu utapata kuwa ni mzito kwako. Utajipata ukifinywa kuunda visingizio halafu utaanza kutafuta mipangilio uwezo na uerevu wako uskume watu na vitu. Na huo sio mtindo wa Calvary Chapel.

Hapo mwakani 1969 tulinunua ekari moja na nusu nyumba mmoja kutoka mahali tuliko, katika pembe la Sunflower na Greenville.

Kulikuwemo na shule ya kijijini mle. Tuliubomoa kutumia zile vifaa kulijenga kanisa hili ndogo kwa $40,000 pamoja na viti za kanisa. Baada ya miaka miwili, hili kanisa likawa ndogo. Tulikuwa na ibada tatu, tukiweka viti mia tano kwa wakati mmoja na magari ziliegezwa njiani kote mpaka kupita jengo la Los Angeles Times juu mpaka njia ile ya Ffreeway na fairview. Kwa hivyo tukajua ya kuwa lazima tungefanya kitu.

Wakati ule kipande cha shamba ambalo Cavary Chapel wanaomiliki hii leo likawa linauzwa. Mmoja wa Washirika kanisani alikuwa wakala wa shamba. Alikuwa moja wa ile kundi iliyokuwa imekuja pamoja na kununua hii mali ya ekari kumi na moja, kisha kuiuza na kupata faida. Walikuwa wanakisia bado lakini baraza la jiji la Santa Ana lilikataa matumizi yote waliokuwa wametarajia katika shamba lile. Kisha deni lao lilikua limefikia $350,000 ambayo ilikuwa juu ya hio shamba na ingeuzwa iwapo hawangeilipia. Walikuwa wamesita kulipa faida ya kila mwezi kwa ule dada mumiliki na mwishowe wakalipoteza.

Na Wakala wa shamba ambaye alikuwa katika ushirika wetu akaja kwangu na akaniambia ya kuwa ni vizuri tukilinunua lile shamba. Jibu langu lilikuwa, “Naam, ni jambo gani katika dunia tutakalofanya na ekari kumi na moja?” Naye alipendekeza ya kuwa tungeuza nusu yake. Halafu mwingine akasema tungepata shamba lile na $300,000. Nilisema, “Huu ni mzaha! Kwa nini, akubali $300,000 wakati alikataa $350,000?” Halafu akasema, “Kwa kweli najua mambo madogo kuhusu jinsi yule mwanamke alivyoishi. Alikuwa akilipa kodi kutokana na mapato ya faida ambayo alikuwa akilipwa na hawa jamaa. Kuwa sababu hawakuwa wanamlipa yeye hakuwa na pesa ya kulipa kodi. Amekaribia themanini na alihitaji pesa taslimu na nikafikiria kuwa kama tungempa $300,000 pesa taslimu angechukua.”

Nikasema, “Hilo ni jambo njema, lakini wapi duniani tungepata $300,000 pesa taslimu?” Akajibu, “Kama tunaweza inunua kwa $300,000, basi tunaweza kukopa nusu ya pesa hizo kutokana na akiba iliyomo.

Watakopesha asilimia hamsini ya milki, na tuna $110,000 kwa benki, na nitakopesha $90,000 bila faida kwa mwaka mmoja." Ndio nikasema, "Kweli hataichukua." Ndipo akasema, "Utanipatia ruhusa ya kuzipeana kwa jina la kanisa?" Nami nikasema, "Sawa." Baadaye akanipigia simu akasema, "Chuck, ameitikia." Fikira zangu kwanza zilikuwa, "Vyema, lakini sasa nifanye nini?"

Wakati ule Fairview Street ilikuwa tu imemalizika hadi Sunflower. Nilizoea kuendesha hadi kona la Fairview na Sunflower nikielekea kanisani. Ninapokuwa nimengojea kielekezi cha rangi ya kijani kibichi niingie kushoto, ningeangalia hii ploti kubwa na kuanza wasiwasi. Na nikafikiria, "Unajua, Mungu amekuwa mwema kwetu. Tumelipa deni lote na hatuna deni lolote. Tunayo $60,000 kwa benki. Tuna zaidi ya tunazotaka na mambo yanaendelea vizuri. Ni nini nawafanyia kundi hili la wafuasi kuwaweka katika deni pamoja na nguvu za kujenga hili? Ni nini hili nafanya? Kichwa changu kiko wapi?"

Ningejipata nikitiririkwa na jasho nyembaba nikajaribu kutafakari mambo. Halafu Bwana angenenea moyoni wangu na kusema, "Ni kanisa la nani?" Ningejibu, "Kweli ni kanisa Lako." Halafu angesema, "Kweli, kwa nini kuwa na wasiwasi juu ya fedha?" Nikafikiria "Kwani ni mimi?" Sio mimi nitafilisika. Bwana ndiye atafilisika, kwa nini niwe na wasiwasi? Halafu angesema, "Nani alisababisha haya?" Ningejibu, "Ni wewe. Wewe ndio uliowaleta. Ulileta shida ya mahitaji ya nafasi kubwa." Ndipo akanihakikishia hii ni kanisa lake na ni shida yake. Yeye ndiye aliyeleta hali ile ndipo nikapata tulizo mpaka wakati ule mwingine wa kukaa kwa ile kona na kulitazama lile rasilimali. Nikakaa kama kichwa ngumu, kwa hili lileendelea kwa muda fulani.

Uvumbuzi kuwa ushirika wetu ulikuwa kanisa Lake ulinipumzisha mzigo. Sikuwa na haja ya kubeba mzigo sasa na nilikuwa starehe. Ilikuwa kanisa lake kwa hivyo angelishughulikia. Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu." (Mathayo 16:18). Hakusema, "Juu ya

mwamba huu wewe utalijenga kanisa." Tunatakiwa kuelewa ya kuwa ni kanisa Lake na Yeye mwenyewe alisema atalijenga. Wakati Yesu alimwuliza Petro swali, "Je, wanipenda?" (Yohana 21:16). Petero alimjibu, "Ndiyo, Bwana, wewe wajua kuwa ninakupenda." Yesu hakuwa na kusema, "Nenda nje na kujenga kanisa langu." Yesu alimwambia, "Lisha kondoo zangu" - hivi ni kusema, "watunze na uwalishe." Ni kazi Yake kuliongezea kanisa, na pia ni kazi Yake kujenga kanisa. Na kazi yangu ni kupenda kondoo, kuwatunza, kuwalinda, kuwalisha, na kumwamini Bwana atajenga kanisa na kuongezea wale waliookoka.

Tumegundua ya kuwa kila unapong'ang'ana kupata, lazima utang'ang'ana kulitunza hicho ulichopata. Iwapo ulijisukuma sana ili ulipate, basi utakazana sana kuliendeleza. Kudumisha ni jambo ngumu iwapo ni mpango ulio katika mpangilio wa mwanadamu.

Zamani nilikuwa katika dhehebu na nilishurutishwa kulijenga kanisa. Nilikuwa nikitumia chochote kile kilichopendekezwa na kupatiwa. Kulikuwa na mwelekezo wa kukuza kanisa na mitihani kadhaa. Nilijaribu njia zote katika jitihada za kulijenga kanisa. Ndipo nilipojigundulia kwanza kuwa, ukisumbuka kupata lazima usumbuke kutunza. Kama ni kazi ya Bwana ameifanya na kuliongeza kweli hana budi kulifanya liendelee. Hali hii ya kusumbuka kutunza ndio huleta kudidimia kwa huduma. Na hii ndilo jambo la kukuua. Ndilo jambo ambalo hukuongoza katika upotofu wa kila namna. Kwa sababu umesumbuka kulipata hili kundi basi umejipatia kundi ambalo utasumbuka kulitunza, na hilo ni jambo ngumu sana.

Kote katika nchi yetu, tunaona makanisa mengi makubwa ambayo yametokana na mipangilio kabambe ya kujikuza. Lakini lazima uiendeleze ile orodha ya mambo. Lazima uwekeze zaidi na na kulishikilia au itaanguka. Vile vile, zile nguvu pamoja na mvutano unaotakikana kuliendeleza litakuua. Kuna makanisa mengi makubwa yanayopendeza siku hizi, lakini pia tunao viongozi ambao wamechoka, sababu ya kujikakamua kuendeleza lile ambalo wamelijenga.

Kujikakamua kupata haimaanishi kuingilia mtindo mpya za kukuza kanisa. Hili pia laweza kutendeka mahala kwenye msisimuko wa ki roho, ambapo kanisa lina kuzwa kwa msisimuko bandia wa karama za Roho Mtakatifu. Hapa tena unao wakati mgumu sana, sababu ukitumia ule msisimuko bandia kuwavutia wafuasi, kwa ukweli umeingia njia moja ambayo itaendelea kuwa ngumu jinsi unavyoendelea. ukiwavutia watu kupitia lile ambalo ni la kibandia hata ziwe za ajabu ajabu na kama huo ndio wajibu wako mkuu, basi lazima uendelee kutafuta zingine za kiajabu ili uwashikilie wale ambao umewavuta kwa njia hiyo.

Kuna jambo la kiuasili kwetu sisi wanadamu ambayo haijalishi tumepitia mambo za kiajabu vipi, kwa muda nadra tutachoka na kutaka jambo lingine geni – mtazamo mpya, mwelekeo mpya na mvutio mpya wa nguvu. Inaonekana kuwa inachukua nguvu nyingi zaidi kuweka usawa wa huu msisimuko, na kivutio.

Jambo la kutazamia: kujisifu kwangu kutumia mashua kulianza miaka mingi iliyopita nikiwa na mashua moja ya urefu miguu 12 pamoja na mashine ya Johnson yenye 25hp. Hilo lilikuwa jambo la kufana sana. Tulijifunza kukuea. Lazima kungekuwa na mtu wa kushikilia pua ilikuiweka mashua ikipaa juu kwa juu, lakini bado tulijifunza kukwea tukiitumia. Ilikuwa ni ajabu sana msimu wa kwanza wa kiangazi. Wakati baridi tulinunua Javelin hull, ikafungwa na chandarua ya glasi (faiba) na tukaiweka sawasawa. Ilikuwa na chombo cha miguu 14 jahazi bora kabisa. Lakini mtambo ule kidogo cha Jonhson 25hp hakingewezana na la Javelin hull. Ndipo tukanunua Mercury 55E ambalo lilikuwa bora zaidi. Hakuna yeyote alitakiwa kutokea nche kushika masikio kuliongoza. Na hili pia lilikuwa la ajabu. Lakini kufikia mwisho wa kiangazi mlikuwa na mashua zinatupita na ndipo tukaamua kuiuza Mercury 55E na kununua Mercury 75E. Lakini pia Javelin hull ya miguu 14 haingetoshana vyema na mercury 75E. nikafikiria, “Mashua za kukaa nje ni nzuri lakini nafikiri ni vizuri, lakini mashua ya kukaa ndani ni bora zaidi.” Ndipo tukanunua

Chevy 354. Utakomea wapi? Kwa bahati nzuri, nilikoma ingawaje bado kuna jambo kubwa na bora zaidi hapo mbele.

Haya ni sawa na ule mvutio unaoletwa na msisimuko wa ki roho. Unaweza sikia wengi wakisema “Asema hivi Bwana” na baadaye hayaleti mabadiliko yoyote au tofauti. Kwa hivyo lazima uendelee kufanya jambo jipya na geni na pia tofauti. Utafikiria kilele cha kuwa unacheka sana au kubweka kama mbwa au kuguruma kama simba. Tazama vile makanisa mengi yametoka kutoka mtindo huu hadi mwingine, na hata mwingine. Ni jambo lisilo la kukata kiu. Unamaliza kutumia yalio sawa hadi unaingilia yasio sawa. Lazima uendelee kutia mchuzi pamoja na mambo kadha wa kadha ambayo yataleta msisimuko ambao watu wanautumainia kwa hamu kuu.

Sisi wa Calvary Chapel hatuna msisimuko ule. Hatuko katika kufuatilia mtindo wa mwili/uasili au mtindo mpya ya kufurahisha watu na kuwavutia. Neno la Bwana ndilo tunalo amini, ndilo tunafunza, na ndio tunatarajia. Ndio msingi ambao tumejenga. Halichosheshi. Ndani yake hamna kilele cha kushindwa. Linaendelea mbele na mbele.

Kwa sababu hili, tumepumzika jinsi ya kustarehe ambayo yadhihirika katika huduma yetu. Ni kanisa Lake kwa hivyo hatuna budi kuchoka. Hatuna warsha za kukuza kanisa, ama jinsi ya kujenga kanisa la kuwavutia wengi, au jinsi ya kukuza mikakati ya miaka mitano. Nani ajuaye kama tutakuweko miaka mitano ijayo. Wacha tuhudumu leo!

Nilialikwa kunena katika semina ya viongozi mle Phoenix kwa kundi la wenye harakati na wanaokuza mipango ya jinsi ya kukuza kanisa kwa karne mpya. Watu wakuu wengi walikuwa katika semina hii wakikuza mikakati. “Ni jinsi gani tutaweza kushughulikia mahitaji yajayo na tukuze mikakati ifaayo ya kanisa?”

Naam, nilimkasirisha kiongozi mkuu kwa sababu nilisema, “Nina philosophia hii, 'Kama halijavunjika usijaribu kulirekebisha.'” Mungu bado anaendelea kubariki mafunzo ya Neno lake, kanisa linaendelea kukua, Bwana anaendelea kuongezea kanisa kila siku, na anayeheshimu Neno lake kama vile alivyosema atafanya. Ninarithika ya kwamba kama Mungu anabariki Neno lake, nitaendelea kufunza hii Neno. Kwa nini nibadilike? Kama kuna siku itafika ambapo hiyo halitafanya kazi, basi Neno la Mungu limeshindwa. Sasa kwa nini tulifunze?”

Hata hivyo yule kiongozi mwelekezi alikasirishwa sana na jambo hilo, na baadaye mchana kutwa tulikuwa bado twajibizana kuhusu hiyo jambo. Jambo la kufana zaidi sijawai itwa tena kunena katika warsha zile za ajabu.

Ninapata kuwa ninapomalizia Agano la Kale, nina njaa na tena niko tayari kwenda kwa Agano Jipya. Ninapomaliza na Agano Jipya ni jambo la kufurahia kurudi katika kitabu cha Mwanzo katika Agano la Kale. Inaendelea kukujenga kila wakati unalipitia. Unajifundisha na kunufaika zaidi. Unaimarishwa, na pia watu wanaimarishwa. Neno halizeeki. Na pia haligandi. Halifikii mahali ambapo linahitaji utafute njia mpya za mtazamo au uzoevu. Neon litabakia ni Neno la Mungu, ambalo ni hai na lenye nguvu na linahudumia roho za watu.

# 5

# NEEMA JUU YA NEEMA

*“Maana ni vizuri moyo ufanywe imara kwa neema...”* (Waebrania 13:9)

Calvary Chapel inatambulika kwa msimamo dhabiti katika maudhui ya Neema ya Bwana. Tumetambua ya kuwa pasipo neema ya Mungu hamna mmoja wetu angepata nafasi. Tunahitaji neema ya Mungu katika maisha yetu. Twaihitaji kila siku. Tumeipitia na tumeokolewa na hiyo neema kila mmoja. Na pia tunasimama katika ile neema. Tunaamini katika upendo na neema ambayo inatafuta kuwarejesha walioanguka.

Kuna makanisa mengine ambayo kamwe neema ya Mungu haipatikani. Mara nyingi ukatili usiobadilika wa Kisheria kwenye msimamo na mwongozo wa kanisa ambao hauruhusu toba na urejesho. Utastushwa na kushangazwa na msimamo niliochukua kwa sababu ya kutaka urejesho kwa walioanguka. Kila wakati nimwonapo mtumishi wa Mungu mwenye kipawa ameanguka katika ushawishi wa adui, ninamkasirikia sana Shetani ambaye anatafuta jinsi ya kuwaibia watumishi wetu.

Tumeuchukua msimamo dhabiti kuhusu neema. Tunaamini kuwa Bibilia inafunza kuwa Mungu ni mwingi wa neema. Hii ndiyo tabia/mwenedo wake mkuu katika uhusiano wake na mwanadamu. Kama angekuwa sio Mungu wa neema hakuna hata mmoja wetu angepata nafasi yoyote! Sote tunahitaji neema na rehema ya Mungu. Kila wakati ninapopsali, simuombi Mungu haki, isipokuwa nikimwombea mtu mwingine. Kila wakati ninapojiombea ninakuwa ninaomba, “Neema!” au, “Rehema Bwana, nirehemu! Nihurumie! Mtendee haki huyo mtu ambaye amenitendea mabaya, lakini Bwana, mimi nahitaji huruma.”

Ni jambo la kustaajabisha kuwa, baada ya kupokea rehema na kupokea neema, Bwana anatuonyesha jinsi tunavyohitajika kuonyesha neema na rehema. Alisema, "Heri wenye rehema maana hao watapata rehema." (Mathayo 5:7).

Inafurahisha kwamba Yesu anaonekana akilinganisha msamaha na jinsi tunavyopendelea kusamehe. Hii ni wazi katika ile inalojulikana kama Sala ya Bwana. Mwisho wa huo muundo wa maombi, anatilia mkazo jambo moja na hili ni ombi ambalo tunaloomba juu ya kusamehe. "Bali, msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu." (Mathayo 6:15).

Yesu alipeana methali ambazo zilishughulikia umuhimu wa kusameheana. Katika Mathayo 18, tunaona Bwana ambaye alimsamehe mtumishi wake deni la dola millioni kumi na sita. Lakini huyo mtumishi alienda kwa mtumishi mwenzake aliyekuwa akimdai dola kumi na sita pekee na akafanya awekwe katika gereza la wenye deni. Yule mwajiri alimwita mtumishi wa kwanza akamwuliza, "Ulikuwa na deni langu ya pesa ngapi? Na si nilikusamehe? Na kwa nini nimesikia kuwa umemtupa mjoli kwa jela? Alimkemea na akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote." (Mathayo 18:23-35).

Kama tumesamehewa kwa wingi, kwa kweli inatupasa tusamehe. Kama tumepokea neema ya Mungu, tunatakiwa kudhihirisha hiyo neema kwa wale walioanguka. Nahitaji neema ya Mungu kila siku. Ninasimama kwa neema ya Mungu. Nimeokolewa kwa neema sio kwa matendo. Ndio utukufu/sifa ukamrudie Mungu kwa yale ametenda. Siwezi kujisifu kwa yale nimetenda. Hakuna lile ambalo nimetenda. Sio kwa matendo ya haki bali ni kwa neema, tumeokolewa.

Hii ndio funzo kuu tunayopata katika Agano Jipya na kwa hivyo ni funzo ambayo tunatilia mkazo. Vitabu vya Warumi na Wagalatia vinadhihirisha wazi, kwa sababu zinaleta wazi neema ya Mungu na

kufanywa haki kwa imani. Hii inasimama kinyume na utakatifu wa kibinafsi ambao huja kwa kutenda na kufuata sheria.

Tunaamini katika kuwatafuta na kuwarejesha wale walioanguka kama vile Paulo alivyowafunza Wagalatia, "Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Roho mrejesheni upya mtu kama huyo kwa Roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe." (Wagalatia 6:1). Namshukuru Mungu kwa neema ambayo nimepokea, na nikiwa nimepokea neema hii ya Mungu, nataafuta niipeana kwa wengine.

Ninamkasirikia Shetani wakati ninaposikia kuwa mhuduma mwenye kipawa ameanguka. Wale ambao wana nguvu za kipekee na karama za Mungu wanaonekana kama ndio lengo maalum la Shetani. Sitamruhusu shetani apate ushindi. Ninajaribu kuwarudisha kwa ufalme wa Mungu ili wakatumie karama zao kumtukuza Mungu.

Nimewarudisha watu wengi sana katika maisha yangu. Hili ni jambo ambalo napenda kufanya. Ninapenda kuchukua wale walioadhirika na kutengeneza kitu cha kupendeza kutoka kwao. Nina gari aina ya 1957 Ford Skyliner. Naam, kama ungeliona wakati nilipolipata kwanza lilionekana kama lilikuwa tayari kutupwa sehemu la takataka. Lakini utoshelevu ulioko ni kuchukua kitu kama hicho, utumia wakati wako na kuifanyia kazi, kulitawanya vipande vipande, kulisafisha na kuondoa kutu, kulipaka rangi na kufunga pamoja kila sehemu na kulipaka rangi na halafu mwishowe unapata kitu kizuri na kinachovutia, kinachotokana na kitu kilicho kuwa kimeharibika. Kunayo furaha na kutosheleza. Pia napenda kutenda hivyo na nyumba zilizozeeka. Binti yangu kila mara hununua vyumba zilizozeeka na zinaharibika na halafu anasema, "Baba njoo." Napenda kuchukua hivi vyumba vilivyozeeka halafu ninavitengeneza kuwa vitu vya kuvutia, vya kisasa na vizuri. Na hayo pia yanaonekana katika maisha ambayo Shetani amevuruga.

Napenda kuchukua, kuunda upya na kuyajenga maisha ambayo yameharibika. Watazame watumishi wengi wa Calvary Chapel, maisha yao yalikuwa yameharibika kabisa. Lakini tazama vile Mungu amewarudisha, na tazama utajiri na thamani ambayo inajitokeza katika maisha yao. Ni kazi nzuri ya Mungu leo kuona wale ambao ulimwengu umewatupa kama bure ukiwaona wanabadilika na kuwa vyombo vya heshima.

Tunaamini kuwa kama tumesamehewa twatakiwa kusamehe. Kwa kuwa tumepokea rehema lazima tuonyeshe rehema. Tumepokea neema, lazima tuonyeshe neema na hii ni jambo la umuhimu sana kwa huduma ya Calvary Chapel.

Katika Injili ya Yohana, sura ya nane, kuna hadithi ya kusisimua sana. Yesu alikuja kwa hekalu, na katika mstari wa pili, alikaa chini kufundisha. Papo hapo, mafundisho yake yalisumbuliwa na vurugu. Kulikuwa na kilio na kelele. "Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati. Wakamwambia, 'Mwalimu, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini.'" (Yohana 8:3-4).

Maadui wa Kristo walikuwa wakijaribu mara kwa mara kuleta tofauti kati ya mafundisho ya Yesu na Musa. Watu, kwa kawaida walimtazama Musa kama chombo kilichowaletea sheria ya Mungu. Hakukua na swali kuhusu mamlaka ya Musa. Alinena kwa niaba ya Mungu.

Kama Yesu angesema neno ambalo lingehitilafiana na sheria ya Musa, basi Yesu hangekiri kutoka kwa Mungu. Hilo ndilo lilikuwa jambo kuu kuhusu talaka. Walimuuliza Yesu kama mtu anaweza kumtalaki mkewe kwa sabau yoyote? Naye Yesu akawajibu, "Nami nawaambia ninyi, kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini." (Mathayo 19:9). Walimjibu kwa kusema Musa aliwaambia wangewapatia

talaka kwa kuwapa karatasi ya talaka. Walifikiria walikuwa wamemnasa Yesu. Naye Yesu akaenda nyuma ya Musa na kusema hapo mwanzoni mambo hayakuwa vile. Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo zao, aliwaruhusu muwape wanawake karatasi ya talaka, lakini hapo mwanzo mambo hayakuwa hivyo.

Hapo tena walikuwa wanajaribu kumnasa kupitia torati. "Katika torati Musa aliamuru kuwapiga kwa mawe wanawake namna hii, nawe wasemaje?" Haya walisema, wakimjaribu ili wapate sababu ya kumshtaki. (Yohana 8:5-6). Hili lilikuwa jambo la kawaida. Lakini Yesu hakusema lolote. Naye akainama, akaandika kwa kidole chake udongoni.

Sasa, ni nini aliandika kwa udongo? Mimi sijui. Pengine aliandika, "Mwanamume yuko wapi?" Walisema. "Walimfumulia katika uzinzi." Kweli hawangemshika kwa uzinzi bila kumshika mwanaume pia? Kulingana na sheria ya Musa wote wawili walitakiwa wapigwe mawe. Kwa hivyo kama walifuata sheria ya Musa pia wangemleta mwanaume. Pengine mwanaume alikuwa rafiki na wakamwachilia aende. Kwa kweli haikuwa haki."

Maadui wa Yesu walighadhabika. Alikuwa tu anaandika chini kama kuwadharau. Ndipo wakasisitiza swali. Mwishowe akasimama akawaaambia, "Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza kumtupia jiwe." (Yohana 8:7). Akainama tena, akaandika nchini. Wakati huu nafikiri najua vile aliandika. Inawezekana kuwa aliyaandika majina ya wale waliosimama pale tayari kuhukumu, labda alianzia na yule mzee zaidi. Nafikiri alianza kuandika aina nyingi za dhambi ambazo yule mzee alikuwa ametenda, pengine rafiki wa kike ambaye alikuwa naye, na pengine Yesu akawaonyesha kwa undani mambo ambayo walifanya. Na hapo mwishowe yule mtu akasema, "Ndio sasa nakumbuka mke wangu aliniambia nifike nyumbani mapema leo. Rafiki, lazima niende." Baada yake kwenda Yesu aliandika tena jina la aliyefuata kwa umri na pia akaandika mambo machache aliyokuwa akifanya, naye pia akatoroka.

Mmoja baada ya mwingine waliondoka, wakaendelea kutoka kuanzia waliozeeka mpaka kwa vijana, mpaka mwishowe hakukuwa na mtu aliyeachwa. Ndipo Yesu akasimama, na akimtazama mwanamke, akamwambia, “Mwanamke, wako wapi wale washitaki wako? Hakuna yeyote amekuhukumu?” Akasema, “Hakuna yeyote, Bwana.” Ndipo Yesu akamwambia, “Na mimi pia sitakuhukumu, nenda na usitende dhambi tena.” (Yohana 8:10-11).

Tazama jawabu nzuri kwa Yesu “Hata mimi sitakuhukumu enda na usitende dhambi tena.”

Wakati kumetokea ajali mbaya na magari huwa yamebondeka-bondeka na miili ya watu imetapakaa, kuvunjwavunjwa, na damu inatoka na imelazwa barabarani. Kuna aina mbili za magari ya dharura yanafika katika sehemu ya ajali. Aina ya kwanza kufika na lile la polisi. Na kazi yao ni kuzingira ile sehemu kwa ukanda wa usalama na kuzuia magari. Ndipo wanatoa pedi na kutazama mahala sawa pa magari, wanapima alama za mtelezo na kuhoji mashahidi.

Kazi yao ni kujua ni nani aliyevunja sheria. Ni nani wa kulaumiwa kwa huu mkasa? Jukumu lao kuu ni kutambua ni nani amevunja sheria na kusababisha yaliyotendeka.

Aina ya pili ya gari huwa ni ya wahudumu wa matibabu. Hawa hawashughuliki na nani alikosea. Kuna watu ambao wameumia barabarani. Kazi yao ni kuwahudumia wale wanatokwa na damu, wawafunge bendeji. Watazame waone kama kuna mifupa imevunjika, na kuwaweka kwa machela na kisha kwenye ambulansi. Hawafikirii ni nani wa kulaumiwa au la. Hawako hapo kuzua lawama, wako hapo kuwasaidia wale walioumia.

Pia kuna aina mbili za wahuduma kanisani ambao nimeona. Wale wanaochukua mtazamo wa askari; wao hufika mahala pa msiba, maisha

yaliyovunjika na wanachukua kitabu cha sheria watakusomea sheria. “Una haki ya kunyamaza, lakini lolote unalosema laweza kutumiwa dhidi yako.” Wako katika mahali hii ili kutambua ni nani wa kulaumiwa, na kuwasomea sheria.

Na pia tuna wale wahudumu ambao ni kama wauguzi na hawasumbuki ni nani aliyevunja sheria ila wanawezaje kuponya? Vipi tunaweza kusaidia? Vipi tunaweza kuhudumia mifupa iliyovunjika na haya maisha yaliyovunjika? Vipi tunaweza kurejesha sehemu tofauti pamoja? Vipi tunaweza leta uponyaji?

Na sasa katika maelezo ya Yohana 8 ni Mafarisayo. Walikuwa wametoa kitabu cha sheria. “Sheria yetu inasema tumpige mawe. Wewe wasemaje?” Lakini Yesu alipendelea kumhudumia, kumsaidia, kurudishia maisha yake pasipo kuhukumu, “Nami sikuhukumu.” Lengo lake kuu lilikuwa ni kuyarudisha maisha yake katika hali bora ya zamani.

Tunatafuta kuwahudumia watu walioumizwa. Lengo letu kuu ni kuwarejesha katika hali yao ya awali ili wafanye kazi tena. Yohana anatuambia kuwa sheria ilitufikia na Musa, lakini neema na ukweli zilitujia kupitia Kristo. Kama nitakuwa mhudumu wa Yesu Kristo, lazima nihudumu tofauti. Tunawaona wengi ambao ni Wahudumu wa Musa. Niwakatili na wanafuata sheria. Sheria imevunjwa, na watakwambia vile sheria inasema. Na pia tunamwona Yesu akisema, “Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu awe wa kwanza kumtupia jiwe,... wala mimi sikuhukumu.”

Ni furaha yetu kutumika kuwarejesha wale walio hukumiwa na sheria. Ninaamini ya kuwa kabla ya kurejeshwa ni lazima kuwe na kutubu. Naamini ya kuwa sheria ilikuwa mwalimu wa kuleta watu kwa Kristo. Wale ambao hawajakuja na kutubu wanahitaji sheria kwa hivyo kunanafasi ya sheria. Ni takatifu, yenye haki na ni nzuri ikitumika kisheria. Ninafikiria wakati mwingine tunazidi na kutoa adhabu hata baada ya kutubu. Hatuko

tayari kwa urejesho. Yesu alisimama kwa neema na ukweli. Yatupasa kutafuta kuwarudisha, lakini tusisahau kuwa kutubu kunahitajika.

Ni jambo la ajabu kuona maisha ambayo yamepondwapondwa na yenye kuchibuka yakipata mazao katika Ufalme wa Mungu. Lakini neema pia ina hatari zake. Ninaweza kukosewa kwa kusamehe na kuwaonyesha watu neema. Yawezekana kuwa kutubu kwao sio halali. Yaweza kuwa bado wako na nia iliyofichika. Nimeonyesha neema kwa watu ambao bado waliendelea kutenda dhambi na ambao mwishowe walinidhuru. Mimi sio mkamilifu. Nimefanya kosa katika kuhukumu na nimeonyesha neema kwa wale bado hawakutubu maovu yao.

Nimepata nafasi kuwaleta watumishi ambao nilidhani wametubu na muda si muda tabia zile zile zilikuwemo. Nimekosea. Na nitakosea usoni. Lakini nitakwambia hili, kama nitakosea nataka kukosea upande wa neema badala ya upande wa kuhukumu.

Katika Ezekieli 34 Mungu alinena kinyume na wachungaji wa Israel. Waliachilia kondoo kupotea na hawakwenda kutafuta waliopotea. Mungu alikuwa na mambo magumu ya kusema kuhusu wachunganji ambao hawakuona umuhimu wa kutafuta na kuwarudisha waliopotea. Naamini kuwa Mungu atakuwa na huruma nami na makosa yangu kwa neema kuliko vile atakuwa kama ingekuwa ni kwa njia ile nyingine na ninamhukumu ambaye amesamehewa.

Kuna Maandiko matakatifu mengi ambayo yanatukanya kuhusu kuhukumu. “Msihukumu, msije mkahukumiwa nanyi.” (Mathayo 7:1). Sisi tunajiwekea kanuni zetu za hukumu, wakati tunapowahukumu wengine. “Wewe u nani unayemhukumu mtumishi wa mwingine? Kwa bwana wake mwenyewe yeye husimama au huanguka. Naam, atasimamishwa, kwa kuwa Bwana aweza kumsimamisha.” (Warumi 14:4). Singetaka kukosea katika upande wa kuhukumu. Kumhukumu mtu yeyote bila sababu ambaye ametubu. Nachukia kuwa katika nafasi ya kukosea katika kufanya

hukumu. Tena, nikikosea nataka kukosea nikiwa upande wa neema kwa sababu najua Mungu atanirehemu badala ya kama ningemhukumu kwa makosa, sitaki kupatwa na kosa hilo.

Ni rahisi kuanguka katika hali ya kisheria. Tunatakiwa kutahadharishwa juu ya jaribu hili. Angalia dhidi ya kuwa na msimamo mkali. Nimegundua kuwa, kwa wingi sana mtu akiingia kwa uzito katika Theologia ya Mageuzo, wanaingilia tena mambo ya kisheria. Wanahakikisha kuwa "T" zimefungwa na "I" imetoneshwa vizuri. Theologia ya Mageuzo iko na mambo mazuri, lakini pia yanayochoma kama nungu. Ukiishikilia kwa nguvu, utapata makali yake.

Watu wengine wanakataa sababu wanafikiria ninasitiri aina nyingine ya maandishi, na hao huwa sawa. Lakini kusitiri juu ya mambo yenye mvutano ni jambo la kujadiliwa kwa sababu linazo pande mbili. Na nimejua kuwa ni muhimu kutokuwa mgawanishi na kutowaruhusu wengine kukingamiza juu ya mambo fulani kwa sababu wakingamiza kutakuwa na mgawanyiko.

Mfano ulio bora ni shida iliyoko katika kuelewa Maandiko yanayohusu Ukuu wa Mungu na Jukumu la binadamu. Kwa kweli Bibilia yafunza yote mawili, lakini katika kuelewa kibinadamu haya ni tofauti. Watu ambao wanagawanisha katika jambo hili, hudai ya kwamba hatuwezi kuamini yote mawili, sababu ukichukua Ukuu wa Mungu kupita kiasi inafaa wajibu wa mwanadamu. Vile vile ukichukua wajibu wa binadamu kupitia kiasi itaondosha ukuu wa Mungu. Kosa hili hutendeka wakati mtu anauchukua kanuni na anaielekeza katika uelevu wa kibinadamu. Ukitumia hekima ya kibinadamu na kutoa Ukuu Mtakatifu wa Mungu nje ya hekima ya kibinadamu humwacha mtu bila chaguo lolote.

Kwa hivyo ni vipi tutaweza kulishughulikia kwa ufasaha Neno la Ukuu wa Mungu na Jukumu la mwanadamu? Twatakiwa kuamini yote mawili kwa imani, kwa sababu siwezi kuyaweka sawa kwa kuelewa

kwangu sielewi vile yanakuja pamoja. Lakini nayaamini yote mawili. Naamini ya kuwa Mungu ni Mkuu na pia naamini kuwa ni jukumu langu, na Mungu anachukua wajibu kwa ule uamuzi ninafanya. Naamini Mungu kwa rahisi kuwa maneno yote yanathibitisha kuwa Maandiko ni kweli.

Kuna mchungaji ambaye alikuja na kitabu kidogo juu ya mafundisho ya Calvinism (ambao wanaamini kuwa Mungu amekwishatenga wale wataokolewa na hatunalakufanya kwa sababu Mungu ameshawateuwa wale watamkubali), na juu ya kifuniko au ukurasa wa gozi, namna chombo cha kupimia (ratili) na John Calvin (mwanzilishi wa Calvinism) alikuwa upande mmoja na Yohana 3:16 upande mwingine. Wewe ungesimama upande upi?

Usikangamizwe na usiruhusu watu kukangamiza wafuasi wako kwa sababu watu hugawanyika sawa sawa katika jambo hili. Kwa hivyo ukichukua nafasi ya katikati hutapoteza nusu ya wafuasi wako. Kwa kweli, ungetaka kupoteza 50% ya wafuasi wako?

Unajua kitu cha maajabu kuhusu kuitwa Calvary Chapel? Watu hawajui unasimama wapi. Weka Ubatisa kama jina, na watu wanajua msimamo wako na nusu ya watu hawatakuja kwa sababu ni kanisa la Kibatisti. Ukiweka jina Kipresbeteri, watu watajua msimamo wako, na nusu yao hawatakuja kwa kuwa wanatambua unachoamini. Weka jina la Nazarini, na papo hapo watakuweka kwa shimo la njiwa, wanajua wewe ni nani na hawahitaji kwenda.

Lakini Calvary Chapel ina jambo la maajabu juu yake. “Watu hawa wanaamini nini? Mimi sijui lakini wacha twende tuone”. Na uwanja wote ni wetu. Unataka kutega samaki katika dimbwi kubwa kama unavyoweza kupata. Wakati unauza kitu unatafuta lile soko kubwa la kupendeza kabisa. Hatuligawi soko vipande na kusema, “Kweli, tunaenda kutega samaki kwa hili soko ndogo.” Wacha soko liwe kubwa. Tega mahali samaki wanauma.

# 6

# AULA YA NENO

*“Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha.” (1 Timotheo 4:13)*

Msingi mwingine tofauti wa Calvary Chapel ndio jitihada zetu za kutangaza/kufunza ushauri wote wa Mungu. Tunaona kanuni hii ikidhihirika wakati Paulo alikutana na wazee wa Waefeso katika Mitume 20. Walipokuwa katika ufuko wa Aegeliana mle Mileto karibu na pwani la Waefeso, Paulo alisema kuwa hana hatia kwa damu ya mtu awaye yote, “Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.” (Mitume 20:27).

Sasa, kuna uwezekano gani wa mtu kusema kuwa ametangaza, “Kusudi lote la Mungu?” Njia pekee ya mtu kudai hivyo kwa wafuasi wake ni kama amewafunza Neno la Mungu kamili, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Ukishawafunza wafuasi wako Bibilia yote, sasa waweza kuwaambia, “Sikujiepusha na kuwahubiria habari yote ya kusudi lote la Mungu.”

Hii haiwezi kufanywa kwa mahubiri za mada. Mahubiri za mada ni nzuri, na sina nafasi yake, lakini wakati unahubiri kwa mada kuna mvuto wa kibinadamu wa kuhubiri zile mada unazopendelea. Na kunazo mada katika Bibilia ambazo hazivutii sana, hazisisimui watu lakini ni mambo muhimu ambayo yanafaa kushughulikiwa. Mwelekeo wa kibinadamu kwa kweli ni kuyaepuka hayo. Kama unahubiri kwa mada, kuna uwezekano wa kuepa mada ambazo ni ngumu, na watu hawatapata mtazamo uliosawazika kwa ukweli wa Mungu. Kwa hivyo umuhimu wa kupitia kote katika Bibilia, hivi sasa unaweza sema, “Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.”

Sasa, naamini naweza waambia watu wa Calvary Chapel Costa Mesa, “Nimewahubiria habari ya kusudi lote la Mungu,” kwa sababu tumewapeleka kutoka Mwanzo hadi Ufunuo mara saba. Sasa twajitayarisha kwa mara ya nane. Hatuepuki sehemu yoyote. Na hii ndiyo maana wengi wa Calvary Chapel, na wale walionawiri kabisa, utapata wanafuatilia sawasawa mkufunzi wa Neno la Mungu na wanasoma Bibilia, kupitia ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho.

Kwa mara nyingi mafundisho ya Calvary Chapel ni ya mada wa ufafanuzi. Hii haimaanishi kuwa kwa wakati mmoja hatushughulikii swala fulani au kuwa mahubiri ya mada. Hatusemi kuwa mahubiri ya mada ni mabaya au ni ya kishetani. Yako na nafasi yake. Kuanguka katika ushurutisho wa kisheria ambapo tunatazama kila mahubiri kuona kama yalikuwa na ustadi wa kuhubiri na kama yalitandazwa vizuri. Lakini, kwa wingi mno, tunafuata mfano wa Isaya ambaye alisema, “Kwasababu hiyo neno la BWANA kwao litakuwa hivi, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni huku kidogo na huku kidogo;” (Isaya 28:13) Hii mistari inadhihirisha jibu la watu juu ya mtindo wa Isaya wa kufunza.

Walileta mzaha juu ya huu mtindo, lakini ndio ulikuwa bora zaidi. Walikuwa wakiteta juu yake, kwa madharau wakisema kuwa ilifaa aende akawafunze watoto kwa sababu mafunzo yake yalikuwa ni “amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, na huku kidogo na huku kidogo.” Walisema haya maneno kwa kudhihaki. Lakini, ni ya umuhimu sana kuwafunza watu Neno la Mungu kwa mstari na kanuni kwa kanuni. Tukifanya hivyo tunawaletea kusudi lote la Mungu.

Faida nyingine ya kufunza kusudi lote la Mungu ni kuwa unapofikia maswala magumu ya kushughulikia ambayo yanahusu maisha ya kibinafsi au katikati ya mwili wa kanisa, unaweza yaelezea waziwazi. Hatupaswi kushangaa juu ya watu kufikiria, “Loh! Leo ananilenga mimi.” Watu waliomo wanajua kuwa ni kipengele cha maandishi yanayosomwa leo. Kwa hivyo, haiwezi kuwa, “Loo, sasa ni mimi amenilenga,” kwa sababu

wanangudua ya kwamba unafunza kitabu chote, na ya kwamba hauruki kutoka mada hii hadi nyingine. Tunaenda moja kwa moja katika somo la Neno la Mungu.

Katika kitabu cha Nehemia nane mstari wa nane, wakati Wana wa Isiraeli waliporudi kutoka mateka na wakarejea kuujenga mji, viongozi waliwakusanya watu pamoja na wakajenga jukwaa ndogo. Wakaanza asubuhi na mapema kulisoma Neno la Bwana kwa watu. Nehemia 8:8 yatangaza, “Nao wakasoma katika kitabu, katika torati ya Mungu, kwa sauti ya kusikika; wakaeleza maana yake, hata wakayafahamu yaliyosomwa.”

Naamini huu ni mfano mzuri wa mahubiri ya ufafanuzi wa kusoma Neno, eleza na uwafanye watu kuyafahamu maana yake. Nimeona kuwa wakati mwingi sipati kuelewa na kipengele fulani bila kukisoma mara hamsini au sitini. Papo hapo inaanza kukusanyika katika fikira zangu. Naamini ni ya muhimu kutumia tafsiri mbalimbali kukusaidia kuelewa na maana ya kipengele fulani. Nafurahia uchambuzi ambao Mungu amewapea watu wengine katika vipengele vya Neno. Lakini kusema kuwa napendelea na nasoma tafsiri, lazima pia mara nyingi ninasoma ukurasa na mwingine wa hizi tafsiri na sipati lolote la kutumia. Wakati mwingine unaposoma tafsiri saba juu ya kipengele fulani, ukimalizia umechanganyikiwa kuliko ulivyoanza. Sababu kuna mawazo mbali mbali au fikira juu ya kipengele fulani. Kwa hivyo naamini mojawapo wa tafsiri iliyo bora zaidi ni Bibilia yenyewe.

Ni vizuri kukumbuka kuwa mara nyingi hatupati matokeo mara moja au usiku kucha katika Calvary Chapel. Inachukua muda kuzidisha na kukuza hamu ya Neno la Mungu kwa watu. Inachukua muda kukua. Katika Calvary Chapel ambayo yamepandwa katika sehemu mpya inachukua miaka kadhaa kuweka msingi, kutayarisha ardhi, kulima mchanga ulio mgumu na kupanda mbegu katika udongo wenye rotuba. Halafu ni lazima

ungojee. Mbegu haileti mazao kwa usiku moja. Mbegu lazima imee na ikue, lakini mwishowe, itaanza kuzaa matunda.

Watu wengi ambao nimeona wamejitokeza na wakifikiria mwaka wa pili unapokaribia kuisha, wanagonga mwamba wa shida. Na wanakata tamaa. Ni wazi kuwa haitatendeka mahala walipo. Wanaanza kuamini kuwa watu hapo ni tofauti na wale wengine na kuwa haiwezi ikatendeka. Utashangaa ni wangapi wanaenda nje, na baada ya miaka miwili wanarudi wakisema waliondoka sababu hakuna linalotendeka. Nawapa moyo kungojea miezi sita au wakati kama huo. Huku nikiwaambia, “Tazama, umemaliza sehemu iliyokuwa ngumu. Umemaliza kulima. Pia umemaliza kupalilia mchanga. Umemaliza kupanda. Sasa ngojea na utazame na uone kama matunda yatatokea.” Kwa desturi ya kawaida, ni katika mwaka wa tatu ambao unaaza kuona matunda yanayotokana na upandaji wa neno la Mungu katika Roho za watu. “Nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikazaa, moja mia, moja sitini na moja thelathini.” (Mathayo 13:8). Lakini hii haitendeki kwa usiku moja.

Hili linakuwa la kuvunja moyo mahali kuna wale wanakuja kwa moto na mmuliko, na wanaonekana kuvutia umati kwa wingi. Watu wana hamu kuu ya kuona miujiza, kuomba mito wa huduma, na wewe bado huko hapo wajikokota. Huwezi kuona maendeleo mengi au kukua, na hawa wengine wana mlipuko wa kunawiri. Lakini kama vile Mungu alivyomwambia Danieli, “Na walio na hekima watang’aa kama mwanga wa anga; na hao waongozao wengi kutenda haki watang’aa kama nyota milele na milele.” (Danieli 12:3).

Tarehe nne Julai ni furaha kutazama moto wa kusisimuka wa baruti za anga, mmeko wa utukufu, na kila aina ya rangi iliyojaa angani tokana na miale za moto. Kila mtu alilia “masalale” na “salale” lakini hii ni ya muda mfupi. Kufumba na kufumbua, ni jivu tu. Ni mwanga mkubwa halafu unaisha. Hivi ndivyo huduma nyingi zilizo na mwangaza mkubwa halafu zinaisha na kudidimia. Lazima uamue ni aina gani unataka kuigiza.

Unataka kung'aa kama nyota milele na milele? Ama ungetaka kuwa kama baruti za anga ya mwanga wa ghafla, kuingia kwa uwanja kwa njia ya kuvutia, lakini bila nguvu za kudumu?

# 7

# NAFASI KUU YA KRISTO

*“Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu na kuwa ni Bwana...”* (2 Wakorintho 4:5)

Mmojawapo wa sifa bainifu za Calvary Chapel ni ule Ukuu wa Yesu Kristo katika ibada yetu. Haturuhusu desturi au tabia ambazo zitawafanya watu kutokuwa waangalifu kwa Yesu au kutoa mawazo kwa Yesu na kuelekeza kwao. Kwa mfano haturuhusu watu kusimama peke yao wakati tunaimba kanisani. Wakati mtu anasimama, wale walio karibu wanamtambua na wanastaajabu, “Kwa nini anasimama?” Mtazamo unatolewa kwake Kristo na unaelekekezwa kwa yule amesimama.

Jicho linasisimua sana kwa sababu linavutiwa na mwendo. Kwa wakati mwingi, nimewaona wale wanaosimama pekee yao katika ibada wakiamua kuwa hawapati utukufu/sifa na ndipo wanainua mikono yao na kuiyumbisha. Hilo linavutia jicho. Lakini pia huwavunja mawazo na watu wanaanza kustaajabu ni kwa nini wanasimama pale. Wanafikiri nini? Je wanajua wanajiletea sifa? Nini kinaendelea? Naamini ni muhimu mambo haya kushughulikia kwa sababu mambo kama haya hufanya kupoteza wafuasi wa kanisa. Kama ningeenda kanisani na hayo yafanyika, ningefikiria kuwa ujumbe ulikuwa wa haraka, lakini sikuweza kuvumilia haya mambo mengine kwa urahisi.

Nilikuwa katika Calvary Chapel nyingine mbeleni na waliruhusu mtu kusimama mmoja mmoja. Kwa bahati mbaya, vile mtu mmoja anafanya wengine pia wataiga. Kulikuwa na jamaa mmoja kila usiku ambaye alikuwa chini katika safu ya kwanza na yeye alikuwa anacheza ngoma pale. Ilikuwa ni wazi kuwa yule mtu hakuwa na akili timamu vile na bila

tashwishi alikuwa na shida ya kisaikolojia. Alipata mazingara ambayo angefanya sarakasi zake na akubalike, lakini hii inasumbua sana. Nilinena na mchungaji kuhusu jambo hilo na yeye alitetea kile kitendo, ndipo nikafikiria, “Yote ni sawa, mumejiamulia kubaki hivyo.”

Katika Calvary Chapel Costa Mesa, mtu akisimama, mashemanzi humkaribia na kumkaribisha mle sebuleni, halafu mchungaji mmoja anaongea naye kwa upole na upendo. Wao husema, “Hatutaki kitendo kama hiki kwa sababu tumegundua ya kwamba inavutia hisia za watu wakati wa ibada. Na kwa kweli hungetaka kutoa hisia za mtu kutoka kwa Kristo hadi kwako, ungetaka hivyo kweli?”

Tunawaeleza kuwa wanavuta utukufu/sifa kwao, na watu wanapoteza mtazamo mkuu ambao ni Kristo. Tunanena na wao kwa upendo na kupendekeza wasifanye hivyo na kama wakikasirika inaonyesha kuwa walikuwa wakifanya kimwilini wakati wote. Kama walikuwa ndani ya Roho na kutembea kwa Roho, wataichukua ndani katika Roho. Watasema, “Aha, sikugundua hilo. Niwiie radhi.” Lakini ukiona wote wamekuchukizwa kwa upesi basi utajua walikuwa wakifanya katika mwili.

Yesu alisema, “Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni.” (Mathayo 6:1). Halafu aliudhihirisha vile watu walitaka wapate utukufu/sifa katika matendo yao ya wema kama wanaabudu. Kubali ama ulikatae, kama umesimama na kuyumba yumba wakati wale wengine wamekaa, litavutia watu kukutazama.

Nilikuwa katika Calvary Chapel nyingine ambayo walikuwa na wadada walivalia nguo zenye ufundo zilizotambalisha dansi wakati wa pambio za kuabudu hapo mbele. Sasa, kama kuna jambo ambalo linavunja mawazo kwangu, ni hili. Walikuwa wazuri, lakini nikagundua kuwa sikupata mengi kutoka kwa pambio za ibada usiku ule. Niliwatazama

hawa wasichana pamoja na mienendo yao, huku nikijaribu kuelewa na tafsiri zao za nyimbo. Na tena, nikaongea na mchungaji mwishowe, na akapata kuelewa na tangu siku ile, alisimamisha aina hii ya sani ya tafsiri, baada ya kugundua kuwa ilikuwa inavunja mawazo.

Tulikuwa na kanisa tuliloshirikiana kule Basil, Uswizi na ndilo lilikuwa kanisa la kufurahisha sana Uropa. Tukitazamia uwezo na vile mambo yalikuwa yakitendeka nafikiria ndilo lilikuwa kanisa kubwa sana la Kiprotestianti Uropa wakati ule. Kila mwaka ningeenda Basil na kunena katika ushirika. Lilikuwa jambo la kufana sana. Walikuwa wamepata maono yote ya Calvary Chapel. Walikuwa na pambio na kundi kubwa la kuabudu, na mafundisho ya Neno. Walikuwa na ma mia ya vijana ambao walihudhuria ibada ya Jumapili usiku kwa kanisa hili lenye desturi za Kijerumani. Kanisa la serikali liliwaruhusu kutumia mahala pao. Kanisa la serikali lilikuwa likitumia siku ya Jumapili asubuhi peke yake. Kwa sababu ni wazee sita tu walihudhuria, kasisi alisema kuwa Calvary Chapel yetu ingekuwa ikitumia Jumapili usiku. Ilikuwa inajazana mpaka juu na ilikuwa na kazi nzuri ya kuwafikia wengi. Walioenda kuwafikiria wengine walikuwa na kibarua kigumu. Walikuwa wamefungua duka la kunywa kahawa. Walikuwa na ratiba nzuri iliyokuwa inaendelea. Walikuwa wanashughulikia watoto waasi na waliokuwa katika madawa ya kulevya. Kanisa lilikuwa limepandwa au limejengwa mahala mlipokuwa mna wingi wa madawa ya kulevya na watoto waliokoka walihitaji mahali pa kuishi, kwa hivyo kanisa liliwapatia. Kanisa pia lilikuwa limejenga kiwanda cha kuunda aina mbalimbali za hedaya gunia hilo lilikuwa ni kujaribu jambo lenye mafanikio. Watoto walijaliwa, na wale wenye vipawa vya sanaa walizitumia kwa kuchora. Lilikuwa linakua kwa kasi.

Wakati wa mwisho nilikuwa pale walikuwa wameingilia dansi yenye tafsiri wakiwemo na wasichana wenye mavazi ya dansi. Walikuwa wamlete mchungaji msaidizi mwenye asili ya Kipentakosti, na walikuwa wameingilia biashara ya kusimama wakati wa kuabudu. Mchungaji

hakuwa amekomaa kabisa wa kushughulikia hili. Nikanena naye baada ya ibada na nikasema, “Haya mambo lazima yaishe. Yatakuaribu.” Kwa ukweli, hata hakuwa akiongoza mkutano. Niligundua kuwa wakati wangu ulipofika kukaribishwa, hawa wasichana walienda kule wakanong’ona kwa sikio lake, halafu wakaimba pambio moja halafu na dansi moja. Wenye dansi ndio walikuwa wakiongoza mkutano, sio mchungaji. Ndipo nikamwongelesha kuhusu hili lakini alikuwa hapendelei kuliingilia swala lile. Kwa hili, hatuna kanisa Basil leo. Waliachana nayo, na Wapentakosti wakaendeleza, na kanisa likawafukuza na sasa hamna kazi inaendelea mle.

Kwa hivyo ni muhimu tumweke Yesu kama mtazamo mkuu wa kanisa na tuwe na uchache wa mambo ya kuvuta watu kwetu. Wakati mambo ya kuvuta watu kwetu yanatokea, yashughulikiwe na ikiwezekana yazungumziwe hadharani.

Wakati nilikuwa katika Chuo cha Bibilia, mlikuwemo na jamaa mmoja ambaye angekaa katika mstari wa kwanza. Sana sana katika zile nafasi bora zaidi za ibada, wakati Roho wa Mungu anawahudumia watu mioyoni, yeye angeinama chini halafu angesimama juu mikono imeinuliwa. Angepiga yowe, “Haleluya!” Kila mtu angecheka. Lakini fikra za kila mmoja zilikuwa kwa huyu aliyekuwa akilia, “Halleluya!” Umuhimu wa somo unapotezwa. Aliharibu mahubiri mengi kwa vitendo vyake. Ndipo nikaamua nitakomesha hili! Nikakaa nyuma yake, na alipoinama kuingia kwa “Halelluya” nikamshika mabega na nikaanza kumfinya nafsi na nikamshikilia kwa magoti yake. Hakuna mtu mwingine aliyekuwa na ujasiri wa kumsimamisha. Walimwachilia tu aendelee na lilikuwa jambo la kusumbua sana!

Miaka michache iliyopita nilikuwa Colarado Springs kwa mfungo, na kulikuwa na mtu hapo mbele ambaye alikuwa ni pungwani. Kwa kumtazama tu ungeelewa na haya. Wakati tulipokuwa tunaimba pambio za sifa, yule mtu alikuwa anacheza na kukimbia mbele ya madhabau.

Nikamuuliza mchungaji, "Kwa nini unaruhusu haya?" Akasema, "Naam, walitaka uhuru…" Nikajibu, "Tazama huu sio uhuru. Kama kulikuwa na mgeni ametembea kanisani mwenu kwa mara ya kwanza, na amwone huyu jamaa chini, hangerudi tena, na angefikiri ushirika wenu una wenda wazimu."

Tunafika mahala ambapo tunakubali mambo ambayo ni mabaya kwa sababu hatuna ujasiri wa kuyasimamisha. Tunaogopa kulaumiwa kwa kuzima moto wa Roho. Nitazima aina hiyo ya roho! Na sio Roho Mtakatifu bali huyu roho ambaye analeta utukufu/sifa kwa binadamu kusumbua watu kwa kumwabudu Bwana.

Zamani (na hili halijafanyika katika Calvary kwa muda mrefu) tulikuwa na watu walioamka wakati wa ibada na kujaribu kusema kwa dimi. Tena mashemanzi waliingilia kati. Waliwakaribisha katika chumba cha wageni, na wachungaji waliwaelezea kuwa Calvary haturuhusu kusema dimi hadharani au kutoa unabii hadharani kama vile makanisa ya ki roho au ya Kipentakosti. Kutoka kwa jukwa/mimbara nikaeleza kuwa karama ya dimi inaruhusiwa katika Agano Jipya, na kuwa kuna nafasi nzuri ya ndimi. Nikaelezea vile Paulo alivyo weka wazi, katika fungu lake mwenyewe, ni afadhali kunena maneno matano yanayoeleweka baadala/kuliko ya maneno elfu kumi yasiyoeleweka wakati ako kanisani. Walakini, alikuwa akishukuru kuwa alinena na dimi kuliko wote. Katika wakati wako maalumu ni jambo la kujenga sana. Ni njia ambayo unaweza kumsifu Mungu na kumwabudu. Lakini kwa kanisa linalotoshana na Calvary Chapel, na watu wengine hawawezi kusikilikia tafsiri, sio jambo la kujenga katika ibada zetu za hadhara kutumia karama hii ya Roho, hata mkiwemo na tafsiri. Si ya kujenga au kufaa, kwa hivyo hatulifanyi. Hatuliruhusu katika ibada zetu za hadhara, lakini tunahimiza mtu kutumia karama hii katika nafasi yake ya maombi.

Kama kuna kundi la waumini na mkutane kwa maombi kumwomba Mungu, basi utumizi wa kipawa hiki utaruhusiwa pamoja na utafsiri. Lakini

ninaamini mkiwemo na wasioamini inaleta kuchanganyikiwa na maswala mengi. Kwa hivyo, ni vizuri kuifungia kwa waaminio ambao wamekusanyika pamoja kumngojea Mungu, kama vile tunavyofanya katika mkutano wa kipekee wa jioni. Inajenga na pia inaruhusiwa pale. Watu wanamtafuta Mungu na kujazwa na Roho wake, kwa hivyo katika mazingira haya linaruhusiwa.

Paulo alisema katika I Wakorintho 1:29, “Mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele ya Mungu.” Ninashangaa kama tunagundua jinsi ilivyo hatia kujaribu kuleta utukufu/sifa kwetu badala yake Bwana? Kweli, tunataka kuondoa utukufu/sifa wa watu kutoka kwa Kristo na kuuleta kwetu sisi? Nafikiri hii ni hatia zaidi. Na kwa kweli singependa kupatwa na kisa hiki.

Katika Agano la Kale tunapata mfano jinsi jambo hili lilivyo na hatia. Wakati waisrael walipomaliza kulijenga hema la Bwana na kuweka samani, walikusanya watu pamoja na kuweka wakhfu na pia wakatoa kafara. Kusanyiko lote la Waisraeli lilikuwa na kila mtu alikuwa mahala pake. Haruni alikuwa na joho la kipadri na vile vile vijana wake na wale wengine wote kulingana mpango wa Mungu, wote walikuwa kwa mpango. Halafu, kwa haraka, wakati watu walikuwa pale wakingojea kuanzisha, moto wa Mungu ukaja ukashika madhabau. Ulikuwa ni mwaka wa hiari. Watu wote waliona dalili ya uwepo wa Mungu na wakaangusha binja na kupaza sauti kuu. Kulikuwa na furaha nyingi mno kila mahali, na msisimuko wa nafsi kwa kujua kuwa Mungu alikuwa katikati ya watu wake. Nao wana wawili wa Haruni, Nadabu na Abihu wakatwaa kila mtu, chetezo chake wakatia moto ndani yake wakatia na uvumba. Wakaanza kuingia ndani iliwapate kutoa chetezo chake mbele za Bwana ndani ya pahala patakatifu. Na Biblia inasema kuwa moto ukatoka hapo mbele za Bwana na ukawaka nao wakafa mbele za Bwana. (Mambo Ya Walawi 10).

Ninaamini kuwa walipawa katika msisimuko na furaha ya wakati ule. Walikuwa wanaenda kudhihirisha kwa watu nafasi yao kama padri na jinsi walivyo "wa maana." Kwa sababu ya hili, wakafa.

Ninatazama kwa kusudi moto usio wa kawaida. Watakiwa uwe mwangalifu kuhusu moto usio wa kawaida pia wewe-msisimko ambazo hazitokani na Mungu pekee, na huduma ambayo haitokani kwa Mungu. Ni shughuli ya kuleta utukufu/sifa kwa chombo badala ya mwenye chombo.

Tunaona haya katika Kanisa la Mwanzo juu ya Anania na Safira. Hapa tena ni jaribio la kuleta sifa na utukufu/sifa kwa binafsi. Anania na Safira waliuza thamani yao na wakaleta fedha kwa kanisa, walijifanya wametoa kila kitu. Naamini hili lilikuwa la kujisifia na kustaajabisha watu, ambao wangesema, "Waoneni wale! Wametoa kila kitu kwa Mungu!" wakati ukweli ni kuwa wameshikilia zingine.

Sote tunapendelea utukufu/sifa kama huo. Tunapenda watu wanafikiria sisi ni wa ki roho. Jitahadhari! Mwili wetu umeoza. Nataka kujulikana kama mtu aliyekomaa ki roho. Mwili wangu unafurahisha watu wafikirie kuwa mimi ni wa ki roho wala sio nilivyo. Wakati mwingine tunajaribu kuleta hisia ya namna hii, na ninafikiria hii ni aina moja ya laana za kanisa. Wachungaji wengine wanatafuta mfano wa kukomaa ki roho ambao sio wa kawaida.

Hili linaanza kuguzia Matendo yao. Wanaanza kupata sauti ambayo inasikika kuwa takatifu, wanashikana mikono yao kwa njia spesheli, na wanasema, "Ee, dada mpendwa, niambie yote kulihusu." Tabia zao zote zinabadilika na tabia zao za dhihirisha kuwa ni mtu Mtakatifu. Na wanapendelea hilo. Wanapenda watu wafikirie kuwa wao ni majitu ya ki roho. Wanapenda watu wapende Neno jinsi wanavyoipenda, au wafikirie kuwa wanatumia wakati mwingi sana katika maombi. Wanatabasamu na kusema, "Inachukua kujitolea nafsi, unajua."

Kwa kweli tunatakiwa kuwa waangalifu juu ya kuunda manzili inayoashiria wema na kupenda sifa zitokanazo na watu. Katika mfano wa Anania na Safira, waliadhibiwa kwa sababu walivuta uangalifu na utukufu/sifa kwao wenyewe, utukufu/sifa ambao ungemwendea Bwana. Na walilipa kwa ghalama kali. Mungu hagawanyi utukufu/sifa wake. Kuwa mwangalifu! Usiruhusu mambo ambayo yanaweza badalisha mtazamo. Tunataka kumweka Yesu kama mtazamo mkuu wa watu. Ni muhimu sana kumweka Yesu kama mtazamo mkuu katika ibada zetu.

# 8

# KUNYAKULIWA KWA KANISA

*“Tukitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu Mkuu na Mwokozi wetu.”* (Tito 2:13)

Kunyakuliwa kunaeleza wakati ambao Yesu atakuja, bila tahadhari, na kuchukua kanisa lake kutoka humu duniani. Baada ya kunyakuliwa, Bwana atamwaga ghadhabu yake duniani hii yenye dhambi. Kuna wachungaji wengine ambao hawana hakika kuhusu kunyakuliwa au wanasema hawana hakika kunyakuliwa kutafuatiliwa na mateso. Wao husema hawana hakika ya msimamo wao kuhusu jambo hili. Siamini kuna sababu yoyote ya kutokuwa na msimamo juu ya jambo hili. Tuna Bibilia na tuna uwezo wa kujifunza juu ya jambo hili barabara. Naamini kuwa maoni yako kuhusu kunyakuliwa kutakuwa na athari fulani kwa kufaulu kwa huduma yako.

Kwanza sote twajua kuwa Yesu aliandika atarudi tena. Katika Yohana 14 twasoma, “Msifadhaike mioyoni mwenu, mnamwamini Mungu, niamini na mimi. Nyumbani mwa baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.” (Yohana 14:1-3). Bwana aliahidi atakuja tena na kupokea wanafunzi wake ili pale alipo tuwe pia.

Paulo akiandikia Wakorintho alitangaza, “Angalieni, nawaambia ninyi siri.” (1 Wakorintho 15:51). Fumbo katika Agano Jipya linamaanisha kitu ambacho bado hakijafunuliwa na Mungu katika kuendeleza Ufunuo wake, lengo na mipango yake kwa binadamu.

Kwa mfano, Paulo alinena kwa Wakolosai juu yake ni, “Jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa fumbo hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.” (Wakolosai 1:27). Manabii wa Agano la Kale hawakuelewa maana ya Yesu ndani mwetu. Hata malaika walitamani kuelewa kwa ukamilifu mambo haya (1 Petero 1:12). Katika kifungu cha 1 Wakorintho 15:51 tunaonyeshwa, “Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho italia.”

Bibilia inapoarifu ya kuwa “sote tutabadilishwa” ina maanisha kuwa kutakuwa na badiliko la kimsingi. “Maana sharti huu uharibikao uvae usioharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa.” (1 Wakorintho 15:53). Waamini wote watapitia ubadiliko wa utukufu Yesu atakapokujia kanisa lake.

Jambo hili liliwasumbua Wathesalonike. Paulo alihudumu huko kwa muda mfupi tu wa wiki chache, lakini akawafunza mengi. Kati ya hayo mengi, aliwafunza juu ya Kunyakuliwa kwa kanisa. Wathesalonika walitazamia Ufalme ujao.

Naamini kuwa ni lengo la Mungu kuwa kila umri wa kanisa, ushawishike kuwa ni wa kizazi cha mwisho. Naamini pia kuwa ni mpango Mtakatifu wa Mungu kwa kanisa kuishi likitarajia kila wakati kurudi kwa Bwana. Yesu akiongea juu ya kurudi kwake, alisema, “Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo.” (Mathayo 24:46).

Kanisa la mwanzoni liliamini Yesu ataanzisha ufalme papo hapo. Katika sura ya kwanza ya Matendo, Wanafunzi wake walimwuliza, “Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?” (Matendo 1:6). “Je! Tuko tu siku chache kabla ya hilo?” Walikuwa wanasisimuka kwa matarajio kuwa Bwana atasimamisha Ufalme wakati wowote.

Yesu aliwajibu kwa kusema, “Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwachilia juu yenu Roho Mtakatifu.” (Matendo 1:7-8).

Kulikuwa na uvumi katika kanisa la mwanzo ya kwamba, Bwana atarudi kabla ya Yohana hajakufa. Kila wakati Yohana alipopatwa na homa au maumivu ya koo, kanisa lote lilisisimuka. Kwa hivyo Yohana akaandika Injili ili afafanue vile Yesu alisema. Yesu alipokuwa akimweleza Petero jinsi atakavyokufa, halafu Petero kama kawaida yake, akasema, “Lakini Bwana, naye je?” Yesu akajibu, “Ikiwa nataka huyu akae hata nijapo, imekupasaje wewe? Wewe unifuate mimi.” (Yohana 21:22) Yohana aliweza kufahamu kuwa Yesu hakusema atakuja, bali alisema “Iwapo nitakuja.” Kwa hivyo Yohana alikusudia kuweka bayana sintofahamu huu kuwa Yesu angerejea kabla ya kifo chake Yohana.

Wathesalonika walikuwa wakitumaini Yesu arudi, lakini wapendwa wengine wao waliaga dunia na Yesu bado hakuwa amerejea. Waliamini kuwa kwa sababu wanafariki kabla ya kurudi kwa Yesu, hawataweza kushirika katika ufalme wa utukufu. Katika I Wathesalonike mlango 4, Paulo alirekebisha dhana hii potovu kuwa kama mtu atakufa kabla ya Yesu kurudi atakosa ufalme wa Mungu. Kwa hivyo akasema, “Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.” (1 Wathesalonike 4:13). Paulo akaendelea na kusema, “Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo nao hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa Neno la Mungu, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti.” (1 Wathesalonike 4:14-15). Paulo aliamini kuwa labda atakuwa hai na atamwona Bwana atakaporudi. Alisisitiza kuwa hatutawatangulia waliolala. “Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika

Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, na tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki na Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo.” (1 Wathesalonike 4:16-18).

Kuna watu wanaosema, “Siamini Kunyakuliwa kwa kanisa,” kwa sababu wamechunguza Bibilia yote na hawakupata neno ‘Kunyakuliwa.’ Lakini katika I Wathesalonike 4:17 tunasoma ya kuwa, “Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.”

Neno ni Kigriki lililotafsiriwa ‘kunyakuliwa’, ‘kuchukuliwa’ ni ‘harpozo’ linalomaanisha ‘kutekwa kwa nguvu’. Ni neno linalohusiana na mambo ya kijeshi linalokaribia na kuchukuliwa mateka. Katika Kilatini neno ‘harpozo’ lilitafsiriwa kama ‘raptuse’ ndipo neno ‘harpozo’ la kingereza likapatikana. Yesu atarudi kunyakua kanisa lake. Hilo litakuwa tokeo la kwanza.

Tokeo la pili ni wakati Yesu Kristo atakaporudi tena, wakati atarudi na kanisa lake kuanzisha ufalme wake duniani. Kunyakuliwa basi ni tofauti na Kurudi kwa mara ya Pili kwa Yesu Kristo. Tunaambiwa, “Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia.” (Ufunuo 1:7). Pia, “Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu.” (Wakolosai 3:4). Kurudi mara ya Pili kwa Yesu kutakuwa kwa kuanzisha ufalme wake ulimwenguni. Alikiri kabla ya Kurudi kwa mara ya Pili tukio litatanguliza ni kanisa kunyakuliwa likawe pamoja na Bwana. Jambo ambalo napenda zaidi ni kwamba, “na hivyo pamoja na Bwana milele.” (1 Wathesalonike 4:17).

Kuna tofauti kubwa kati ya Yesu kujia kanisa lake na Yesu kuja na kanisa lake. Atakuja kwa sababu ya kanisa lake siku ya Kunyakuliwa. Lakini kuja kwa Yesu Awamu ya Pili, atakuwa anakuja na kanisa lake.

“Wakati Yesu, ambaye ni uhai wetu, ataonekana,” (kuja kwake Awamu ya Pili) “basi pia sisi tutaonekana naye katika ufalme wake.” (Wakolosai 3:4).

Yuda 14 anaongoa kuhusu Kurudi tena Awamu ya Pili inaposema, “Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu.” Zakaria pia alirejelea hilo alipoandika, “Na siku hiyo, miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, upande wa mashariki na upande wa magharibi; litakuwako huko bonde kubwa sana; na nusu ya mlima ataondoka kwenda upande wa kaskazini, na nusu itaondoka kwenda upande wa kusini. Nanyi mtakimbia kwa njia ya bonde la milima yangu; kwa maana bonde lile la milima litaenea hata Aseli; naam mtakimbia, kama vile mlivyokimbia mbele ya tetemeko la nchi, siku za Uzia, mfalme wa Yuda; na Bwana, Mungu wangu atakuja, na watakatifu wote pamoja naye.” (Zekaria 14:4-5)

Unyakuzi unaweza kufanyika wakati wowote. Hakuna unabii ambao haujakamilika kabla ya Unyakuzi. Unaweza kutokea kabla hujamaliza kusoma sura hii, na tungefurahi kweli kweli kama lingetokea.

Kunazo tabiri ambazo bado hazijakamilika kabla ya Yesu kurudi tena. Mpinga Kristo ni lazima afunuliwe, na ulimwengu mpaka upitie wakati wa mateso makuu na hukumu. Haya yanalingana na kabisa au kurudi Awamu ya Pili kwa Yesu. Yesu aliongea kuhusu ishara hizo za kurudi kwake katika Luka 21:28, “Basi mambo hayo yaanzapo kutokea (ishara za kurudi kwa Yesu Awamu ya Pili), changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia.”

Mwaka uliopita Oktoba ikikaribia kuisha, kabla ya sherehe za Haloweni, nilikuwa napitia duka moja kuu Califonia Kusini nikiwaona wakisimamisha Santa Claus, paa wa tuduji na mapambo mengine ya Krisimasi, lakini ilikuwa bado Oktoba, nikamwambia bibi yangu, “Tazama,

wanaziremba mapambo kuhusu Krisimasi! Hii ni nzuri sana! Napenda wakati wa kupeana shukrani! Akasema, “Hayo si mapambo ya kupeana au kutoa shukrani! Hayo ni ya Krisimasi!” Nikasema, “Nafahamu hayo! Lakini, pia nafahamu kuwa Shukrani huja kabla ya Krisimasi. Kwa hivyo ikiwa wanarembesha wakijitayarisha krisimasi, basi siku ya Shukrani iko karibu. Kwa hivyo, ni sawa, tunapoona dalili za kuja kwa pili, tunajua kuwa kunyakuliwa kuko karibu.

Yesu alielezea dalili za kuja kwake akijibu swali alililoulizwa, “Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?” (Mathayo 24:3). Yesu alikuwa amepitia hekaluni na wanafunzi wake wakataja jinsi mawe yalikuwa makubwa. Yesu akasema, “Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.” (Mathayo 24:2). Walipofika katika mlima wa Mizeituni, wakamuuliza Yesu, “Nayo ni nini dalili ya kuja kwako na mwisho wa dunia?” (Mathayo 24:3). Kwa hivyo hawakuwa wanauliza mpangilio mmoja tu wa dalili. Walikuwa wakiulizia dalili za kuharibiwa kwa Hekalu, na pia dalili za kumalizika kwa kizazi cha sasa cha serikali ya binadamu na kuja kwa ufalme wa Mungu.

Hawakuuliza kuhusu, na labda hawakuelewa, kuhusu kunyukuliwa kwa kanisa. Lakini Yesu akawaeleza dalili za kuharibiwa kwa hekalu na pia dalili za kurudi kwake mara ya pili. Anaponena kuhusu dalili za kurudi tena kwake, hunena pia juu ya mateso makuu. “Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe.” (Mathayo 24:21). Yesu pia awaonya, “Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu).” (Mathayo 24:15). Wakati mtakapoona uharibifu ukisimama katika mahali patakatifu, mtajua ni wakati wenu kutoka katika Jerusalemu na kukimbilia jangwani. Na baadaye, “Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbunguni zitatikisika; ndipo

itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi." (Mathayo 24:29-30).

Kabla ya kunyakuliwa, kunazo utabiri kadha ambazo lazima yatimizwe. lazima Mpinga Kristo afunuliwe na kuthibitisha ufalme wa Shetani kwa uwezo mkamilifu wakati wa dhiki kuu. Haya mambo mpaka yafanyike kabla ya kurudi Awamu ya Pili kwa Yesu. Lakini hakuna jambo ambalo mpaka lifanyike kabla ya kunyakuliwa kwa kanisa. Hiyo ndiyo sababu tunahimizwa tuwe macho na tuwe tayari, "kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa saa msiodhania Mwana wa Adamu yuaja. Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo." (Mathayo 24:44,46).

Yesu hapo akaanza kuwaeleza kwa mafumbo kadha wa kadha. Lililo la muhimu kwa kila mbaazi ni tuwe makini na tuwe tayari kumpokea wakati wowote. Kila fumbo lilirejelea umuhimu wa kuwa unyakuzi u karibu, yaani unaweza kutokea wakati wowote.

Katika Mbaazi/fumbo ya Wanawali Kumi twasoma, "Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara." (Mathayo 25:2). "Na hao walipokuwa wakaenda kununua, bwana arusi akaja, nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa. Halafu wakaja na wale wanawali wengine, wakasema, Bwana, Bwana utufungulie. Akawajibu akasema, Amin nawaambia, siwajui ninyi. Basi kesheni, kwa sababu hamuijui siku wala saa atakayorudi Mwana wa Adamu." (Mathayo 25:10-13). Sisitizo ni kukesheni na kuwa tayari, kwa sababu hamjui lini Bwana atakujia watumishi wake.

Mathayo 24:42-44 tunasoma, "Kesheni basi, kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili, kama mwenye nyumba angaliijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha, wala

asingaliacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani ndiye Mwana wa Adamu yuaja.

Kwa hakika naamini kuwa kanisa halitapitia katika Dhiki Kuu. Aliponena kuhusu Mateso Makuu katika Luka 21, Yesu alisema, “Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka haya yote yatakayotokea na kusimama mbele ya Mwana wa Adamu.” (Luka 21:36). Sasa ikiwa Yesu aniambia niombee jambo fulani, niamini nami, nitafanya hilo! Naomba, “Bwana nataka nihesabike nastahili kuepuka haya mambo yatakayotokea duniani.” Huu ndio muktadha wa Dhiki Kuu.

Tunaelezwa katika Ufunuo 1:19 ya kuwa kitabu kimegawanywa sehemu tatu. “Basi, uyaandike mambo hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo na yale yatakayokuwa baada ya hayo.” (Ufunuo 1:19). Katika sura ya kwanza Yohana aliambiwa, “Andika mambo unayoyaona”, na akaandika maono ya Yesu akitembea katikati ya vinara vya taa saba vya dhahabu, aliyekuwa na nyota saba katika mkono wake wa kiume. Aliandika kuhusu maelezo ya Yesu katika hali yake ya kutukuzwa.

Sura ya pili na ya tatu, Yohana anaandika juu ya “mambo yaliyopo.” Haya yanarejelea ujumbe wa Yesu kwa makanisa yale saba ya Asia. Naamini ya kuwa pia yanawakilisha makanisa saba halisi ya hiyo siku, pia yanaweza kuwakilisha majira au vipindi saba ya historia ya kanisa. Vilevile yanaweza kuwakilisha makanisa unayoweza kuyapata hivi leo.

Kuna makanisa leo ambayo yameacha upendo wa kwanza. Leo kuna makanisa ambayo yanakumbatia mafundisho ya Wanikolai. Kuna kanisa la Smirna linaloteseka ulimwenguni leo kama wale wanaoteseka nchini China, Sudan na mahali kwingine. Naamini kuna kanisa la Thiatira ambalo limefuata fundisho la “Umariamu.” Tunaona kanisa la Sardi linaoneshwa katika Uprotestanti uliokufa, “una jina la uhai nawe umekufa.” (Ufunuo 3:1).

Naamini kuwa kuna kanisa la Filadefia, kanisa lililodumu katika ukweli wa Neno. Linaweza kuwa halina nguvu lakini Bwana asifiwe "amewapa mlango uliofunguliwa mbele yao, na ambao hapana awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza Neno langu, wala hukulikana neno langu." (Ufunuo 3:8). Pengine hatukuitingisha nchi wala mbingu lakini shukuru Mungu tunaonyesha mfano hata ingawa mdogo!

Lakini pia kuna kanisa la Laodikia, ambalo limemweka Yesu nje. Anasimama mlangoni na kubisha, na kusema, "Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami." (Ufunuo 3:20).

Kwa hivyo naamini kuwa kuna nguzo tatu za kutumiwa ujumbe wa makanisa saba. Katika sura ya nne, mstari wa kwanza, anapomalizana na ujumbe kwa makanisa, Anatanguliza kingine kwa kutumia neno la Kigriki 'meta tauta' (Baada ya mambo haya), ambayo pia alitumia katika Ufunuo 1:19. Twahitajika tuulize, "Baada ya mambo yapi?" Baada ya mambo ya sura ya pili na tatu. Ni mambo ambayo yanahusu kanisa na tunasoma, "Baada ya hayo naliona, na tazama, mlango ukafunguka mbinguni, na sauti ile ya kwanza niliyoisikia kama sauti ya baragumu ikanena nami, ikisema, panda hata huku, nami nitakuonyesha mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo." (Ufunuo 4:1).

Baada ya agizo hili, Yohana alisema, "Mara tu nilipokuwa kwa roho: na lo tazama, kiti cha enzi kiliwekwa mbinguni, na Mmoja alikalia kiti cha enzi." (Ufunuo 4:2). Halafu akaelezea ilivyo kiti cha enzi cha Mungu pamoja na mviringo wa upinde wa mvua pamoja na malaika waliokuwa wanaabudu. Akaona viti ishirini na nne vya enzi ndogo zaidi vikiwa vimekaliwa na wazee wakitazama ibaada za mbinguni vile malaika wanatangaza sifa za milele, mienendo/tabia na utakatifu wa Mungu. "Hawapumuziki mchana wala usiku wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, akiyekuwako na aliyeko na

atakayekuja." (Ufunuo 4:8). Walivyokuwa wakitangaza utakatifu wa Mungu, wazee ishirini na wanne wanaanguka kwa nyuso zao, wanachukua mataji yao ya dhahabu na kuyatupa kwenye bahari ya glasi na kutangaza, "Umestahili wewe Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa." (Ufunuo 4:11)

Halafu mawazo ya Yohana yanatekwa na kuelrkezwa kwa hati ndefu kilichoandikwa nyuma na mbele ambacho kiliwekwa mihuri saba. Na Malaika mwenye nguvu akahubiri kwa sauti kuu, "Nani astahiliye kukifungua kitabu, na kuzivunja muhuri zake?" (Ufunuo 5:2). Na Yohana aandika, "Nami nikalia sana kwa kuwa hapakuonekana mtu astahiliye kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama." (Ufunuo 5:4). Naamini kuwa kitabu hiki ni hati ya kuthibitisha uenyeji/uumiliki ya dunia, kulingana na kanuni za Ukombozi wa Wayahudi. Kulikuwa na wakati uliokubalika ambao ungekomboa mali uliyopeana au uliyopoteza kama ungehitimisha mahitaji yaliyokuwa katika hati ya wokovu/ukombozi, ulivyo wakilishwa na kitabu hicho. Hayo yaonyesha katika hekaya ya Ruthu wakati wa Boazi alipolikomboa shamba lililokuwa la Elimelechi ili apate biarusi. Pia twaona mfano wa Yesu aliyenunua na kugharamia bei ya kuukomboa ulimwengu ili apate bi arusi wake ambaye ni kanisa.

Huko mbinguni, twamwona Yohana akilia kwa sababu, kulingana na Kanuni za Kiyahudi kama hautaweza kuukomboa mali yake wakati uliotengwa, huridhiwa na mwenyeji mpya milele. Una nafasi moja tu, ukishindwa mali huchukuliwa kabisa na mwenyeji mpya. Wazo la ulimwengu kuwa milele chini ya mamlaka na utawala wa shetani, lilikuwa la huzuni sana, likamfanya Yohana akunyate na kulia kwa uchungu mkuu, mpaka mzee mmoja alipomwambia, "Usilie; tazama, Simba aliye kabila ya Yuda, shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kila kitabu, na zile muhuri zake saba." (Ufunuo 5:5). Yohana asema hakumwona kama

simba wa kabila la Yuda. Alimwona kama mwana kondoo aliyechinjwa. Isaya asema, “Maana alikuwa mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi katika nchi kavu, Yeye hana umbo la uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani…. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu, Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.” (Isaya 53:2,5).

Katika Ufunuo sura ya tano twasoma, “Akaja, akakitwaa kile kitabu katika mkono wake wa kiume yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi. Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu. Nao waimba wimbo mpya wakisema, wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme wa makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi.” (Ufunuo 5:7-10).

Tunapotazama haya maneno ya wimbo kwa makini, tunatambua kuwa ni kanisa pekee linaloweza kuyakariri. Wakati Bwana yu mbinguni akipokea hati ya kumiliki dunia, tutakuweko tukimshuhudia akipewa kitabu kutoka kwa mkono wa kiume wa aliyeketi kwenye kiti cha enzi. Tutajiunga kuimba pambio la fahari, “Wastahili wewe kukitwaa kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, uka mnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa, na taifa.” (Ufunuo 5:9). Katika Luka 21, Yesu aliwaeleza wanafunzi wake juu ya dalili zitakazoashiri Kurudi kwake Mara ya Pili na pia Dhiki Kuu itakayotangulia mwisho wa nyakati. Alisema, “Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu.” (Luka 21:36).

Wakati Dhiki Kuu utakapotokea duniani, natarajia kuwa mbinguni nimesimama mbele ya Mwana wa Adamu na nikiimba ustahilivu wa

Mwana-Kondoo. Ni kanisa pekee linaloweza kuimba wimbo huu wa ukombozi. Tukifuatilia nyakati, tutapata kuwa kanisa linaimba wimbo huu katika sura ya tano, kabla ya kufungulia kwa kitabu sura ya sita, na hayo yatangulia wakati wa Utesi Mkuu duniani. Tunasoma pia kwamba, "Ametukomboa sisi kwa Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa, na taifa ukawafanya kuwa ufalme wa wakuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi." (Ufunuo 5:9-10).

Tutazama kanisa limesimama mbele ya Mwana wa Adamu na Yesu, wakizungumza kuhusu Dhiki Kuu, wakisema, "Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu." (Luka 21:36). Niamini mimi, ninataka kuwa pamoja na kikundi hicho huko juu!

Ufunuo sura ya sita inaanza kwa maelezo ya dhiki kuu. Kila wakati Bwana anapofungua muhuri hukumu inayoungana inaachiliwa duniani. Muhuri wa kwanza unapofunguliwa, Yohana anaandika, "Nikaona, natazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda ana uta, akapewa na taji, naye akatoka, akishinda tena apate kushinda." (Ufunuo 6:2). Naamini kuwa huu ni Ufunuo wa Mpinga Kristo. Wengine hu amini kuwa mpanda farasi huyu ni Yesu Kristo! Lakini, tutakapokichunguza kifungu hiki zaidi, tutapata ya kuwa inafuatwa na vita, njaa, ukame, umwagaji damu na robo ya watu wanouawa. Haya hayaonekani kama ufalme wa Mungu, na kurudi kwa fahari kwa Bwana. Naamini ni Mpinga Kristo.

Naamini kuwa vikosi na nguvu za Mpinga Kristo zimo duniani leo na kile ambacho kinawazuia kumiliki dunia ni uweko wa kanisa. Tuna nguvu hafifu, sio nyingi, lakini inatosha kuzuia nguvu za (giza) Shetani kumiliki kabisa. Siamini kuwa Mpinga Kristo anaweza kumiliki dunia mpaka kanisa linyakuliwe.

Paulo, katika 2 Wathesalonike sura ya pili asema, "Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yupo azuiaye sasa, hata

atakapoondolewa. Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye ni Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake." (2 Wathesalonike 2:7-8). Hii inaambatana na Ufunuo sura ya sita kifungu ambapo Kanisa liko mbinguni Yesu anapochukua kitabu. Anapoanza kuachalia hicho kitabu, hukumu unaachiliwa juu ya dunia. Ni wakati ambapo ghadhabu ya Mungu inaachiliwa.

Katika Warumi 5:9, Paulo anatuambia, "Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tukaokolewa na ghadhabu kwa yeye." Anarudia haya kwa Wathesalonike wa Kwanza 5:9, "Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana yetu Yesu Kristo."

Sisi, kama kanisa "hatuhesabiwi kwa ghadhabu." Katika Warumi 1, Paulo aliandika, "Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu." (Warumi 1:18). Sio kwa hali ya Mungu kuhukumu wenye haki na wenye dhambi.

Sasa ni kweli ya kuwa Wakristo katika huu ulimwengu watakuwa na dhiki. Ulimwengu utatuchukia, kwa hivyo hatufai kushangazwa na mateso mahangaiko. Yesu alisema, "Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia nyinyi." (Yohana 15:18), na "Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu." (Yohana 16:33). Kwa hivyo, ulimwenguni mnayo dhiki. Lakini ni nini chanzo cha dhiki ya kanisa? Sio Mungu! Shetani ndiye chanzo cha dhiki.

Kama Shetani ndiye chanzo cha dhiki, unaweza kutarajia kuwa wana wa Mungu ndio watakaoteswa. Lakini wakati Mungu ndiye chanzo cha hukumu hilo linabadilisha kila kitu. Mungu tayari amehukumu dhambi zetu

msalabani mwa Yesu Kristo. Yesu alitwikwa hukumu ya Mungu kwa uovu wetu.

Kumbuka malaika waliokuwa njiani kuelekea kuharibu Sodoma? Walipitia na kumtembelea Ibrahimu. Wakasema, “Tumharifu Ibrahimu yale tunayotarajia kutenda?” Wakaamua, “Mbona tusimwambie?" Kwa hivyo wakamjulisha ya kuwa dhambi za Sodoma zimepanda na kufika mbinguni na walikuwa wanataka kuhakikisha hayo na kuuharibu mji.

Ibrahimu akawaomba wasubiri kwa kuwa mpwa wake Lutu alikuwa anaishi hapo. Akasema, “Je! Utaharibu mwenye haki pamoja na mwovu? Huenda wakawapo wenye haki hamsini katika mji; utaharibu, wala hutauacha mji kwa ajili ya hao hamsini waliomo?” Bwana akasema, “Nikiona katika Sodoma wenye haki Hamsini mjini, nitapaacha mahali pote kwa ajili yao.” Ibrahimu akajibu akasema, “Huenda wakapunguka watano katika wale hamsini wenye haki, Je! Utaharibu mji wote kwa kupungua watano?” Akasema, “Nikiona kuna arobaini na watano, sitauharibu mjii.” Akazidi tena kusema naye, akinena, “Huenda wakaonekana humo arobaini?” Akasema, “Sitafanya kwa ajili ya hao arobaini.” “Huenda wakaonekana huko thelathini?” Akasema, “Sitafanya nikiona humo thelathini.” Akasema “Tazama, nimeshika kusema na Bwana, huenda wakaonekana huko ishirini?” Akasema, “Sitaharibu kwa sababu ya hao ishirini.” Akasema, “Bwana asiwe na hasira, nami nitasema mara hii tu, huenda wakaonekana huko kumi?” Akasema sitaharibu kwa ajili ya hao kumi.” (Mwanzo 18:23-33).

Na ni nini kilitendeka? Wakati malaika walipoingia mji wa Sodoma, walipata mwenye haki mmoja tu, Lutu, amekaa mlangoni. Lutu alijua hulka/uovu za Wanasodoma. Petro atujulisha ya kuwa Roho yake mwenye haki ilikuwa inasumbuliwa na jinsi walivyokuwa wakiishi. Lutu, bila kutambua kuwa walikuwa malaika, akawaalika kwake nyumbani. Usiku huo, wanaume wa Sodoma wakaja kwake, wakagonga mlango wakisema, “Wapi wale watu waliokuja kwako usiku huu? Uwatoe kwetu,

tupate kuwajua." (Mwanzo 19:5). Walitaka kuwanajisi. Lutu akajibu, "Basi nawasihi ndugu zangu, msitende vibaya hivi." (Mwanzo 19:7).

Malaika walimwingiza Lutu ndani mwa nyumba wakati umati ulipoanza kuupiga mlango karibu wauangushe. Kisha wakawapiga watu waliokuwa mlangoni kwa upofu. Tunajulishwa waliendelea usiku kucha kujaribu kupata mlango. Asubuhi yake malaika walilazimika kumbeba Lutu kumwondoa Sodoma kwa kuwa hawangeweza kuuharibu akiweko.

Lutu ni aina ya kanisa ambayo itakombolewa. Petro anatwambia Bwana "alimwokoa Lutu, yule mwenye haki aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa hao wahalifu; (maana mtu huyu mwenye haki akikaa kati yao, kwa kuona na kusikia, alijitesa roho yake yenye haki, siku baada ya siku, kwa matendo yao yasiyo na sheria). Bwana anajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu." (2 Petero 2:7-9). Mungu atawaokoa wenye haki na pia atahifadhi waovu kungojea siku ya hukumu.

Jambo la msingi ni kuwa Bwana wa ulimwengu ni mwenye haki. Ni mwenye haki kwa hivyo hatawaharibu wenye haki na waovu. Kwa kuwa Mungu ndiye chimbuko la hukumu, basi Mungu atawaokoa wenye haki kutoka kwa hukumu. Hapo mbele, Mungu alikuwa amehukumu ulimwengu kwa uovu kupitia kwa Gharika. "Bwana akaona kuwa maovu ya binadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni wake ni baya tu siku zote." (Mwanzo 6:5). Lakini kati ya waovu wote ulimwenguni kulikuwa na mwenye haki mmoja, Nuhu. Mungu akamdumisha na kumhifadhi Nuhu na alipoachilia hukumu yake. Nuhu alikuwa amewekwa muhuri na akaweza kupitia kwa salama wakati wa Gharika, sawa na jinsi Mungu atakavyohifadhi Elfu Mia Moja na Arobaini na Nne katika Ufunuo sura ya saba ambao hawakuumizwa na utesi wa hukumu. Nuhu ni aina ya wale Elfu Mia Moja Arobaini na Nne waliopigwa muhuri na kupitia hukumu.

Wakati wa nyakati hizo, kulikuwa pia na mtu mwingine mwenye haki, Henoko. “Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa.” (Mwanzo 5:24). Henoko ni mfano wa kusisimua kwa kanisa. Alinyakuliwa.

Siamini kuwa kanisa litapitia Dhiki Kuu. Lakini kuna Maandiko watu fulani wanayotumia kujaribu kuonyesha kanisa litakuwako humo. Hoja moja inayotumiwa inategemea tafsiri ya ‘parapanda ya mwisho.’ Katika 1 Wakorintho 15, Paulo ananena juu ya Kunyakuliwa anaposema, “Angalieni, nawaambia ninyi siri, hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika.” (1 Wakorintho 15:51–52). Wengine hujaribu kuunganisha haya na tarumbeta saba za hukumu katika Ufunuo na wasema kuwa tarumbeta ya saba ndiyo ya mwisho. Wanaona huu kama ushahidi kuwa hatutanyakuliwa mpaka tarumbeta ya mwisho ilie, ambayo ni hukumu ya mwisho.

Kuna mawazo kadhaa ambayo yanatokana na haya. Kwanza, tarumbeta saba za hukumu katika Ufunuo zinapatiwa malaika saba wapulize na walete hukumu zinazoambatana ulimwenguni. Tukichunguza ni nani anayepuliza kila moja ya tarumbeta hizi, tunawaona wote ni malaika. Katika 1 Wathesalonike 4:16, Paulo anaongea kuhusu kunyakuliwa kwa kanisa, “Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu, nao waliokufa katika Yesu watafufuliwa kwanza.” (1 Wathesalonike 4:16). Parapanda ya Kunyakuliwa sio ya malaika, ni parapanda ya Mungu!

Baada ya malaika wa nne kupuliza parapanda yake, kuna sauti kuu, “Ole, ole, ole, wao wakaao juu ya nchi! Kwa sababu ya sauti zisaliazo za baragumu za malaika watatu, walio tayari kupiga.” (Ufunuo 8:13). Baada ya baragumu ya tano kupigwa, tena sauti inasema, “Ole wa kwanza

umekwisha pita. Tazama, bado ziko ole mbili zinakuja baadaye." (Ufunuo 9:12). Ni wazi kuwa ni ole ambazo zinatangaziwa wale walio ulimwenguni. Lakini kunyakuliwa sio ole! Ni fahari!

Hoja nyingine inayotumiwa ni Ufunuo sura ya 20. Yohana anapotazama vikundi tofauti mbinguni. Tukianzia mstari wa nne twasoma, "Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya Neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chopa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu. Hato wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimia miaka elfu." (Ufunuo 20:4-5). Hoja wanayoleta ni kuwa katika kufufuka kwa mwanzo, Yohana anaona wale waliokatwa vichwa kwa ajili ya kumshuhudia Yesu, na wale hawakumsujudia yule mnyama wale kuipokea chapa waliishi na kutawala na Kristo miaka elfu. Wengine husema huu ni ushahidi madhubuti ya kuwa kanisa litapitia utesi na kufa kwa ajili ya injili.

Lakini wacha tusome tena. Katika mstari wa nne, twaona viti vya enzi, na kwa wale walio vikalia, hukumu ikatolewa. Tuchunguze tuone hawa washindi ni akina nani? Kwa ujumbe wa washindi, kwa kanisa, twasoma, "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi." (Ufunuo 3:21). Yohana aona kanisa kama sehemu ya kufufuka kwa kwanza. Pia anaona wale watakaouliwa wakati wa Dhiki Kuu kwa sababu walikataa kupokea Chapa ya Mnyama. Hii ndiyo idadi kubwa inayopatikana katika sura ya saba ambapo mzee nasema, "Je! Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, hao ndio wanaotoka katika Dhiki ile iliyo Kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo." (Ufunuo 7:13-14).

Lakini tazama kwa makini kuwa wanasimama katika hekalu yake takatifu wakimtumikia bila kusita mchana na usiku. Kanisa ni bi-arusi wa Yesu. Yesu alisema, "Siwaiti tena watumwa; maana mtumwa hajui atendalo Bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu." (Yohana 15:15). Kwa hivyo, tunalo kundi hili la pili linalojumuishwa mitume wafia dini wafao wakati wa Dhiki iliyo Kuu. Watakuwa sehemu ya ufalme, lakini kanisa litakuwa limenyakuliwa kitambo! Na kuna njia bora zaidi ya kwenda. Kwenye ufalme wa Mungu kuliko kuwa mfiadini baada ya kupitia Dhiki Kuu.

Katika Ufunuo 10:7 twasoma zaidi juu ya baragumu ya saba. Yasema, "Isipokuwa katika siku za sauti ya malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiria watumishi wake hao manabii." (Ufunuo 10:7). Siku ni kwa wingi, lakini unyakulizi utakuwa mara moja, kufumba na kufumbua. Kwa hivyo, hatuwezi kwa hakika tukaunganisha tarumbeta ya mwisho na baragumi ya saba katika Ufunuo. Tofauti kabisa, tarumbeta itakapolia, tutabadilishwa mara moja.

Katika injili ya Mathayo, Yesu alisema, "Lakini mara, baada ya dhiki siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika; ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao waamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika wake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu hadi mwisho huu." (Mathayo 24:29-31). Hapo twaona mara baada ya dhiki ya siku hizo, Yesu atajitokeza kwa ulimwengu wote.

Baadaye atakusanya wateule wake kutoka pembe nne, kutoka upeo mmoja wa ulimwengu hadi mwingine. Lakini wengine wauliza, "Si kanisa

ndilo wateule?" Ndio, kanisa ndilo wateule lakini pia Wanaisraeli. Hapa wateule linarejea Waisraeli. Unaweza kuangalia vifungu vingine katika Agano la Kale ambapo jambo hili naelezwa. Mungu atakusanya Wayahudi kutoka pembe zote za Dunia. Katika kifungu hiki Yesu anaongea juu ya wateule wake, taifa la Israeli sio kanisa. Isaiya anasema, "Naye atawatwekea mataifa bendera, atawakutanisha watu wa Israeli waliotupwa, atawakusanya watu wa Yuda waliotawanyika, kutoka ncha nne za dunia." (Isaiya 11:12). Israeli itakusanywa pamoja tena.

Je! Na kuhusu Maandiko yaneneyao juu ya Mpinga Kristo akipigana na mitume? Danieli 7:21 asema, "Nikatazama na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda." Katika Ufunuo 13:7 twasoma, "Tena akapewa (Mpinga Kristo) kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila, na jamaa na lugha na taifa." Ni nani watakatifu? Hawawezi kuwa kanisa kwa sababu Yesu alimwambia Petro, "Na ni juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda." (Mathayo 16:18). Hakika kufanya vita na watakatifu na kushinda, inamaanisha kuwa watakatifu wa Kiyahudi sio kanisa.

Siamini kuwa kanisa litamwona Mpinga Kristo amewezeshwa au amepewa nguvu humu duniani. Singestaajabu kama Mpinga Kristo akawa ni mmoja wa viongozi wakuu humu duniani. Lakini siamini kuwa kanisa litamwona Mpinga Kristo akionyesha nguvu zake kamili duniani.

Katika 2 Wathesalonike 2, Paulo anaponena juu ya huyo muasi, mwana wa kuzimu, asema, "Na sasa lizuialo mwalijua, yule apate kufunuliwa wakati wake. Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yuko azuiaye sasa, hata atakapoondolewa. Hapo ndipo atakapofunuliwa yule muasi, ambaye Bwana Yesu atamuua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa Ufunuo wa kuwapo kwake." (2 Wathesalonike 2:6-8).

Siamini kuwa Mpinga Kristo anaweza kuchukua utawala na mamlaka ya dunia kanisa likiwa bado lipo. Naamini kuwa Roho Mtakatifu katika kanisa ndiye nguvu inayozuia nguvu za giza kuzunguka na kushinda ulimwengu sasa. Lakini mara tu kanisa litakapoondolewa, hakutakuwa na kizuizi chochote cha nguvu za giza kuchukua mamlaka. Kile kinachozuia kitazuia mpaka atolewa. Ndipo huyo muasi [mtu wa dhambi], mwana wa kuzimu, atakapofunuliwa. Hii ndiyo sababu sitafuti kujua Mpinga Kristo ni nani. Hii ni njama nyingine danganyifu na ya kupotoshwa na Shetani, inayowafanya watu wamtafute Mpinga Kristo badala ya Yesu Kristo.

Sababu watu wengine wanachanganya unabii ni wanayofanya matukio yote yawe ya ki roho na wanalichukua kanisa kuwa Israeli. Wasema Mungu amemalizana na taifa la Israeli kwa sababu walimkataa Masihi. Wanaamini kuwa Mungu ametupilia mbali Israeli na kuchukua kanisa kwa niaba yake, na sasa kanisa ndilo Israeli ya Mungu. Wanachukua unabii unaohusu Israeli na kuufanya wa kanisa. Ukifanya hivo, inachanganya picha yote ya unabii.

Kama jua lilichomoka asubuhi ya leo, basi Agano la Mungu na Israeli bado lipo. Alisema, “Kama vile jua linazidi kuchomoza, Agano langu na Israeli inadumu.” Mungu bado ana haja na Israeli, bado anawadhamini. Katika kitabu cha Hosea, Mungu asema, “Nenda tena na umrudishe tena, mwoshe na umsafishe na umrudie.” Danieli mlango wa tisa inasema kuwa Mungu bado ana mkataba wa miaka saba wa kutimiza na Waisraeli, ambapo atafanya biashara nao moja kwa moja.

Haupati mfanoau kiekelezo cha unyakuzi katika Agano la Kale. Henoko ni aina ya kanisa aliyebadilishwa kabla ya gharika. Danieli, naamini pia, ni aina ya kanisa. Kumbuka Nebukadreza alipojenga sanamu yake kuu na kutaka kila mtu kuisujudia. Naamini kuwa huu ni mfano wa sanamu ambayo Mpinga Kristo atajenga na kuiweka hekaluni na kutaka kila mtu aiabudu. Nebukadreza alitaka kila mtu kuisujudia sanamu hiyo nyimbo zilipochezwa. Kwa hivyo nyimbo zilizochezwa, wote walisujudu na

kuabudu sanamu, isipokuwa Shadraka, Meshaki na Abednego. Wakalidayo walimjulisha Nebukadreza, “Kuna wavulana watatu hapa wa Kiyahudi ambao hawakuabudu. Nyimbo zilichezwa na wanasimama tu!”

Kwa hivyo akawaita hao vijana watatu wakiyahudi, na akasema, “Ni nini hii ninasikia? Hamkusujudu? Tutawapa nafasi nyingine, lakini msiposujudu mtarushwa kwenye tanuri ya moto!” Wakamjibu, “Mfalme! Eeh mfalme hamna haja kukujibu katika neno hili, kwa sababu Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa kutoka kwa tanuri ile uwakayo moto, na kama si hivyo, hatutakubali kuiabudu miungu yako wala kuisujudia sanamu yako!” Napenda aina hii ya ujasiri! Hauwezi kusimamisha au kuzuia watu kama hao!

Nebukadreza alighadhabika sana akaamuru tanuri itiwe moto mara saba zaidi kuliko ilivyo awali kuwashwa tena. Wayahudi watatu walirushwa ndani, na watu waliowarusha, moto ukawauwa wote kwa sababu waliukaribia. Lakini vilivyochomeka kwa Shadraka, Meshaki na Abednego ni kamba Wakalidayo walizowafunga nazo. Nebukadreza akatazama motoni na akauliza, “Ni wangapi tuliwatupa ndani pale?” Wakajibu, “Watatu ewe mfalme.” “Mbona nawaona wanne? Nao wanatembea katikati ya moto hali hawana dhara na sura ya yule wa nne ni mfano wa Mwana wa Mungu. Enyi Shadraka, Meshaki na Abednego, tokeni huko!”

Walipotoka ndani, moto haukuwa umewadhuru hata kidogo hata nywele za vichwa vyao hazikuteketezwa. Hata harufu ya moto haikuwapata hata kidogo. Kila mtu alistaajabu naye Nebukadreza aliyejulikana kuwa mkuu kwa kutoa amri, akasema, “Ninatoa amri ya kuwa hakuna Mungu kama wa Shadraka, Meshaki na Abednego aliyeweza kuokoa kutoka tanuri ya moto.”

Lakini Danieli alikuwa wapi wakati haya yote yalikuwa yakitendeka? Unadhani Danieli alisujudia mbele ya sanamu? Ikiwa ni hivo, wamjua Danieli aliye tofauti kutoka kwa yule ninayemjua! Kumbuka katika sura ya

kwanza, Danieli hatajitia unajisi, hata kwa chakula cha mfalme. Sidhani kuwa mtu alikuwa na azimio kama hilo moyoni angehisi hata kidogo kusujudu. Pengine Danieli alikuwa ametumwa na mfalme kumfanyia kazi mahali pengine. Danieli anakuwa kama mfano wa kanisa ambalo litaondolewa wakati Mpinga Kristo atakapoinua sanamu yake na kuwataka watu wote waiabudu. Sisi, ambao ni kanisa tutakuwa tukihudumu pahali pengine, katika mandhari ya mbinguni!

Ukitambua kuwa Mungu ndiye chanzo cha dhiki, moja kwa moja watu wa Mungu hawatapitia dhiki ile. Haitakuwa haki au kufuatana na haki za Mungu kuhukumu mwenye haki pamoja na wenye dhambi.

Petro asema kuwa Mungu "wala hakuuachilia ulimwengu wa kale, bali alimhifadhi Nuhu, mjumbe wa haki, na watu wengine saba, hapo alipoleta Gharika juu ya ulimwengu wa wasiomcha Mungu." (2 Petero 2:5). Mungu aliwahifadhi wenye haki lakini alipoleta Gharika juu ya ulimwengu wa wasioamini Mungu. Hivi ndivyo vile hukumu ilivyo. Inawalenga wasiomcha Mungu. "Tena akaihukumu miji ya Sodoma na Gomora, akiipindua na kuifanya majivu, akaifanya iwe ishara kwa watu watakaokuwa hawamchi Mungu baada ya haya." (2 Petero 2:6). Lakini "akamwokoa Lutu, yule mwenye haki na aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa hao wahalifu; maana mtu huyu mwenye haki akikaa kati yao, kwa kuona na kusikia, alijitesa roho yake yenye haki, siku baada ya siku, kwa matendo yao yasiyo na sheria; basi, Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya kuhumu." (2 Petero 2:7-9). Hii inatangaza wazi lengo au nia ya Mungu.

Naamini kuwa kupitia watu wa Agano la Kale kama Lutu, Nuhu, Henoko na Danieli, tunaona ukweli kuwa kanisa halitakuwa hapa wakati wa Dhiki Kuu. Maandiko yanasema waziwazi, "Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana yetu Yesu Kristo." (1 Wathesalonike 5:9). "Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki

katika damu yake, tukaokolewa na ghadhabu kwa yeye.” (Warumi 5:9). Na “Kwa ghadhabu ya Mungu inaonekana kutoka mbinguni dhidi ya dhambi za binadamu, anayeshikia ukweli kwa watenda dhambi;” (Warumi 1:18) - lakini hili halimwelezei mwana wa Mungu.

Naamini kuwa Mungu alitaka kila kanisa liamini kuwa ndilo ya mwisho. Kuamini haya kuna umuhimu mara tatu. Kwanza, inatuhimiza na kutusisimua kwa kazi tuifanyayo, kuhubiri Injili. Hatuna wakati, kwa hivyo tunahitajika, “na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzuiayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu.” (Waebrania 12:1). Yale tuliyoamuliwa kufanya tuyafanye haraka hakuna wakati tunahitaji kuhubiri injili kwa sababu hamna muda. Bwana anarudi karibuni!

Pili, inatupa mwelekeo unaofaa juu ya mali ya kiulimwengu. Mali yote ya ulimwengu itachomeka. Tunaiweka raslimali yetu yote katika mambo ya humu ulimwenguni lakini yote itachomeka. Yesu alisema, “Bali jiweekeni hazina mbinguni.” (Mathayo 6:20). Alisema, "Tumieni udhalimu wa hazina kwa lengo la uzima wa milele.” Mungu akikubariki na mali vyema! Lakini inatulazimu tuitumie kwa lengo la uzima wa milele. Kwa kuwa Yesu yuaja tunapata mwelekeo unaofaa kati ya vitu vya Ki-Roho na mali ya humu duniani. Twatambua kuwa mali ya ulimwenguni yatapita kwa haraka na ni vitu tu vya Ki-Roho ndivyo vitadumu milele. Tukijua kuwa tuna maisha mara moja tu ambayo yanapita, twatambua kuwa ni yale tunayofanya Kristo yatadumu hapo twapata mwelekeo unaofaa.

Sababu ya tatu ambayo ni dhibitisho kuwa Yesu ataka kila kizazi kiamini ndicho cha mwisho ni kudumisha utakatifu maishani mwetu. Yesu alisema, “Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo.” (Mathayo 24:46). Sitaki Bwana atakaporudi anipate nikitazama sinema yenye kutia ashiki au nikizuru sehemu tofauti za kutia ashiki katika mtandao. Tafakari! Kuamini kuwa Yesu anaweza kurudi wakati wowote, hudumisha utakatifu maishani mwetu. Bwana Yesu

anaweza kurudi leo! “Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo.” Yohana alisema, “Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo. Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu.” (1 Yohana 3:2-3). Inatupatia tumaini la kujitakasa. Ndivyo maana naamini kuwa ni muhimu tuweke imani hii iliyotofauti ya kuamini kukaribia kwa kurudi kwa Yesu na tusijitie katika tuhuma.

Natarajia Bwana wa mbingu aje aninyakue ili niweze kuwa naye. Kama alivyosema, “Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimamna mbele za Mwana wa Adamu.” (Luka 21:36). Hilo ndilo ombi langu, na ni tumaini langu nitakuweko, na jambo la kusisimua ni kuwa linaweza kufanyika wakati wowote! Naamini kuwa Bwana alitaka sisi tuishi na tumaini hili kwa nyakati za kanisa.

Na naamini pia kuwa tumaini la kutokea kwa utukufu/sifa wa Mungu wetu mkuu na Mwokozi Yesu Kristo ndilo litatumiwa na Mungu kama chache ya kuchochea ufuaji katika kanisa. Hili ndilo linalochochea ufuaji leo, kuwa hakuna muda mwingi. Bwana yuaja karibuni. Tunaishi ukingoni mwa wakati kabisa, kama Paulo alivyosema, “Naam, tukijua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi umekwisha kuwadia; kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini.” (Warumi 13:11).

Mungu atusaidie kudumisha imani hiyo iliyobarikiwa na kuileta kwa watu wote ili:

1. Waweze kutambua umuhimu mkuu wa kuishi na Yesu kabisa.
2. Wawe na mwelekeo unaofaa kuhusu mambo ya ulimwengu ambayo kwa upesi utuzingira na kutuvuta nyuma.
3. Waweze kuishi maisha ya utakatifu; na

4. Waweke mioyo na maisha yao safi/ takatifu katika kumhudumia Bwana wakijua anaweza kurudi wakati wowote.

Nataka kuwa macho na nataka kuwa tayari kumlaki atakapokuja. Sitaki kuwa nafanya jambo linizuiayo na kunivuta nyuma. Nataka kuwa tayari kwa Bwana wangu.

Naamini ni muhimu mno kutangaza mafunzo haya ya kunyakuliwa na kuwahimiza watu wawe macho na wakitarajia kwa sababu, bila haya, tumaini lipi tunalo duniani leo? Twahitajika kuwahimiza watu na ukweli kuwa siku bora yaja karibuni. Kuwa tayari! Bwana anarudia watu wake, na atatuchukua tukae naye.

# 9

## KWA KUWA MLIANZIA KATIKA ROHO

*“Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lolote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu. Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa Agano Jipya; si wa andiko, bali wa Roho.”* (2 Wakorintho 3:5-6)

Calvary Chapel ni kazi iliyoanzishwa na Roho Mtakatifu. Kila mfumo mpya na mkuu huzaliwa na Roho. Tukitazama historia ya kanisa ya aina tofauti ya mwondoko wa Mungu, tunagundua kuwa zote zilizaliwa na Roho. Lakini isitoshe mwondoko ule wa Mungu kihistoria ulionekana kuzaliwa Ki-Roho mpaka kilele cha kutafuta kutosheleka kwa mwili. Hii inaonekana kuendelea katika historia ya kanisa. Mwondoko uliokuwa hai kwa Roho wafifia kwa sababu ya kaida ya dini.

Tambiko si kitu bali na kufuata utaratibu ule ule, na ile tofauti iliyoko katika kufanya mambo kwa mazoea, na kaburi ni kwa upana wake na kina chake. Tunaona nguvu za kanisa zikipeanwa katika vyombo/mashine zinazosaidia maiti kuonekana ni kama bado lina uhai. Kusudi lote linaelekezwa kuzuia mwondoko usikufe. Tunaamini kuwa kama mpango hauwezi kujiendeleza wenyewe, jambo la rehema sana la kufanya ni kuwachia ukufe.

Katika kitabu cha Waamuzi tunasoma juu ya mviringo wa kutokuwa waminifu kwa Waisraeli. Ni jambo la kuudhi sana ukiona vile Waisraeli walivyotenda mabaya mbele za Bwana, na vile Bwana alivyowapeana kwa adui zao. Wangekaaa utumwani, na baada ya miaka aroibaini wangemlilia Mungu. Mungu angewasikia na angetuma mkombozi na mambo yangebadilika kwa muda. Lakini Waisraeli wangetenda mabaya tena mbele za Mungu na tena wangeenda utumwani. Tunaona kurudiwa kwa

jambo hili katika maisha yetu. Wakati mambo yanaenda vizuri, tuna uzoevu wa kuzembea. Na wakati tunapoingia katika shida, tunamlilia Mungu. Kila wakati nikisoma kitabu cha Waamuzi, ninawakasirikia sana wana Waisraeli. Nafikiria, "Unawezaje kumuasi Bwana? Huwezi ukaona kinachoendelea? Huoni mafuatano ya mambo yanayotendeka?"

Nikitazama historia ya kanisa, ninaona kitu sawa. Mungu anainua mwondoko mpya. Unazaliwa na Roho. Kuna kufurahia na ufufuo. Roho anatembea kwa nguvu. Tazama aina mbalimbali za mwondoko wakati Mungu aliwatumia watu kama vile John Wesley na Martin Luther. Ni dhahiri kuwa nguvu na upako wa Roho Mtakatifu ulikuwa juu yao. Lakini tukitazama makanisa ya Methodist hata Lutheran leo, nikitaja machache tu, yamejawa na usasa. Kuna uhaba wa Roho, na hata kupinga nguvu na karama za Roho. Lakini hii miondoko ilizaliwa na Roho. Na ndipo inatoweka historia ya kanisa. Mungu anainua kazi mpya na anaanza mwondoko mpya Calvary Chapel ni mojawapo ya kwanza ya hizi. Roho wa Mungu alitembelea na anatembea na ameinua kazi mpya. Ilianzishwa kwa Roho. Kama vile Mungu alivyomwambia Zekaria. "Si kwa uwezo, wala nguvu, bali ni kwa Roho yangu asema Bwana wa majeshi." (Zekaria 4:6).

Paulo naye aliyaandikia makanisa ya Galatia, makanisa yalianza katika Roho, na akawakemea, "Je! Mmekuwa wajinga namna hii? Baada ya kuanza katika Roho, mnataka kukamilishwa sasa katika mwili?" (Wagalatia 3:3). Mungu ataenenda kwa umbali mno kuhakikisha kuwa viongozi wake wateule wanamtumainia kwa Roho na sio nguvu zao au hekima. Ni jambo la ajabu ukiwatazama wale ambao Mungu ametumia, wale ambao amewainua kuongoza watu katika njia za Bwana.

Musa ni mfano mmoja. Unakumbuka hadithi ya kichaka kilicho waka moto bila kuteketea. Wakati Mungu alipomwita Musa mwanzoni alikataa, akisema, "Mimi ni nani, hata niende kwa Farao, nikawatoe wana wa Israeli watoke Misri?" (Kutoka 3:11). Musa akamwambia, "Mimi sijiamini. Mimi ni

nani? Nimekuwa humu kwa miaka arobaini." Natafakari kuwa alitarajia kuchunga kondoo maisha yake yote yaliyombakia. Alitazama kuwa huu ndio uliokuwa urithi wake maishani. Kwa hivyo Bwana alipomwita alimjibu, "Mimi ni nani? Sina ujasiri wowote, Bwana."

Sasa, inashangaza kuwa alianza kwa imani kuu, lakini Mungu aliimwaga nje. Inashangaza kuwa alikuwa na hisia ya majaliwa siku mmoja. Stefano anatuambia kuwa alifikiria kuwa Waisraeli wangeelewa kuwa Mungu alimchagua yeye kuwaongoza, lakini hawakuelewa mpaka mara ya pili (Matendo 7). Ni mfano mzuri wa kutofautisha kati ya kazi za kimwili na kazi za Roho. Musa kwanza alidhania atafanya kazi ya Mungu na nguvu za kimwili. Lakini kwa nguvu zake hakuweza hata kumzika Mumisri. Yakini alipokuwa akiongozwa na Roho, Waisraeli waliweza kulizika jeshi lote la Wamisiri.

Nafikiri kila mmoja wetu anaweza jilinganisha na aliyipitia Musa. Mara nyingi tunaanza katika mwili kufikia mwito wa Mungu maishani mwetu. Mara nyingi tunaanza katika nguvu za mwili na tunajipata tumeshindwa. Naamini kuwa mtu akishindwa kwa mwili, anaelekea jangwani na anaacha huduma, na mara nyingi harudi tena. Anakufa moyo na kukata tamaa, kwa sababu alijaribu katika mwili lile ambalo alihisi ni mwito wa Mungu katika maisha yake.

Musa alitenda lile. Alihisi mwito wa Mungu katika moyo wake. Alijua kuwa Mungu alikuwa amemteua kwa kusudi, lakini alijipata katika jangwa kwa miaka arobaini. Wakati huu, alipoteza kujihisi kwa ubinafsi na tumaini ya yale Mungu angefanya akimtumia. Alijua kuwa wakati alikuwa na kadi zote kwa upande wake, alikosea. Lakini Mungu alimjibu Musa akamwambia, "Bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe." (Kutoka 3:12). Kwangu mimi hili nila ajabu! "Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" (Warumi 8:31).

Ndipo Musa alimjibu akamwambia, “Lakini, tazama, hawataniamini, wala hawataisikia sauti yangu; maana watasema, Bwana hakukutokea.” (Kutoka 4:1). Kwa ufupi alikuwa akisema, “Bwana sijahitimu. Hawataniamini. Watasema, Mungu hajanena na wewe.” Na ndipo Mungu akamjibu Musa akamwambia, “Ni nini hiyo uliyonayo mkononi mwako?” Akasema, “Ni fimbo.” Mungu akamwambia, "Itupe chini.” Akaitupa, na kwa kupitia ishara mbalimbali, Bwana akamhakikishia kuwa atakuwa pamoja naye.

Katika mstari wa kumi wa sura ya nne, Musa akamwambia Bwana, “Ee Bwana, mimi si msemaji, tokea zamani, wala tokea hapo ulisema na mtumishi wako; maana mimi si mwepesi wa kusema, na ulimi wangu ni mzito.” Musa alilia, “Sina nguvu. Sio msemaji. Si mwepesi wa kusema na ulimi wangu ni msito.” Mungu akakataa na kusema, “Ni nani alikifanya kinywa cha mwanandamu? Ni nani aliyekupa uwezo wa kuongea au kuzungumza?” Mungu anaweza kushinda ulemevu wetu. Yeye ndiye aliyeumba kinywa chetu kwanza.

Na katika mstari wa kumi na tatu akasema, “Ee Bwana, nakuomba, tuma kwa mkono wake huyo utakayemtuma.” Kwa ufupi, “Bwana, tafuta mtu mwingine kwa kazi hiyo. Sina nia. Sitaki kufanya hiyo kazi.” Hapo ndipo Bwana alimkasirikia Musa na akaenenda kwa mpango wa pili. Alimtumia Haruni kusema badala ya Musa. Ni huzuni lakini mara nyingi tunakosa yaliyo mema ya Mungu na tunamfanya achague mpango wa mbadala wa pili.

Ninaamini katika mapenzi ya Mungu yaliyo elekezwa na mapenzi yaliyo huru. Naamini kuwa Mungu atatuinua juu kulingana na vile tunampa nafasi, na atafanya yaliyo mema kwetu katika kiwango hiki. Lakini pia naamini kuwa mara nyingi tunamlazimisha kuja chini kwa kiwango chetu badala ya sisi kuinuliwa kwa kiwango Chake. Tunamleta Mungu chini na mara nyingi tumshurutiza Mungu kwa kiwango chetu cha kuwajibika.

Tazama yale Mungu aliyapitia ilikumfikia Musa mtu ambaye hakujiamini, hakusadikika, hakuwa na uwezo, na hata hakutamani, lakini bado alikuwa amechaguliwa na Mungu kuwakomboa watu.

Katika kitabu cha Waamuzi, wana Waisiraeli walipotenda maovu mbele za Bwana na kuanza kuabudu miungu mingine, Mungu aliwatia mikononi mwa Midiani. Midiani walifunika nchi kama kabisa kama nzige. Walichukua mazao yao mara tu yalipokuwa tayari kuvunwa. Wana Waisiraeli wakaanza kumlilia Bwana kwa sababu ya utumwa na mateso. Basi Mungu akamtuma malaika wake kwa Gideoni ambaye alikuwa akipepeta ngano ndani ya shinikizo iliyomficha kuonekana na Wamidiani. Malaika wa Bwana akamwambia Gideoni, "Enenda kwa uwezo wako huu, ukawaokoe Israeli na mkono wa Midiani." (Waamuzi 6:14). Naye Gideoni akamjibu, "Ee Bwana nitawaokoa Israeli kwa jinsi gani? Tazama, jamaa zangu ndio walio maskini sana katika Manase, na mimi ndimi niliye mdogo katika nyumba ya baba yangu." (Waamuzi 6:15) "Bwana unaikuriza chini ya mkebe. Familia yangu ni maskini na mimi ndimi mdogo katika jamaa yangu."

Alifikiria kuwa yeye hawezi, lakini ukweli ni alikuwa aliye stahili, kwa sababu alikuwa mfano wa mtu ambaye Mungu alihitaji. Mungu alitaraji kumtumia mtu ambaye alijua kuwa hakuwa amehitimu au uwezo wa kulikomboa taifa, mtu ambaye alijua angemtumainia Bwana kwa jambo lolote kutendaka. Mungu pia alimleta Musa mahali hapa ili aweze kumtumia.

Wakati hatuna tumaini ndani ya nguvu zetu, tunajua ya kwamba ikiwa kazi yeyote itafanyika, mpaka Bwana ndiyeatakayeitenda. Wakati nilihisi mwito wa Mungu kwa huduma katika maisha yangu, nilienda katika chuo cha bibilia na nikajitayarisha. Nikiwa chuoni, nilikuwa Raisi Mkuu wa Darasa, Raisi wa Chama cha Wanafunzi, na nikatayarisha mpango wa wanariadha kwa shule. Kwa kweli, nilihisi kuwa nilikuwa na jambo la kuwapatia. Wakati nilianza katika huduma, nilijua kwa kweli nilikuwa na

ukamilifu na mwanzo mzuri wa kujenga kanisa ambalo litafahulu mahala popote.

Nilijiamini sana, ndipo Bwana aliniweka katika ala. Aliniruhusu kusumbuka miaka kumi na saba bila mafanikio. Nililazimika kufanya kazi isiyo ya kawaida ili niweze kimu jamii yangu na nikae katika huduma. Kama sio ule mwito wa Mungu katika maisha yangu ningekata tamaa. Kwa ukweli, mara kwa mara nilipanga kuachana na huduma, lakini Bwana alinirudisha. Haya yote yalitendeka kwa sababu nilitumainia uwezo wangu.

Bwana aliniruhusu kutumia miaka yangu ya kwanza nikishindwa, mpaka aliponiweka mahali ambapo sikuwa na lolote la kupeana. Na ndipo nilianza kumtegemea Roho na kumtumainia. Wakati huu ndio nilimwacha Mungu aifanye kazi kwa Roho Wake. Sikujaribiwa kuchukua utukufu/sifa kwa ile kazi Mungu alikuwa akitenda. Alinileta kwa msalaba na kunitoa ubinafsi wangu na tamaa zangu. Wakati Mungu alianza kutenda kazi kwa Roho wake, inafurahisha na ni jambo la kusisimua kutazama yale Mungu anaweza kutenda.

Mara nyingi kunahitajika huku kuondoa kwa ubinafsi. Wakati Gideoni alisema, “Ee, Bwana, tazama, jamaa zangu ndio walio maskini sana katika Manase, na mimi ndimi niliye mdogo katika nyumba ya baba yangu,” badala ya kujitoa nje, kwa kweli alikuwa akiwakifisha kwa Mungu kuwa amepata aina ya mtu aliyekuwa akimtafuta, yule ambaye hatajisifu au kujitukuza kwa ushindi, lakini angemtukuza Mungu.

Ni jambo la kustaajabu kuwa, Mungu alipomtumia Gideoni, na Wamidiani wakatawanyika na kushindwa, Waisraeli walikuja kwa Gideoni na kumwambia, “Tawala wewe juu yetu… Gideoni akawaambia, mimi sitatawala juu yenu wala mwanangu hatatawala juu yenu; yeye Bwana atatawala juu yenu.” (Wamuzi 8:22-23). Huu ndiye mtu ambaye Mungu alitazamia.

Nawatazama watu ambao Mungu aliwakusanya karibu na Daudi. Kila mmoja wao alikuwa na masikitiko, madeni na kuhangaika. Walikusanyika kwake na akawa kingozi wao. Walikuwa kundi wasio na nguvu na walioshindwa kama wanaume 400, lakini Mungu akawainua kuwa jeshi kuu.

Na pia natazama watu ambao Mungu amewaleta karibu nami na kujichekelea nikiwaona wale Mungu amewatumia. Wao nikama wale watu wa Daudi, wale wametupiliwa bali na jamii, na bado tazama yale Mungu ametenda.

Wakati Mungu alimwita Jeremia, alimjibu, "Aa Bwana Mungu! Tazama, siwezi kusema; maana mimi ni mtoto." (Yeremia 1:6). Wakati Yesu aliwaita wanafunzi wake, aliwachagua wavuvi na mtoza ushuru. Yeye hakuenda katika chuo kikuu cha Waebrania huko Yerusalemu na kusema, "Wewe Gamalieli, ni nani walio werevu na kukamilika sana hapa?" Alienda katika bahari ya Galilaya na akawaita hawa wavuvi.

Kwa Hivyo Calvary Chapel sio mara ya kwanza Mungu kuwatumia waliotupiliwa mbali na jamii kutenda kazi ya ajabu. Lakini inashangaza na mara nyingine huzunisha ya kwamba Mungu anapoanza kututumia, tunaanza kutafuta sababu ambazo Mungu anatutumia. Tunajaribu kuwa wakamilifu katika mwili.

Akiwaandikia Wakorintho Paulo alisema, "Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa." (1 Wakorintho 1:26). Alikuwa anawaita ili watazame ya kwamba Mungu hakuwaita watu wengi waliokamilika- sio wengi wenye hekima ya mwilini, sio wengi wenye nguvu, sio wengi wenye cheo. Anaendelea na kusema, "Bali Mungu aliyachangua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa,

naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko.” (1 Wakorintho 1:27-28).

Halafu anatupatia sababu katika 1 Wakorintho 1:29 “mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu." Umuhimu wa Mungu ni kuwachagua wale ambao kwa hakika hawafahi, alafu kuwapaka upako wa Roho wake. Baada ya, matokeo yakija, ni la ajabu na kushangaza kwa ulimwengu. Hapendi nguvu za mwili kutukuzwa mbele Yake.

Luka anatwambia katika sura ya kumi ya kwamba wanafunzi wake walirudi kwa kushangilia kwa kazi ya Mungu ndani ya maisha yao. Wakati ule ule, walipokuwa wakizungumza kuhusu hayo, Yesu alikuwa akishangilia katika Roho Wake. Na akasema, “Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya umewaficha wenye hekima na akili; umewafunulia watoto wachanga; Naam, Baba, kwa ndivyo ilivyokupendeza.” (Luka 10:21). Yesu alikuwa akimshukuru Baba ya kwamba alificha mambo kwa wenye hekima na akili na kuwafunulia watu wa kawaida wasio na hekima, kwa sababu ilimfurahisha machoni Mwake.

Ninashangaa kuwa tunapoanzia katika Roho, wakati mwingi tunajaribu kukamilika katika nguvu za mwili. Wengine wa wachungaji wa Calvary Chapel wamerudi shule. Shule nyingi zilikuwa na hamu yao kwa sababu ya kunawiri kwao katika huduma. Walitaka kuwaonyesha kuwa walihitimu kutoka kwao, na kuwaambatanisha na kunawiri kwao katika huduma. Shule nyingi zilitamani kuwapata, ndipo wakawapa daraja spesheli kimasomo kwa ajili ya tajriba ya maisha yao.

Waliweza kusoma mafulizo kidogo wa masomo, na pamoja mambo ambayo walipitia wakapata shahada. Na sasa shule zao, huwatumia kama mfano maalumu wa kunawiri kwa wanafunzi wao. Wengine walirudi shule kupata hizo digrii kwa sababu wakati wa dodosa, watakuuliza, “Una digrii yeyote?” na ni kama jambo la kuaibisha kusema, “Kwa kweli, sina digrii yeyote.”

“Ulienda seminari gani?”

“Sikuenda seminari.”

“Ulienda chuo kikuu gani?”

“Naam, kwa kweli sikuweza hata kupata hati ya sifa (diploma) ya shule ya upili.”

Inaweza kuwa jambo la kuaibisha kukubali kuwa hauna elimu yeyote. Wakati “Nani ndiye nani” yule atakuandikia na kusema kuwa umechaguliwa kuwa katika toleo la mwaka huu, wanataka kujua una digrii ngapi na ulienda chuo gani kwa sababu mtu anataka aweze kusema, “Sawa, tazama huyu mtu ana shahada ya uzamifu (Ph.D.).” Kwa namna moja tunahisi kuwa tunaweza kuwakifisha na hata kuwa tayari katika mwili. Tulianza kwa Roho na njia pekee ya kuendelea kufaulu ni kuendelea katika Roho.

Katika Mathayo 11:25, “Wakati ule Yesu akajibu akasema, Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga.” Ni jambo la kushangaza vile tunavyojitenga na Ufunuo wa ukweli wa Mungu kwa kuwa na hekima na akili. Yesu alikuwa akifurahia kuwa baba yake hakuufumbua ukweli kwa wenye hekima na akili, bali kwa watoto ili utukufu/sifa umwendee Mungu.

Wakati Gideoni alikuwa tayari kwenda kupigana na Wamidiani, alikuwa ameshindwa zaidi kwa nambari ya watu. Wamidiani walikuwa 135,000, naye alikuwa tu na 32,000 waliosikia mwito wa kwanza. (Waamuzi 7:2). Lakini Mungu akasema, “Watu hawa walio pamoja nawe ni wengi mno hata nikawatie Wamidiani katika mikono yao, wasije Israeli wakajivuna juu yangu wakisema, Mkono wangu mwenyewe ndio ulioniokoa.” (Waamuzi 7:2). Bwana alikuwa anasema ya kwamba hawezi kutenda na 32,000. Mungu anataka kufanya kazi, lakini Yeye mwenyewe

anataka utukufu/sifa wa kazi anayoifanya. Hii ndiyo maana anatumia vitu vidogo vya humu duniani iliawaibishe wenye hekima. Watu wanaweza tu kutazama, watingishe kichwa na kusema, “Sielewi na hili, lakini upako wa Mungu uko pale. Kwa kweli Mungu anawatumia.” Nashangaa ni mara ngapi ile kazi Mungu anataka kufanya inapingwa kwa sababu Mungu hapati watu wa kawaida wa kutumia. Wengi wa wale akonao ni wale wenye shahada za uzamifu (Ph.D.).

Sasa, nimelaumiwa kama aliye kinyume na masomo. Hata Calvary Chapel mara nyingi huitwa wasio soma au waliokinyume cha masomo. Pengine nimekosea, lakini siombi msamaha. Ninaamini katika elimu. Maisha yangu mwenyewe yalikuwa ni maisha ya kusoma. Bibilia inatwambia “Jitahidi kujionyesha kuwa umekubalika na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la ukweli.” (2 Timotheo 2:15). Naamini Mungu hutumia vyombo binadamu, na anatayarisha vyombo ambavyo hutumia. Naamini ni ya muhimu kutayarishwa kwa Neno la Mungu, lakini sikutokana na msimamo wa kibinadamu. Elimu ya kweli haitokani na hekima ya dunia, lakini kwa kuelekezwa na hekima itokayo kwa Roho Mtakatifu.

Wakati wanafunzi walisimama mbele ya kamati ya dini, kamati ilistaajabu katika kuelewa kwao na Bibilia. Lakini wakatambua kuwa walikuwa na Yesu. Vile vile, tukikaa na Yesu kwa Neno lake, tutapata yote tunayohitaji kwa ibada na huduma. Hauhitaji miaka nne ya shahada ya uzamifu (Ph.D.). Mara nyingi zinaweza kuwa kizuizi kuliko baraka. Naamini kuwa anwani ‘Daktari’ inaweka ukuta katikati yako na watu, ambao huzuia huduma kwao. Watu watakukatalia katika fikira wanaposema ‘Daktari.’ Unajiweka katika sehemu ya juu na wao wahisi kuwa duni. Na mwishowe hauwezi kuwahudumia kwa kiwango ambacho wanaweza kujitambulisha nayo.

Kila mwaka tunakutana kupanga Mpangilio wa Warsha ya Wachungaji ya kila mwaka. Ninakutana pamoja na Raul Ries, Mike

MacIntosh, Greg Laurie, Skip Heitzig na wengine wengi. Wakati ule tulikuwa na mkutano baada ya Raul na Mike kupata digrii ya udaktari, kila mmoja alikuwa analeta mzaha kuhusu anwani yao. 'Dkt. Raul Ries na Dkt. Mike MacIntosh.' Tulikuwa tukiwapa wakati mgumu na ndipo mmoja wao akasema, "Kweli, kama nanyi mngeenda shule na kupata masomo ya kutosha, mnaweza kupunguza ukubwa wa makanisa yenu kwa kipimo ambacho unaweza kuongoza."

Nilifikiria kuwa hayo yalikuwa mazuri sana. Kwa sababu ulianza kwa Roho, kama ukijaribu kuwakifisha kwa nguvu za mwili, utapiga tu kazi ambayo Mungu ametenda na anataka kutenda. Njia iliyopo ya kuendelea ni kuenda katika Roho. Kama tulianzia katika Roho, na tuendelee katika Roho! Shukuru Mungu licha ya hiyo ya kwamba Raul bado ni Raul na Mike bado ni Mike, watu ambao wanajua kutoweza kwao na ukosefu wao, watu ambao wana mtumainia Roho kwa yote.

Mungu alimwambia Yeremia, "Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua." (Yeremia 9:23-24). Hili ndilo jambo la muhimu ya kuwa unamfahamu na kumjua Mungu. "Mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana." (Yeremia 9:24).

Hiyo ndio sababu Mungu anawachagua wale wasiohitimu kabisa kama sisi, anatujaza kwa Roho wake, na halafu anafanya kazi ya ajabu kupitia kwetu, ambayo inashtua na kushangaza ulimwengu. Sasa, tunawezaje kuwa wajinga na kujaribu kutafuta sababu ya kuelezea ni jinsi gani Mungu alitutumia, ili tujisifu wenyewe badala ya kumtukuza Mungu na yale ametenda?

Paulo akiwaandikia Wakorintho alisema, "Maana ni nani anayeku-pambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea? Lakini iwapo

ulipokea, wajisifia nini kama kwamba hukupokea?" (1 Wakorintho 4:7) Sasa ni nini ulicho nacho zaidi ya mwingine? Chochote ulicho nacho umepokea kama zawadi kutoka kwa Mungu. Na Kama umekipokea, kwa nini ujitukuze kama hukupokea, kana kwamba wewe ni kitu cha maana?

# 10

## UWEZO WA JUU WA UPENDO

*"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." (Yohana 13:35)*

Bila upendo vipawa vyote na nguvu zote za Roho Mtakatifu ni bure na isiyo na thamani yoyote. "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao." (1 Wakorintho 13:1). Paulo anasema kuwa kuna wale wanaweka bidii katika kunena kwa lugha nyingine, na wanatazamia kama karama hii ndio msingi wa kwanza wakudhihirisha kujawa na Roho au ubatizo wa Roho. Lakini watu hawa wakiwa hawana upendo, kunena na ndimi/kwa lugha nyingine hamna maana kuliko kelele tu ambayo hutokana na shaba. Ni kelele tu. Sio jambo la ushahidi au dhibitisho. Inaweza chukuliwa kama msingi wa kudhibitisha uwepo wa Roho, lakini haina dhibitisho la kitu chochote kama hakuna upendo. Ni sawa na shaba iliyo na upatu uvumao ni kelele tu wala sio ushahidi kwa lolote lile.

Nyingi za kanuni za dini na usahihi na kuelewa na Bibilia hazina maana kama hakuna upendo. Hata nikielewa na mafumbo makuu, kama vile fumbo la Utatu wa Kiungu yaani (Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu), au Ukuu wa Mungu, au wajibu wa mwanadamu, kama sina upendo, zote ni bure. Na kama ninajileta mbele ya nyuso za watu na kufanya kazi ili waone na waamini upande wangu, kanuni zangu za usafi/utauwa hazinisaidii kwa lolote lile. Yote ni bure bila upendo.

Nimekuja kuafikia ukingo ya kwamba ni vizuri kuwa na nia nzuri kuliko kuwa na jibu nzuri. Kama maajibu yangu ni mabaya, Mungu anaweza kuyageuza kwa Ufunuo wa ukweli wake. Lakini mara nyingi

inachukua maisha yote kubadilisha nia/dhana. Ni vizuri tukiwa na nia/dhana nzuri na jawabu mbaya, badala ya jawabu nzuri na nia/dhana mbaya. Kumbuka hayo wakati ule utajipata ukibishana juu ya msimamo fulani wa kanuni za dini au jambo fulani.

Mapenzi ya Mungu juu yetu ni tutambue upendo wake na tushiriki upendo ule na wengine. Yesu alisema, "Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo." (Yohana 13:34). Hii ni amri kubwa. Na pia akasema, "Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake." (Yohana 14:21). Yohana alisema, "Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona?" (1 Yohana 4:20). Na anauliza, "Je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?" (1 Yohana 3:17).

Yohana amenena sana kuhusu kuweka amri za Mungu katika waraka wa kwanza. Lakini ni amri gani ambayo tumesikia kwake? Ni kuwa lazima tupendane mmoja kwa mwingine.

Kama tukihudumia ushirika na kundi au ni somo la nyumba la Bibilia au kwa kanisa la watu elfu kumi, lazima tujieleze wazi kuwa lengo letu kuu ni upendo. Upendo huu lazima udhihirishwe katika matendo yetu, nia na hata kwa maisha yetu. Ni heri kila mmoja akaona upendo wa Kristo ukidhihirika maishani mwetu. Kama vile Paulo alipomwambia Timotheo, "Bali uwe kielezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi." (1 Timotheo 4:12). Kila wakati tafuta nafasi ya kuelewa na kuonyesha huruma, kuwaona watu kupitia huruma wa Yesu Kristo.

Nimetambua kuwa ufunguo wa huruma, ni kufahamu au kuelewa. Ezekieli alisema, "Nilikaa huko waliokuwa wakikaa." (Ezekieli 3:15).

Naamini kuwa hii ni jambo la muhimu kujaribu kufanya, hata kwa fikira zako. Jiweke katika maisha anayopitia. Kaa mahali alipokaa. Tazama kwa upande wake. Wakati mwingi tunatazama jambo kutoka kwa upande wetu, lakini jaribu kutazama kutoka kwa upande wake.

Wakati mwingine kuna watu wanatukasirisha kwa tabia zao au kwa sababu ya tabia fulani ambazo tunazichukia. Nilimsikia Dkt. James Dobson akisema kulikuwa na mtu katika shule ambaye alimchukia sana, na huyu jamaa pia alimchukia. Maisha yao shuleni hawakushiriki kwa lolote lile. Baadaye, Dkt. Dobson alikutana na yule mtu mahala pa kutubu, na alijua ya kwamba mpaka atakutana naye uso kwa uso. Ndipo akaandika mambo ambayo hayakumpendeza na ndio sababu alimchukia. Alipokutana na yule mtu akamwambia, “Wajua lazima nitubu kwako kwa kuwa katika maisha yetu shuleni, nilikuchukia na hizi ndizo sababu.” Dkt. Dobson akaanza kusoma sababu zote kwa nini alimchukia huyu mtu. Halafu yule jamaa akajibu na kusema, “Naam, nilikuchukia pia wewe, na kwa sababu zile zile ulinichukia.” Dkt. Dobson alisema kuwa alizitazama zile sababu na kugundua ya kwamba alikuwa anajitazama kwa kioo. Naona hii ikiwa ya kweli kabisa na ya kuchekesha vilevile.

Zile tabia ambazo hatupendi juu yetu, ndizo zenye tunachukia katika wengine. Tumevumiliana na tunaishi nazo, lakini wakati tunazitazama kwa wengine, hatuwezi kuzivumilia. Zinatuudhi na kutukasirisha. Kuelewa ni jambo la muhimu sana ya huruma.

Kwa miaka ningetumia likizo zangu nikiongoza kambi ya vijana. Ni jambo napendelea sana maishani. Jamii yangu ingekuja pia, na wangekuwa na nafasi ya kufurahia pande nyingine za nchi. Bibi yangu Kay alikuwa akisema, “Lakini mpenzi haukupata likizo.” Naningemjibu, “Aa, mimi nilipata.”

Sasa ukiongoza kambi za vijana, kuna wale wanakasirisha ukiwaambia, “Kaa chini,” nao watasimama. Ukisema, “Simama”, nao

watasalia wameketi. Ukisema, “Sasa haturushi mawe kwa miti. Inaweza kwaruza gome na mende wataingia kwa hivyo haturushi mawe kwa miti,” kwa kweli utawapata wale wale wakirusha mawe kwa miti. Kila wakati wanaasi. Kuna washauri ambao wamekuja kwangu na kusema, “Chuck, ni vizuri umepeleke mtoto huyu kwa mshauri mwingine kwa sababu sitawajibika kwa lile nitakalo mtendea. Nitamuua siwezi kumvumilia.”

Ndipo ningesema, “Mtume kwangu.” Kwa kweli wangeshika huyo mtoto kwa shingo na kumleta kwangu na kusema, “Huyu ndiye nilikuwa nakueleza.” Ningemkalisha chini na kumpa tabasamu, na kusema, “Unataka kunywa kinywaji gani?” Ningeenda kwa duka na kumnunulia kinywaji alichopenda pamoja na peremende aliyoipenda sana. Wakati amekaa pale amejawa na uasi akifikiri hataniambia jambo lolote. Kwa hivyo naanza kuvunja kizuizi/kinga chake. Ni jambo la ajabu vile soda na peremende ndani yake zitavunja kinga yake. Ninaanza kuvunja ule ukuta amejenga halafu naanza kuonyesha shauku au mapendeleo kwake. Mazungumzo yaliendelea hivi.

“Naam, umetoka wapi?”

“Black Canyon.”

“Black Canyon iko wapi? Ni karibu na mto Verde?”

“Ndio.”

“Vizuri. Je, Unasoma?”

“Ndio.”

“Naam, nieleze kwa ufupi kuhusu jamii yenu. Baba yako yuko wapi?”

“Sina baba.”

“Aa, nini lilifanyika na baba.”

“Sijui, sijawahi kuwa na baba.”

“Mmm, na hilo ningumu.”

Ukiendelea na mazungumzo utapata kujua kuwa, mama yake anafanya kazi ya baa na anakuwa na mwanaume tofauti kila usiku. Na mtoto ule ameachwa pekee yake. Na wale wanaume wanaokuja nyumbani hawana huo urafiki, na ndio amezoea kukaa hivyo. Naye mama yake hashughuliki naye. Hadithi inapoanza, moyo wako unavutiwa na huruma. Mtoto huyu masikini hana nafasi. Amejaza hasira zote na chuki dhidi ya dunia hii ambayo anatakiwa aishi. Anajua kujenga hizi ukuta. Haruhusu mtu yeyote amkaribie. Mpaka ajikinge mwenyewe. Ni yeye pekee anajitunza. Sasa umeelewa. Sasa umegundua chanzo cha kutenda na kurejeana kwake.

Ndipo ningemrudia mshauri, nakaa pamoja naye, na ninashirikiana naye kinachoendelea katikamaisha ya huyu mtoto. Nilitaka kumpatia mshauri kuelewa ndipo aweze kuonyesha huruma. Ningemhimiza huyo mshauri kuwa msaidizi wake na amweke kijana karibu naye, kumpa wajibu fulani na kutengeza uhusiano kwa mara nyingi pamoja na usaidizi. Ni jambo la kushangaza mabadiliko yanayoweza kukuzwa kwa muda wa wiki moja kwa huruma.

Kama mchungaji, utakuwa na watu katika kutano wako ambao utahisi vile vile juu yao. Ungependa kuwaua. Lakini unatakiwa uwe na kuelewa. Pata kuelewa ni wapi mwiba uko na nini kinawaudhi. Ukitafuta kuwaelewa, halafu uwe na huruma, kwa kweli unaweza kuwahudumia. Huwezi kumuhudumia vizuri mtu yeyote ambaye haumuhurumii. Mara ngapi tunasoma kwa maandiko, “Yesu akavutwa na huruma.” Wakati aliona mahitaji ya watu? Alielewa na mahitaji haya. Hakuhitaji mtu amweleze kwa sababu alijua ni nini ilikuwa ndani ya mwanadamu. Ni kwa sababu alikuwa na huruma. Kwa hivyo tafuta kuelewa.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake, “Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa;” (Yohana 15:16). Tunda la Roho ni upendo. Amekuchagua wewe ukazae hili tunda. Katika Yohana 13:34, baada ya kuwaambia wanafunzi wapendane kama vile alivyotupenda, anaendelea na kusema, “Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu. Kama vile Baba alivyonipenda, nami nilivyowapenda ninyi kaeni katika pendo langu.” (Yohana 15:8-9). Kwa hivyo tunaweza kuona kipeo cha nguvu ya upendo.

# 11

# KUSAWAZISHA

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli." (2 Timotheo 2:15)*

Jambo lingine ambalo linatofautisha Ushirika wa Calvary Chapel ni matumaini yetu ya kutogawanya watu wa Mungu juu ya mambo ambayo sio muhimu. Hii si kusema hatuja sadikika. Wakati Bibilia inanena wazi wazi, nasi pia tunanena wazi wazi. Lakini kwa mambo mengine tunatazama pande zote mbili za mjadala. Tukitazama tusitengane au kupendelea wenye upande mmoja kuliko mwingine.

Mfano wa kujumuisha waonekana katika kujachilia swala kuhusu huduma ya Roho Mtakatifu. Hatuchukui mtazamo wa Kipentekosti wala hatuchukui mtazamo wa Kibaptisti. Wakati unapochukua mtazamo upande mmoja, unapoteza nusu ya wafuasi. Kwa nini uwapoteze nusu ya wafuasi wako? Tamanio letu ni kuweza kuwahudumia wafuasi wengi kama iwezekanavyo. Wakati tunaanza kuchukua msimamo mkali juu ya mambo ambayo si ya kimsingi kwa wokovu wetu, tunatenga sehemu ya watu. Katika kanuni muhimu za imani, ni lazima tuchukue msimamo kamili. Lakini kwa mambo ambayo yasio muhimu, tunakubali kuwa watu wanaweza kuwa na mitazamo tofauti, na tunakubali haya katika Roho wa neema ni muhimu kutambua kuwa tunaweza kukubaliana na kutokubaliana bado tukae katika Roho wa umoja na upendo.

Tunaamini katika uhalali wa karama za Roho, na karama hizi zaweza kutumika leo. Lakini hatuamini kupitisha kiasi yanayoandamana na uhuru

wa kutumia karama hizi za Roho Mtakatifu. Kwa hivyo tunaepuka malumbano au mabishano.

Kama watu wanataka kuzungumza kwa lugha nyingine, tunawatia moyo kufanya hivyo kibinafsi iliwasaidike kunena upendo wao, na sifa zao na maombi yao kwa Mungu. Tunatazama I Wakorintho 14 kama mfano wetu wa Bibilia. Hatuwekei sheria kuwa mtu akinenea kwa lugha kama msingi wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunaamini kuwa kuna shahidi za namna nyingi ambazo ni muhimu kuliko kunena kwa lugha. Kama vile Paulo alisema, “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao.” (1 Wakorintho 13:1). Hatusisitizi kuongea na lugha kama msingi wa kwanza wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, lakini tunatazama msingi upendo kama tunda la Roho. Naamini kuwa tunaweza kusimama kwa mwamba imara wa Maandiko tukifanya hivyo, na wakati huo huo, kuwahimiza watu kupokea vipawa vya lugha.

Kama vile Paulo alivyoeleza, unaweza ukaitumia kwa maisha yako ya maombi na kwa maisha yako ya kuabudu, ukimwimbia Bwana. “Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda. Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia; Kwa maana wewe ukibariki kwa roho, yeye aketiye katika mahali pa mjinga ataitikaje, Amina, baada ya kushukuru kwako, akiwa hayajui usemayo?” (1 Wakorintho 14:14-16). Kama uko katika hadhara ambao hamna mkarimu, na mna mtu anayenena kwa lugha, inawezekanaje mtu anayeketi katika kiti ambaye hajui lugha kuelewa? Unaweza kuwa unamshukuru Mungu, lakini watu wengine hawajengwa. Tunastahili kufanya mambo kwa adabu na mpangilio. Katika sehemu hii, hatukubaliki na Wapentekosti, wala kwa Waaminio karama za Roho hazipo leo wenye kukataa udhihirisho wowote wa karama Roho Mtakatifu leo.

Mfano mwingine wa kusawazisha mambo yenye mashaka ni mtazamo wetu kwa Calvinism. Hio ndio sehemu ambayo watu wanaingiza hisia sana. Sisi sio “Five Point Calvinists” (waCalvinisti wa vipengelee 5) wala sio Arminiani. Tunaamini katika kuhifadhiwa kwa walioamini. Hatuamini kuwa unaweza kupoteza wokovu kwa sababu ulikasirika au ulidanganya, na kwa hivyo unatakiwa uende mbele Jumapili ifuatayo utubu halafu uokoke.

Tunaamini katika kuhifadhiwa kwa walioamini, lakini pia tunaamini katika ‘uvumilivu wa wateule.’ Hatuamini hivyo kwa sababu kama wewe ni mtume utavumilia, lakini unahitajika kuvumilia kwa kuwa wewe ni mtume. Yesu alisema, “Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli;” (Yohana 8:31), na “Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea. Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.” (Yohana 15:6-7). Yesu mwenyewe ndiye aliyeleta uwezekano wa mtu kutokaa ndani yake. Kwa hivyo tunatafuta sehemu iliyosawazika badala ya kukaa upande mmoja na kuzifinya “Five points of Calvinism.” Unapoichukua msimamo mkali katika mambo hayo yasiona msingi, utafanya watu walio na mafunzo awali ya Methodist, Nazarene, na Arminian kuacha kanisa lako. Kwa nini ufanye hivyo?

Uhifadhi wa milele wa waaminio ni jambo la kujadiliwa kwa lolote lile. Kuna maandiko zinazoaminiwa na pande zote mbili. Kuna Yohana 3:16. Na hii “Yeyote aaminiye” inamaanisha nini? Hii inamaanisha kuwa kila mtu anaweza kuokolewa? Kwangu inakaa kumaanisha hivyo, kwa hivyo hatuchukui msimamo mkali wa Ucalvinisti kuwa upatanishi wa Yesu una kipimo na kwa kuwa Yesu hakufilia kila mtu, bali wale watakaomwamini. Hatukubali kuwa kumwamini Yesu hakuna jukumu la mwanadamu, lakini ni kutokana na mapenzi makuu ya Mungu. Huu msimamo unasema kuwa Mungu amewateua wengine waokoke na wengine wapotee. Kama Mungu

amekuteuwa upotee, bahati ngumu, ndugu. Hakuna lolote ambalo tunaweza fanya. Huku ni kukataa kwamba binadamu ana uwezo wa kuchagua. Badala yake, tunaamini kuwa Mungu ametupa uwezo wa kuchagua. Sababu alitupa uwezo wa kuchagua ndipo upendo tunaodhihirisha kwake uwe wa maana na wa kweli. Hii ndio nafasi ya kusawazisha msimamo ambayo tunachukua.

Kuna watu ambao kila wakati wanataka kuweka Calvary Chapel pembeni. Unaamini katika usalama wa milele? Nami nasema, "Ndio, kwa kawaida naamini katika Usalama wa milele. Ijapo nitadumu katika Kristo, niko na usalama milele." Sasa jadiliana na hiyo. Kama hautadumu katika Kristo, uko salama? Unaweza kuwa na usalama nje ya Yesu Kristo? Sijui ya usalama wowote nje ya Yesu Kristo. Lakini naamini kuwa ninapodumu ndani ya Yesu, ananiweka kutokuanguka, ananileta mbele ya Utukufu wake kama mwenye asiye na kosa na furaha kuu. Na hakuna mtu yeyote anayeweza kunitoa mikononi mwake. Naamini hayo na ninashiriki usalama wa Mungu.

Mara kwa mara mambo hayo yanajitokeza kama elimu ya maana. Watu wanatofautiana katika tafsiri ya maneno machache. Tulikuwa na mfanyi kazi huku Calvary ambaye alijipeana kwa makundi ya usaidizi. Wakati tulipokuwa naye aliwaleta wengi katika imani ya Kristo. Kwa bahati mbaya, tulitengana iliyomwacha akiwa na hasira nyingi mpaka ikamleta kujiunga na kundi la kanuni kali lisilo na jina ambacho kinawahimiza watu waachane na imani ya Kristo iliyo katika Bibilia.

Je, ameokoka? Kwa ukweli, yeye ni adui wa Kristo. Kama mimi ni wa Arminian, ningesema amerudi nyuma. Kama mimi nilikuwa nikiongea kutoka upande wa Ucalvinisti, ningesema hakuwa ameokolewa. Sasa, sote tunazungumzia kuhusu mtu mmoja, lakini njia ambazo tunamweleza yeye huleta utengano.

Tunatambua ukweli huu. Huyu mtu amemkataa Yesu. Hiyo ni wazi. Amerudi nyuma, au alikuwa kweli ameokoka? Shida ni kuwa, nikisema hakuwa ameokoka, sasa usalama wangu uko wapi? Najuaje kwamba nimeokoka? Yeye alikuwa na alama za wokovu. Alikuwa na nia ya kumtumikia Bwana. Alikuwa akitafuta kuwaleta wengine kwa Yesu Kristo. Ninania ya kumtumikia Bwana na nia ya kuleta wengine kwa Yesu Kristo. Labda sijaokoka. Sasa, huo si usalama kwangu.

Sasa, unaona, ni ile elimu ya jinsi maneno inavyokua. Tunawezaje eleza yale tunaona juu ya mtu na ushirika wake na Mungu? Mgawanyiko huu ni kama namwelezea kama aliyerudi nyuma, ama ninasema hakuwa ameokoka. Tukitofuatiana wazi tunaleta mtengano. Tunafukuza nusu ya watu nje ya kanisa kwa sababu nitasema amerudi nyuma na mwingine atasema hakuwa ameokoka. Tukiruhusu huyu mjadala tunagawa kanisa.

Hii ndio maana sishikilii kanuni juu hii kwa sababu naamini kuwa Bibilia inafunza juu ya mamlaka ya Mungu na wajibu wa binadamu. Ukichukua mmoja wapo ya upande kupita kiasi, ukikataa moja utajipata kwa shida sababu Bibilia yafunza yote mawili. Lakini waweza kuuliza, “Wawezaje kuwapatanisha?” Mimi siwezi. Na si lazima. Mungu hakuniuliza niwapatanishe. Mungu aliniuliza niamini. Nikikutana na mtu anayeishi katika zini, katika uzinzi, ama akienenda katika mwili na ansema, “Usistaajabu sababu yangu! Nilimkubali Yesu katika mkutano wa Injili wa Billy Graham nilipokuwa mtoto.” Na bado yeye ni mzinzi na mlevi. Lakini anasema, “Nilipookoka ninaishi nimeokoka! Kwa hivyo usistaajabu juu yangu.” Niamini, ninaposema nitajaribu kumleta kwa ukweli kwa uwezo niwezavyo. Nitampeleka katika Wagalatia 5 mahali ambapo Bibilia inaongea juu ya matendo ya mwili. Ikimalizia Bibilia inasema, “Kama nilivyokwisha kuwaambia ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.” (Wagalatia 5:21). Nitampeleka katika Wakorintho pamoja na Waefeso. Nitamwonyesha mahala wale wanaishi

kwa mwili na wamejipeana kuishi kulingana na nia za kimwili, hawataurithi ufalme wa Mungu.

Bado kwa njia nyingine, kama ninanenea kwa mitume na nia iliyopita kiasi, kila wakati wakikosea na kutenda jambo mbaya, wanahisi kwamba wamepoteza wokovu wao. Nitawapeleka kwa Maandiko yanayo tuhakikishia upendo wa Mungu. Nitawaonyesha vile Kristo anawashikilia na hakuna mtu yeyote anayeweza kuwatoa kutoka kwa mkono wa Baba. Nitawaelekeza kwa vifungu ambavyo vitawapa matumaini.

Msimamo ninaochukua kuhusu suala fulani, unategemea jinsi mtu ninaye nena naye alivyo. Naweza simamia upande wowote na nijadili hadi mwisho. Naweza nikachunguza maandishi kwa watu waliokatika pande zote mbili. Ninaweza kukuruhusu uchangue ule upande unaotaka, na mimi nitachukue ule mwingine. Ninaweza dondoa Maandiko mengi na nilete mjadala mzuri kama wewe.

Ukweli kuwa hili ni swala lenye utata, inadhihirisha kuwa kuna pande mbili. Kama kutakuwa na somo barabara, pengine hakungekuwa na utata. Kama hatungekuwa na Maandiko yasemayo, “Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye na ayatwae maji ya uzima bure,” (Ufunuo 22:17), basi hakungekuwa na utata. Lakini ukweli ni kwamba kuna funzo la uchaguzi ambalo tumepewa na Mungu. Anatayarajia kila mmoja wetu achague. “Chagueni hivi leo mtakayemtumikia,” (Yoshua 24:15). “Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, haya mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya mfuateni yeye.” (1 Wafalme 18:21). Lakini bado Yesu aliwaambia wanafunzi wake, “Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mmwombayo Baba kwa Jina langu awapeni.” (Yohana 15:16). Kuna sehemu mbili za swali hili, na ni muhimu tusipatwe katika msimamo wa upande mmoja tukiuacha upande mwingine maana kufanya hivyo kutagawanya mkusanyiko wako.

Mimi kama vile wanafunzi wengine katika chuo cha Bibilia, walisumbuka na jambo hili. Nilikuwa ninasoma kitabu cha Arthur W. Pink, kiitwacho The Sovereignty of God (Ukuu wa Mungu). Nilichanganyikiwa sana maana Pink alisema kuwa mwanadamu hana uchaguzi katika swala la wakovu. Ni vile Mungu ataamua Hakuna jukumu la binadamu. Nilipokuwa nikisoma hicho kitabu nilichanganyikiwa sana. Nilisimama, nikachukuwa makaratasi yangu, na kuyatupa chini. Nilimwambia Mungu, "Mungu, sielewi na hili." Nilikuwa nimevunjika moyo. Ndipo Bwana akaninenea kwa moyoni mwangu na akasema, "Sikukuuliza uyaelewe haya, nilikuliza uamini Neno langu."

Nilipumzika toka wakati ule kuendelea mbele. Bado katika fikira zangu siwezi kirazini au kuyaleta pamoja mambo haya mawili. Siwezi kuyaleta yote mawili pamoja, na hii shida tunayo kuwa hayo mara nyingi. Nikama chuma za reli. Chuma hizi mbili zinaenda sambamba na zikishikana uko taabani. Ndio na yaamini yote mawili, hata ingawa siwezi kuyaleta pamoja katika fikira zangu. Ninatosheka na kuyaamini bila kuyakata kwa kiwango kidogo cha hekima yangu.

Kujaribu kuleta Mungu katika akili yangu ni somo nzuri ya kuchanganyikiwa. Jaribu kuelewa na maisha ya milele! Jaribu kuelewa na maisha yasiyo na mwisho! Na maisha ya milele jambo kuelewa na pasipo mwisho! Jaribu kufikiwa mahala ukingo wa mbingu uko! Utaenda bali kiwango gani kabla upate kibao kinachosema, "Mwisho uliokufa. Hakuna kutokea! hakuna kitu mbele ya hapa"? Tunatakiwa kutambua kuwa Mungu ni mkuu kuliko kile tunaloweza tafakari au elewa kwa fikira zetu. Alisema, "Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu." (Isaiya 55:8-9). Sasa kama Mungu amesema kuwa Njia zake zi juu kuliko uwezo wetu basi ni kazi bure kujaribu kuelewa ziko juu ya kulewa.

Tunatakiwa kukubali ukuu wa Mungu usio na kipimo. Nikifikia mahali hapa pa utata, mahali ambapo hekima yangu inagonga mwisho, ninasimama pale na kumwabudu Mungu aliye Mkuu na kwamba siwezi kumpunguza kwa hekima yangu.

Uanzapo kuhudumu, uendeleapo kulisoma neno, utakuja kupata haya Maandiko ambayo yanazungumza juu ya ukuu wa Mungu. Unapopata haya Maandiko, funza. Ukifikia Maandiko yanayofunza juu ya wajibu wa binadamu, kweli funza. Kwa njia hii, una uhakika kuwa watu wanapata mlo uliosawazishwa ki roho.

# 12

## SAFARI ZA IMANI

*“Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa kwa thawabu wale wamtafutao.”* (Waebrania 11:6)

Ni jambo la kufurahisha kila wakati kumpa Mungu nafasi kufanya kazi yake. Yeye hutaka uwe sehemu ya kazi yake. Mungu huwa haachi kufanya kazi yake, kwa hivyo ni muhimu kwetu kutambua kile Mungu anataka kufanya. Nimegundua kwamba njia ya kuwezeshwa kutambua kile Mungu anataka kufanya ni tunapotembea katika imani. Tunahitaji kujitokeza ili tuone kile Mungu anaweza kukifanya. Lakini tunapoenenda katika imani, ni lazima tujihadhari na mtego wa kudhania tu. Watu wengi wanaojaribu kutega Mungu ili waone anaweza kufanya nini, hufanya kosa kubwa kwa kwenda nyuma na kutegemea juhudi za mwanadamu ambako hakuna mkono wa Mungu. Wakati mwingine hushusha hadhi zetu. kisha tunatumia nguvu za ziada na jitihada katika mpango ambao kwa hakika sio za Mungu.

Nimechukua mwelekeo huu mara nyingi na kugundua kwamba Mungu hayumo ndani. Nini utafanya sasa? Unaacha na kujiepusha. Kinalotuweka katika shida ni wakati kwa maringo/kiburi tunaposema, “Tutalifanya hili jambo lifaulu.” Tunajipata tukitumia nguvu zetu zote kutengeza kitu ambacho Mungu si mshirika na hili linaweza kukudhuru. Wakati najitokeza katika imani, likifaulu, ninafurahia na kusema, “Vizuri! Bwana aliniongoza.” Lisipofaulu, narudi nyuma na kusema, “Nilifikiria kuwa lilikuwa wazo nzuri, lakini lilianguka.” Ndipo, nikafikiria kuwa kuna tahadhari fulani katika safari ya imani.

Katika Agano la Kale, tuna hadithi ya Sauli. Wakati wa uongozi wake aliweka jeshi dhabiti. Akawa amri mkuu kwa walio wengi, naye Yonathani akawa amiri kwa walio wachache. Halikuwa jeshi kubwa, lakini Wafilisti waliokuwa wamewavamia na walikuwa na mpango wa kuwamaliza Waisiraeli. Walikuwa wamekusanya kundi kuu la wanajeshi pamoja na farasi. Walikuwa wakiogopwa na Waisiraeli hivi kwamba wengi wa jeshi la Waisraeli wakatoroka kufuka mto wa Yordani. Kulikuwa na wachache tu walikuwa wanaujasiri na waliokuwa hawaogopi. Ndipo Yonathani aliamka siku moja na fikira ambayo ilikuwa ya kusumbua, au kufurahisha. Kama Mungu anataka kupeana Wafilisti kwa Waisiraeli, hahitaji jeshi lote. Kama Mungu anataka kufanya kazi, anaweza fanya na mtu mmoja kama vile watu elfu mia moja.

Sasa, ukisimama nakufikiria hayo, kwa hakika ni ya kweli. Mungu hahitaji jeshi lote. Lile Mungu anahitaji ni mtu anayekubaliana na mpango Wake au kusudi Lake. Mungu anaweza kufikia lengo lake kwa kutumia mtu mmoja. Kile anahitaji ni mtu mmoja. Hilo ni fikira lenye kutisha na pia la kufurahia. Hilo fikira lilimweka Yonathani akawa mchangamfu mpaka akamwamusha yule aliyemchukulia silaha na akamwambia, “Wacha twende tuone kama Mungu anataka kupeana Wafilisti kwa Waisraeli leo.”

Walifunga safari ya imani. Ni kule kuwa na fikira zinazosema, “Wacha tuone kama Mungu anataka kufanya kazi leo. Wacha tuone vile Mungu anataka kufanya leo.” Bora tu ujiweke tayari akutumie. Lakini Yonathani aliweka msingi wa kujizatiti au kujikinga. Wakiwa njiani kuelekea kwa kambi ya Wafilisti akasema, “Lazima tujue kama Mungu yuko pamoja nasi. Kwa hivyo tukiwaona maadui wetu, nawatuambie, ‘Ninyi, watu! Mnafanya nini hapa? Ngojeeni, tutatelemka hapo na kuwafunza au kuwapa somo.’ Kwa kweli tutajua kuwa Mungu hataki kuwapeana Wafilisti kwetu leo. Lakini wakisema, ‘Ninyi, watu! kujeni hapa na tutawaonyesha jambo moja au mbili,’ ndipo tutajua Mungu anataka kuwapeana mikononi mwetu.”

Kwa hivyo waliacha swala hilo wazi. Hawakuwaingilia Wafilisti mara moja sababu walifikiria, “Mungu atakuwa pamoja nao na tutawashinda.” Kulikuwa ni muhimu kutahadhari. Hata kama sina uhakika, kutahadhari kidogo ni hekima. Bibilia imejawa na watu waliochukua hatua za imani, wakimpatia Mungu nafasi kutenda lile alilokusudi, kwa ufupi walijipeana kwa Mungu.

Miaka kadhaa iliyopita, tulisikia kuwa redio ya KWVE ilikuwa inauzwa. Wakati ule tulikuwa tunatangazia katika KYMS. Tulikuwa tukiwapa fedha na usaidizi waliohitaji iliwaanze hiki kituo. Raisi wa kituo hicho alikinunua ili alete redio ya Ukristo katika sehemu ya Orange County. The Word for Today ilikuwa ni chanzo cha hii stesheni. Lakini wakati kilipata mdhamini au uongozi mpya, waliamua kucheza mziki wa kisasa na wakakataa mafunzo ya Bibilia. Ndipo tukaenda kwa KBRT, lakini walikuwa na bei ghali sana.

Ndipo tukasikia kwamba KWVE ilikuwa inauzwa. Tukaamua, “Wacha tuwape bei yetu, na tuone vile Bwana atafanya. Kama Bwana anataka tuinunue, basi watakubali bei yetu.” Tulimpa Mungu nafasi ya kufanya kazi. Tulimwuliza Mungu, “Je, unataka kituo cha Kikristo sehemu hii ya Orange County, ambayo italeta hewani nyimbo za kuabudu na mafunzo ya Bibilia? Unahaja na hii?"

Tulikuwa hapo, tulikuwa na haja ya kujitokeza katika imani na kumpa Mungu nafasi. Ilikuwa ni jambo ya imani pekee. Tulikuwa tumeamua ya kwamba hatutashindana na kujadiliana nao juu ya bei. Tunawapa bei yetu peke yake. Ndipo wakasema, “Kuna wengine ambao wangependa kuinunua pia.” Nasi tukasema, “Sawa.” Jambo la kuzungumza na kubishana haitafanya kazi kama umejitolea kwa Bwana. Tuliomba, “Sasa, Bwana, ikiwa unaitaka, sawa, na ikiwa hauitaki, sawa pia.” Mwishowe, ilifanyika, ya kwamba walikubali bei yetu na kwa sasa KWVE ni yetu, na inasababisha huduma ya utukufu/sifa kwa Mungu. Inafurahisha kwa kuwa inaonyesha faida, ingawa tunalipisha fedha kidogo kulingana na vituo

vingine katika sehemu yetu. Tunaleta hewani huduma zingine za kidini kutoka kwa vikundi ambavyo tunashirikiana nao kwa bei nafuu, nakuwapa nafasi nzuri. Mungu ameibariki KWVE, lakini ni kwa sababu tulijitokeza kwa imani na kusema, “Mungu, kama ni jinsi unataka, tutajitokeza kwa imani na kuwapa bei yetu.”

Lakini pia kulikuwako na kituo cha televisheni kilichokuwa kinauzwa. Tuliwapa bei yetu kwa sababu tuliiona kama nafasi ya Bwana kuwaletea kituo cha Kikristo sawa na ile iliyokuwa kwa KWVE. Bei yetu haikukubaliwa na tukaiacha. Hatukujaribu kulazimisha na hatukutaka kwenda mbele za Bwana. Kama Mungu alipenda iwe yetu, angefungua njia. Sasa, tukajitokeza kwa imani na kuona vile Mungu anataka kufanya.

Miaka michache iliyopita, tuligundua ya kwamba tulihitaji mahali kubwa pa Shule ya Bibilia, iliyokuwa huko Twin Peaks Conference Center wakati ule. Ilikuwa inahitaji uwanja huo wote kujenga hii shule, hatukuweza kuendeleza shughuli za baraza pamoja na shule ya Bibilia. Wakati huo huo shamba kubwa la mifugo ambalo lilikuwa linamilikiwa na Los Angeles Rescue Mission lilikuwa tayari kwa uumiliki, katika mji Vista.

Tuliweka rubuni au malipo ya kwanza (Kuonyesha yakuwa tunania ya kitu fulani), lakini wanachama wa baraza la mji wa Vista waliokuwa wanaishi karibu pale wakaanza kupinga kupitia vyombo vya habari tusiweze kununua mahali pale. Ndipo tukaamua, “Si lazima tupiganie kwa hii,” na tukaachana na mahali hapo. Mmoja mwenye kuhusika na kuuza na kununua nyumba, uwanja na vitu vya aina hii, alipoona tangazo kwa gazeti kuwa tulikuwa tumeachanana na ile shamba, alitupigia simu, na kusema, alikuwa na mahali huku Murrieta Hot Spring ambayo haikuwa imewekwa hadharani kwa watu. Tulienda na kuiangalia na tukaona inaweza kuwa mahali pazuri pa shule ya Bibilia. Tuliweka bei yetu ya chini na tukasema, “Kama Bwana anataka iwe yetu, tutaipata.” Natuliipata!

Jambo la kushangaza ni kwamba, tulikuwa tunangojea mahali karibu na Calvary Chapel Costa Mesa kwa miaka mingi. Hii nyumba ya maofisi iliyokuwa na gorofa sita ilikuwa inahitaji $18 milioni. Miaka chache iliyopita, tuliwapa milioni $10 na wakakataa wakisema, "La, inahitaji zaidi kuliko hizo." Halafu mtu mmoja akaongea na muuzaji mkuu na wakakubaliana. Mwishowe tulipata mahali pale kwa $8.9 milioni. Tuliweza kuupata kwa $1 milioni chini ya bei yetu ya kwanza! Tuliweza kuona mkono wa Bwana kwa hayo.

Lakini jambo la kushangaza ni kwamba, kama tulinunua nyumba iliyokuwa karibu na kanisa kwanza, hatungeweza kununua Murrieta Hot Springs. Kwa hivyo tunaweza kuona mkono wa Mungu katika haya yote. Alitaka tupata mali hii yote na akapanga mpangilio na wakati ya kuwa tulikuwa tayari kununua Murrieta Hot Springs wakati iliuzwa kwa bei ambayo ilipendeza kwetu. Sasa tuko hapa na mali zote mbili.

Tulikuwa tunachukua hatua moja kwa moja kama za mtoto anayejifunza kutembea, lakini Bwana alitaka tuchukue hatua kuu. Wewe endelea mbele, na kama Mungu anafungua mlango, we endelea mbele tu. Kuna uwezakano wa kuogofya katika hatua ya imani. Unajitokeza nje kuona vile Mungu anaweza kufanya. Lakini tena kama Mungu hayuko ndani yake hatumpingi. Hatutii nguvu. Hatusukumi mambo. Kama Mungu yuko ndani yake, itafanyika kwa mpangilio wake. Itaenda barabara, na hatutaweza kujiaibisha.

Wakati Greg Laurie alichukua hatamu juu ya somo letu la Jumatatu usiku la Bibilia, Mungu alianza kumbariki sana na hata pia huduma. Tuliwaona vijana wakijitokeza kila jioni kuokoka. Nilimpigia Greg na kusema, "Greg kwa nini usitafute uone kama tunaweza pata wiki moja katika jumba la kufanyia tamasha la Pacific Amphitheater. Ni heri tupate nafasi kubwa tuone vile Mungu anaweza fanya kama tuna nafasi kubwa. Tunafurika pale usiku wa Jumatatu na hatuna nafasi ya kila mutu. Kwa nini tusijaribu jumba la kufanyia tamasha la Pacific Amphitheatre?"

Hii ilikuwa ni Aprili, naye Greg hakufikiria kuwa tulikuwa na wakati wa kutosha kufanya vile. Akasema, “Hatuwezi sasa!” Na nikauliza, “Kwa nini? Wacha tuone kama wana jumba ambayo i’wazi. Wacha tuone vile Mungu angetaka kutenda na nafasi kubwa.”

Tuliwapigia simu Pacific Amphitheater na walikuwa na jumba moja iliyokuwa wazi. Tuliamua kuiita, “Harvest Crusades.” Na tulifurahiya sana kwa maana jumba ile ilijawa na utukufu/sifa! Usiku ule wa mwisho, mahala pale palifurika, mpaka ikawabidi kufunga milango za nje. Waliweka vyombo vya sauti huku nje ili wale watu hawangeweza kuingia ndani wangesikia kutoka mbali. Ilikuwa ya kufana sana! Na ilikuwa na kuendelea kutoka pale lakini ilianzia tu kama hatua ndogo ya imani. “Wacha tuone lile Mungu angetaka kufanya. Wacha tumpe Mungu nafasi ya kutenda wacha tuchukue hatua.” Huenda tukapoteza hela kidogo, lakini vile msemo unaosema “usipochukua hatua, hutapata chochote.”

Mfano bora mwingine katika Agano la Kale wa hatua ya imani, ulionekana katika mji wa Samaria ilipokuwa imezingirwa na majeshi ya Washamu. Shida ilikuwa nyingi katika mji wa Samaria hata kichwa cha punda kikapata kuuzwa kwa vipande themanini vya fedha na kibaba cha mavi ya njiwa kwa vipande vitano vya fedha. Wamama walibadilika wakawa wala watu. Mama mmoja alilia mfalme amsaidie, lakini mfalme akamjibu, “Ninawezaje kukusaidia? Sina chakula kwa meza yangu.” Mwanamke alisema, “Mimi na mwanamke tulikuwa tumeahidiana ya kwamba tuwale watoto wetu, tumemla mtoto wangu kwanza, na sasa amemficha yule wake. Kwa hivyo mfanye amtoe wake ndipo tuweze kumla.” Mfalme akararua nguo zake na kusema, “Mungu nisaidie kama sitokata kichwa cha huyo nabii, Elisha!” Alikuwa anamlaumu Mungu kwa shida zake. (2 Wafalme 6:24-33).

Elisha alikuwa nabii wa kustaajabisha sana, na pia mtu wa kufana. Alikuwa na ufumbuo wa ajabu wa ki roho na ushirika wa ajabu na Mungu, ya kwamba alishangaa wakati Mungu hakumuonyesha mambo. Sasa,

mara kwa mara Mungu amenionyesha, lakini nashangaa kila wakati na pia hushtuka. Hufurahia! Hutendeka tu mara chache maishani mwako. Lakini Elisha alikuwa ameshikilia hilo sana na hata alishangaa wakati Mungu hakumuonyesha mambo. Mimi hushangaa wakati Mungu hunionyesha mambo.

Elisha alikuwa nyumbani na marafiki wakati alianza kujiongelesha, “Haa, unaweza kushinda hizo.” Haya marafiki wake wakamuuliza, “Nini inaendelea Elisha?” Naye akajibu, “Mfalme anatuma mtu aje hapa achukue kichwa changu. Kwa hivyo, akibisha mlango, ninyi mfungulieni na mmfinye kwa mlango. Kwa sababu miguu ya bwanake yuko nyuma yake.” Baada ya muda nadra, mlango ukabishwa, marafiki wa Elisha wakaufungua mlango na waka mweka yule mtu kwa mlango na kumshikilia hapo nyuma ya mlango. Ndipo mfalme akaja pamoja na akida au waziri mkuu wake na kusema, “Na sasa nimekupata wewe! Umesumbua Israeli kwa muda wa kutosha.” Elisha akamjibu, “Mimi siye yule anayeleta taabu Israeli. Wewe ndiye umeletea Israeli taabu kwa kuleta uabudu wa sanamu. Lawama ni kwako!”

Aliendelea kusema, “Usijali. Kesho saa hii, kipimo cha unga mzuri kitauzwa kwa shekeli na vipimo viwili vya shajiri kwa shekeli. Akida ambaye mfalme alikuwa anamtegemea aliyadharau hayo ambayo Mungu alikuwa ameahidi akisema, “Tazama kama Mungu angefanya madirisha mbinguni, je, jambo hili lingewezekana?” (2 Wafalme 7:2). Elisha akasema, “Angalia, wewe utaliona kwa macho yako, lakini hutakula.” (2 Wafalme 7:19).

Kwa nini waziri mkuu aliyumbayumba juu ya ahadi za Mungu? Kwa sababu aliuchukua mtazamo kwa fikira za binadamu, vile Mungu angefanya lile. Mara nyingi, hivyo ndivyo tunajipata taabuni. Hatuwezi kuona vile Mungu anaweza kufanya kazi. Tumejaribu kila kitu na tumeangalia kila njia na tumemalizia ya kwamba haiwezekani. Kama yule waziri, tunasema, “Kama Bwana angefanya madirisha ya mbinguni, je

jambo hili lingewezekana?" Elisha akasema, "Utaliona lakini hautakula." Mungu ataenda kutenda kazi yake, lakini kwa sababu ya kutoamini kwako, hautaweza kusaidika au kupata faida kutokana na kazi ya Mungu.

Hadithi yaendelea na watu wane wenye ukoma walioishi penye takataka karibu na lango la mji wa Samaria Kwa sababu ya ukoma, wao hawakuruhusiwa kuingia ndani ya mji. Waliishi kwa takataka iliyotupwa pale, lakini kwa sababu ya ukame katika huo mji walikuwa na njaa sana. Mmoja wao akamtazama mwingine akasema, "Mbona tukae hapa hata tufe?" (2 Wafalme 7:3). "Hakuna budi kwenda mjini. Kwa hivyo wacha twende kwa kambi ya Washami. Nani anaweza kujua, pengine watatuhurumia na kutupa mabaki ya mikate ili tuishi, au pengine watatuua. Tofauti iko wapi? Bado tutakufa tu!" Walichukua hatua ya imani ambayo iliwekwa kwenye tumaini kwamba pengine wangepata kipande cha mkate au wakose.

Nashangazwa kuwa makanisa mengi hayafikii mahali pale, kama vile watu wachache walioachwa wanatazamana. Ninashangaa hawasemi, "Sawa, kwa nini tukae hapa hadi tufe? Wacha tufanye kitu. Pengine itafaulu au halitafaulu, na hata kama haitafaulu, haijalishi, sababu bado tutakufa. Kwa hivyo wacha tuchukue hatua."

Ninatazama hatua nyingi za imani ambazo zimechukuliwa katika historia. Nani anajua vile Mungu angependa kufanya? Wacha tujitokeze. Wacha tuangalie. Wacha tumpe Mungu nafasi. Hadithi ya Elisha inaisha wakati Washami walisikia kelele ambazo walitafsiri kuwa magari ya farasi ya Wamisri. Walidhania kuwa Mfalme amewajiri Wamisri kama mamluki, na woga ukawaingia au ukawashika. Wakaanza kutoroka, na wakati wale wenye ukoma wanne walifika kwa hema ya kwanza, walipata chakula mezani na hakukuwa na mtu wa kula. Walikula na kuchukua vyote vya thamani ndani pale. Wakaenda kwa hema ya pili na wakapata jambo lile lile. Hakukuwa na watu lakini mlikuwa na chakula.

Walipokuwa wakichukua na kuficha hazina, mmoja wao akasema, "Wenzangu! Ni vizuri tukiwajulisha huko mjini jinsi Mungu ametenda. Tukificha haya na tujiwekee, madhara itatupata." Wakati walirudi mjini, walipaza sauti ya juu kwa mlinzi wa mlango, na kusema, "Kambi ya Washami iko wazi. Kuna chakula ya kutosha kwa kila mtu. Mjulishe Mfalme sasa ya kwamba si lazima watu walale njaa jioni ya leo. Wakati ujumbe ulimfikia Mfalme, alisema, "Nimtego. Hawa Washami wanajua ya kwamba tuna njaa, kwa hivyo walijificha watungojea kutoka nje ya mji. Halafu waje watuteke na kutuua. Usimwachilie yeyote nje ya mji. Funga milango yote ya mji."

Nafikiria kuhusu ya ajali na gharama ya kutoamini. Inatuepusha na kupokea hata wakati Mungu ametupa kwa wingi. Nimekutana na watu wengi ambao wanafikiria kama watu Waisraeli waliokuwa ndani ya mji. Husema, ni mtego wa aina fulani. Ni nzuri sana, haiwezi kuwa kweli. Wakati Mungu anafanya kazi, wanaogopa kujitokeza kwa imani.

Kuna kifungu katika Bibilia ambayo imenifunza mengi sana maishani mwangu. Inapatikana katika Mambo Ya Nyakati wa Pili. Sura ya kumi na nne inaanza na hadithi ya Mfalme Asa alipokuwa anaitawala Yuda. Alikuwa na miaka Ishirini na Tano wakati alipata kukikalia kiti cha enzi. Muda mfupi ulipopita, Wakushi wakaivamia nchi, waliungana pamoja na taifa zingine na wakawa na jeshi la wanaume milioni pamoja na magari ya farasi. Wakati Asa alipokea ujumbe huu wa uvamizi wa jeshi hiyo kubwa, aliomba kwa Bwana na akasema, "BWANA, hapana kuliko wewe aliye wa kusaidia, kati yake yeye aliye hodari, na yeye asiye na nguvu; utusaidie, Ee Bwana, Mungu Wetu; kwa kuwa sisi twakutegemea wewe, na kwa jina lako tumekuja juu ya jamii kubwa hii. Ee Bwana, wewe ndiwe Mungu wetu, asikushinde mwanadamu." (2 Mambo ya Nyakati 14:11).

Na sasa, napenda hii. Hakuwa akisema, "Mungu, nina mpango. Sasa, nataka ubariki huu mpango." Hakuwa akisema, "Sasa Mungu nimechunguza yote. Sasa, bariki ratiba yetu au mpangilio wetu." Haikuwa,

"Mungu kuja upande wangu." Badala, ilikuwa, "Mungu naja upande wako. Katika jina lako tunaendea. Asikushinde mwanadamu. Hawatanishinda, kwa sababu sina chochote. Sina uwezo wowote. Lakini, Bwana, hiyo Kwako haileti tofauti. Nitaenda kwa Jina Yako. Usiwaache wanishinde. Wanaweza nipiga, lakini usiwaache wakupige Wewe (Mungu)."

Hayo ni sawa na yale Yonathani alisema. Mungu hahitaji jeshi yote. Mungu anaweza kulitenda kwa mtu mmoja kama Mungu anataka kufanya kazi. Ni yale Paulo alinena katika Warumi 8:31, "Mungu akiwapo upande wetu, ni nani anayeweza kutupinga?"

Mungu alimpa Asa ushindi dhidi ya Wahabeshi. Asa alipokuwa akirejea, nabii wa Mungu akatoka kumlaki, naye Bwana akanena kupitia nabii, "Nisikieni Ee Asa, na Yuda wote na Benyamini; Bwana yu pamoja nanyi, mkiwa pamoja naye; nanyi mkimtafuta ataonekana kwenu; lakini mkimwacha ataawaacha ninyi." (2 Mambo ya Nyakati 15:2). Alipoanza uongozi kama mfalme wa Yuda, Asa alipata neno kuu kutoka kwa Bwana, "Bwana yu pamoja nanyi mkiwa pamoja naye; Mkimtafuta, mtampata. Ataonekana kwenu; lakini mkimwacha, Atawaacha hivyo."

Chini ya utawala wa Asa, ufalme ulifana sana na watu walibarikiwa sana. Lakini mwishowe alipokuwa ametajirika na mwenye ufanisi na wa kunawiri, ufalme wa juu Waisiraeli ukapanga kuvamia Yuda. Walianza kujenga mji mwenye kuta kuu kaskazini mwa Yerusalemu. Wakajipanga ili wavamie Yuda.

Asa alipowaona wakijenga kuta kuu, alitambua mpango wao kisha akatoa pesa kutoka kwa akiba au hazina ya Hekalu. Alizitumana zile hazina kwa Ben-Hadad, Mfalme wa Shamu, kuwaajiri Washami iliwa wavamie Waisraeli kutoka kaskazini. Washami waliteremka kutoka mlima ya Golani na wakaanza kupiga sehemu ya kaskazini ya Israeli. Mfalme wa Israeli alichukua jeshi lililokuwa likijenga kuta kuu na akawatuma

kasikazini kuwalinda kutokana na Washami. Jeshi lilipoacha miji yenye kuta kuu, watu wa Yuda walikuja na wakateketeza miji.

Ukiangalia matokeo yake, mpangilio wao ulifaulu. Asa hakuwa na shauku kufurahia mpango wake wa ajabu. Pesa zinaweza kutekeleza kazi, na alikuwa akifurahia yale ungefanya kama ungekuwa na pesa. Unaweza kuwaajiri Washami, wao ni mamluki, na unaweza kujizuia au kujikinga. Mpango wa vita ulifana sana.

Hanani nabii alikuja kwa Asa akamwambia, "Kwa kuwa umemtegemea mfalme wa Shamu, wala hukumtegemea Bwana, Mungu wako, kwa hiyo limeokoka jeshi la mfalme wa Shamu mkononi mwako. Je! Hao wakushi na walubi hawakuwa jeshi kubwa mno, wenye magari na wapanda farasi wengi sana? Lakini, kwa kuwa ulimtegemea Bwana, aliwatia mkononi mwako." (2 Mambo ya Nyakati 16:7-8). Wakati ulikuwa mchanga na haukuwa na nguvu na ulivamiwa na jeshi la Wakushi, ulimtegemea Bwana na Bwana alikuokoa au kukupigania. Tumaini lako lilikuwa kwa Bwana. Lakini sasa juu umeongezeka nguvu na uko imara unaamini uwezo wako. Haujui kuwa, "macho ya Bwana hukimbia-kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao, waliokamilika moyo kuelekea kwake." (2 Mambo ya Nyakati 16:9). Huu ndio ufunguo! Macho ya Bwana hukimbia-kimbia duniani yote kutafuta watu wenye mioyo iliyokamilika kwake, ili aweze kujionyesha mwenye nguvu kwa ajili yao.

Vile nabii alikuwa akisema ni kuwa Mungu anataka kufanya kazi. Mungu anakazi ambayo anataka kufanya, na Mungu anatafuta watu ambao wanakubaliana au wako na umoja kwa lile anataka, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili yao. Ufunguo ni kutambua ni nini Mungu anataka kufanya. Nimegundua ya kwamba jambo zuri la kufanya ni kujitokeza. Jaribu na uone. Pengine Mungu atafanya kazi. Wache tumpe nafasi. Lakini tena, kuwa na roho au nia hii "Kama haitawezekana, basi wacha tusiifinye na kujaribu kuifanya itendeke." Na tuzidi kuwa na huo uwepesi

wa kuweza kuachana na mradi wowote ule tunapoona haitendi makusudio yake. Tusiisukume ili ifanye kazi.

Tunaona wazo lile katika hadithi ya Esta wakati Mordekai alimtuma aende akamwone mfalme. Esta alisema, “Huwezi kuenda tu kumwona. Lazima uitwe. Unahatarisha maisha yako ukienda bila kuitwa.” Mordekai akamjibu, “Unadhania kuwa kama hii amri ikikubaliwa, wewe utaepuka? Pengine Mungu amekuinua kwa ajili ya wakati kama huo. Ukishindwa, msaada na wokovu utatokea kwa njia nyingine.”

Kwa maneno mengine, Mungu atatenda kazi yake. Mungu atalifikia kusudi lake. Nchi ya Israeli haiwezi kumalizwa, kwa sababu nikupitia kwao Masihi atakuja. Lazima uwe na uhakika ya kwamba kusudi la Mungu lazima lifanyike. Hata ukishindwa au ukiwezwa, wokovu utatokea kwa njia nyingine. Mungu atafanya kazi, lakini tuna nafasi ya kuwa chombo atakachoitumia kufanya kazi. Naamini kuwa mara nyingi hii ndio hali. Mungu ana kazi ambayo anataka kufanya. Anataka kuifanya na unaweza amua kuwa mshirika wa hiyo kazi. Unaweza kuwa chombo ukiamua. Kwa Esta, lilikuwa ni uamuzi mkuu kwenda kwa mfalme pasipo kuitwa. Asipoinua fimbo lake, Esta atauawa mara moja.

Miaka michache iliyopita kuna kitabu kiliandikwa kilichoitwa, “The Gospel Blimp.” Kiliandikwa na mpangilio jinsi kanisa linavyoweza kuongeza idadi wanaokuja kanisani. Ni jambo la kushangaza ukiona mikakati ya kulikuza kanisa, vyombo na mipangilio ambayo watu wanaweza kununua. Nia ilikuwa ni kuleta bendera na kuwakaribisha watu kuhudhuria kanisa. Waliacha hii bendera kupepea. Nia ilkuwa kuwajulisha watu ya kwamba pale kuna kanisa. Pia waliweka ujumbe, “Yesu Anakupenda” juu ya bendera.

Shida walizokuwa nazo kuiweka ile bendera jua ni hadithi ya kipekee. Mwishowe mawimbi yalikuja au dhoruba ilikuja na watu walikuwa pale wakijaribu kuishikilia. Walianza kubishana wenyewe kwa wenyewe,

na hii ilileta kugawanya kwa kanisa. Nusu ya kanisa ilienda ikikasirikia ile nusu ingine. Hii kweli ni juhudi za binadamu! Badala ya kuleta mapato au faida kwa kanisa, walipata hasara. Hapo mbeleni, walipoona kuwa lile bedera halikufanya kazi, wakasema, "Ooh! Lakini tulitumia $1500 kwa hili bendera. Lazima tuiweke pale juu." Wangesema lilikuwa ni kosa, na waliachilie litawanywe au lipeperushwe na upepo. Tusijaribu kushikilia, lile Mungu anataka lipeperushwe.

Miaka michache iliyopita, nilienda Lubbock, Texas kunena katika Kanisa la Kibaptisti la Kusini. Mchungaji alisema kuwa walikuwa wameamua hawataweka mpango wowote kwa kanisa kwa juhudi zao. Kwa ufupi, hawatajaribu kuleta uhai kwa vitu vilivyokuwa vinakufa.

Hili ni kosa ambalo kanisa imelitenda mara nyingi. Kuna wakati ambapo Mungu anatumia mpango fulani, lakini huo wakati unapita. Kwa bahati mbaya, watu wana uzoefu wakuskumia vitu uhai. Wanajaribu wawezalo ili ziendele mbele. Kwa mapenzi ya Mungu tumejifunza kuacha mambo yafe kifo cha kawaida badala ya kujaribu kuyasukuma kwa mitambo ya kuongeza uhai.

Ni dalili ya kudhoofika wakati unaporejelea ya kale na kusema vile Mungu alitenda, badala ya kuweza kusema, "Tazama yale Mungu anatenda leo." Badala ya kusikia yale Mungu ametenda, ni muhimu tuwe mmojawapo wa kazi ile. Tunatakiwa kushiriki na kujionea kazi za Mungu wenyewe. Ama, haitaendelea. Tunatakiwa kuifanya kila kizazi kinachofuata kama cha kwanza kwa kazi ya Mungu. Kwa njia hii, inaendelea kufanyika. Lakini tukisema, "Tazama vile Mungu alifanya, na vile Mungu alivyomtumia huyu mtu. Tazama vile Mungu amebariki yule mtu!" jihadhari. Wakati tujengapo maziara au mambo ambayo yanayotukumbusha yale Mungu alitenda zamani, hiyo ni siku ya huzuni, kwa sababu kila mmoja wetu anahitajika kutambua kazi ya Mungu kuwa hai na ina upya katika maisha yetu.

Kuna wakati Mungu alikuwa akitumia tamasha ya Jumamosi usiku hapa Calvary Chapel kwa njia ya ajabu. Hizi tamasha za Jumamosi ndio iliyokuwa chombo cha kueneza Injili. Mahali pale palifurika Jumamosi usiku. Tulikuwa na vikundi kadhaa vya uimbaji na mamia ya watoto walijitokeza kila jioni kumkubali Yesu Kristo. Kama ungewahoji watu katika California ya Kusini ni wapi watu walikuwa wanaokolewa, ungepata kuwa walikuwa wakiokoka katika Calvary Chapel usiku wa Jumamosi. Kuna wakati Mungu alikuwa anatumia tamasha hizi, lakini wakati ule ukapita. Miaka miwili iliyopita, kuna wale walisema kwamba walitaka kujaribu tamasha ya Jumamosi usiku tena. Kwa hivyo, nikasema, "Sawa, nendeni mfanye." Lakini wakati ulikuwa umepita. Kwa muda nadra, walijaribu kuzieendeleza, lakini ni kama Mungu alisema "La, huo wakati ulipita." Sasa hiyo sio kumaanisha haiwezi kuja tena mara nyingine, lakini badala kujaribu kuliendeleza huku ikifa pole pole, ni vizuri kulizima au kuliacha. Wacha liende. Wacha likufe. Usijaribu kuliendeleza.

Kwa hivyo, chukua hatua katika imani. Kama ikifanya kazi, furahi. Kama halifanyi kazi, tafuta jambo lingine. Mpe Mungu nafasi. Naamini bila shaka kumpa Mungu nafasi, na likifanya kazi, atukuzwe! Na kama halifanyi kazi, hujaingilia sana, hivi kwamba hauna uwezo kuliacha na kusema, "Kwa kweli, lilionekana kama wazo nzuri lakini, halikuwa?" Usijifunganishe nalo na kuingia ndani hivi kwamba huwezi kujitoa.

Ongozwa na Roho na usiogope kumfuata. Na kama ulianzia katika Roho, usitafute kufanyika kamilifu au haki katika mwili. Naliona hili kama shida, hata kwa wale tumekuwa nao toka mwanzo. Mungu amebariki huduma zao, lakini kwa bahati mbaya wamekuwa wenye mipango zaidi. Wameanza kuongoza mipangilio na kwa hili wanapoteza kitu cha maana sana. Kama ulianzia kwa Roho usitafute kufanywa kamilifu au haki kwa mwili. Hili ni kosa kuu.

Ninamshukuru Mungu kuwa ametupa wachungaji ambao walishika haya maono na kuchukua hatua ya imani. Ninawatazama wakichukua

hatua hizi za imani. Ni jambo la kusisimua kuona vile Mungu anabariki wakati tunachukua hatua na kumruhusu afanye lile atakalo, tukijipeana kama vyombo ambavyo anaweza kufanya lile atakalo kama ni mapenzi yake. Jambo la muhimu au ufunguo ni kujitolea anapo tuhitaji. Kwa hivyo, ajuaye ni nani kuwa macho ya Bwana huzunguka zunguka duniani kote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao, waliokamilika moyoni kuelekea kwake. Gundua mapenzi ya Mungu na ujitumbukize ndani yake. Wacha moyo wako upatane au uwe na umoja na nia ya Mungu, na utashangaa na yale Mungu atatenda na vile Mungu atabariki.